# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Nane – Tarehe 17 Aprili, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza Mkutano wetu wa Kumi na Moja, Kikao cha Nane.

Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu sasa aulize swali lake; kwa niaba yake Mheshimiwa Emmanuel Shangai.

Na. 94

**Ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Endala – Endamariek – Endabash – Karatu**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI K.n.y. MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Kibaoni – Endala – Endamarik hadi Endabash itajengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Jimbo la Karatu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza matengenezo katika barabara ya Kibaoni – Endala - Endamariek hadi Endabash. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilipeleka shilingi milioni 599.97 kwa ajili ya ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 40 kwenye barabara hiyo, na ujenzi wake umekamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali imetenga shilingi milioni 68 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi yenye urefu wa kilomita tano katika barabara hiyo na utekelezaji wake unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali itatenga shilingi milioni 213.02 kwa ajili ya kujenga madaraja mawili katika matengenezo ya sehemu korofi yenye urefu wa kilometa 10 pamoja na matengenezo ya muda maalum yenye urefu wa kilomita mbili katika barabara hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai swali, la nyongeza. Ahsante sana.

Waheshimiwa tuendendelee na Ofisi hiyo ya TAMISEMI, Mheshimiwa Dorothy Mbunge wa Temeke sasa aulize swali lake.

Na. 95

**Fidia kwa wananchi waliopisha maegesho ya malori – Kurasini**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi waliohamishwa kupisha maegesho ya malori eneo la Kurasini tangu mwaka 2015?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tamisemi Mheshimiwa Doctor Festo J. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa uthamini uliofanyika mwaka 2013 na ulipaji wa fidia kufanyika Mwaka 2015, Mwekezaji katika mradi huo alitoa shilingi bilioni 16.83 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa ajili kulipa fidia ambapo wananchi 165 waliofanyiwa uthamini ili kupisha mradi huo wamelipwa fedha zao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya malipo hayo kukamilika, wananchi 44 kati ya 165 waliolipwa fidia hawakuridhika na malipo yaliyofanyika, hivyo wakafungua kesi ya madai ya mapunjo ya shilingi bilioni 3.198 katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kupitia Shauri Namba 50 la mwaka 2016. Tarehe 28 Mei, 2021, Mahakama ilitupilia mbali shauri hilo baada ya wananchi hao kushindwa kuthibitisha madai yao, hivyo, hakuna fidia inayodaiwa na maeneo yaliyotwaliwa kupisha ujenzi wa maegesho ya malori katika eneo la Kurasini kwani wananchi wote wamelipwa kwa mujibu wa sheria, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dorothy swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwamba Mahakama imetupilia mbali suala hili, lakini je, hamuoni sasa iko haja ya Serikali na wananchi tukaweza kukaa pamoja tukapata uelewa wa pamoja ili wajue kwamba kweli walilipwa?

Swali la pili; je, yale maegesho ni lini sasa pataanza kujengwa maana bado pako wazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dorothy Kilave Mbunge wa Jimbo la Temeke kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaona umuhimu wa kukaa na wananchi hawa katika kujenga uelewa wa pamoja ili kuondoa sintofahamu ya baadhi ya wanaodai kufikiri kwamba hawajalipwa. Kwa hiyo nikuhakikishie kwamba

tutapanga utaratibu wa kwenda kuonana na wadai hao ili tuweze kuwapa uelewa wa pamoja wajue kwamba tayari walikwisha lipwa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, kujua lini ujenzi unaanza, naomba hili tulichukue kama Serikali tukalifanyie kazi tuweze kuona lini ujenzi huu unaanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora sasa namwita Mheshimiwa Stanslaus Mabula aulize swali lake.

Na. 96

**Serikali kutimiza masharti ya ajira kwa watumishi**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutimiza masharti ya ajira kwa Watumishi ikiwemo kuwapandisha madaraja na stahiki zingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza matakwa ya kisera, kisheria na miongozo mbalimbali ya

kiutawala na kiutumishi inayolenga au inayoelekeza Serikali katika kumtimizia masharti na haki za mtumishi wake. Aidha katika kufanya hivyo Serikali imeendelea na Utaratibu wa kupandisha madaraja watumishi ikiwemo utaratibu wa mpandisho wa mserereko. Pamoja na hilo Serikali imeendelea pia kuongeza kima cha chini cha mshahara na pia kuongeza *allowance* katika kazi za ziada na posho za muda wa ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo pia mwaka 2021/2022, Serikali ililipa shilingi bilioni 124.3 kwa watumishi 75,007 ikiwa ni malimbikizo *(arrears)* ya mishahara. Vilevile, Serikali iliongeza umri wa watoto wa watumishi wa umma kunufaika na huduma ya bima kutoka miaka 18 hadi miaka 21 ambapo katika kipindi cha mwaka mmoja jumla ya watoto 65,353 wamesajiliwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali; naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zoezi hili la upandishaji wa madaraja kwa maeneo mengine ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Mwanza inaonekana kwa mara ya mwisho ni tangu mwaka 2020/2021, na idadi ya watumishi walio kasimiwa kupandisha madaraja hailingani na waliopandishwa mpaka sasa;

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala la pili, kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu wa likizo kwa watumishi hasa kada ya Walimu;

Je, Wizara ina mpango ngani kuhakikisha kwamba Wizara ya Fedha sasa haitapunguza ile *ceiling* ya fedha za likizo zilizopo na badala yake waongeze zaidi?

Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na jambo la watumishi kupandishwa madaraja nimeeleza katika jibu langu la swali la msingi; kwamba Serikali imeendelea kupandisha madaraja ikiwemo utaratibu wa mserereko, ambao ndio maarufu sasa hivi ambao unaingiza kundi kubwa la wafanyakazi katika kipindi kimoja ili kuweza kuwapandisha katika madaraja stahiki. Pamoja na hilo pia nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali haina mpango wa kupunguza fedha za wafanyakazi katika masuala yanayohusu likizo kama alivyoeleza katika swali lake la pili. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, namwita Mheshimiwa Amina Daud Hassan Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na.97

**Kuhakiki Miradi ya *TASAF***

**MHE. AMINA DAUD HASSAN** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kufuatilia miradi ya *TASAF* iliyokamilika ili kuhakiki uendelevu wake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Daud Hassan, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuhakikisha kuwa miradi ya *TASAF* inakuwa endelevu, jamii huunda kamati ya matunzo na ukarabati ambayo jukumu lake ni kuweka sheria na taratibu za kusimamia matunzo na kuendeleza miradi hiyo. Mradi unapokamilika hubaki chini ya uangalizi wa wataalamu na *TASAF* wakishirikana na Halmashauri husika kwa kipindi cha miezi sita na baadaye mradi huo hukabidhiwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika ambayo huendelea na jukumu la usimamizi, uendeshaji na matengenezo kwa kushirikiana na idara au taasisi inayohusika na miradi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la nyongeza, ahsante Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali mazuri na nina maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaongezea ruzuku wawezeshaji wakati wa malipo wakati wa masafa marefu ya kuwafikia walengwa?

Na swali la pili; shilingi 24,000 ni kidogo sana kwa wakati huu tulionao; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaongezea ruzuku wanufaika wa mfuko wa *TASAF*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Daud Hassan kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la kwanza juu ya kuongeza ruzuku; nataka nimhakikishie Mheshimiwa Amina, kwamba Serikali iko katika mchakato ikijadiliana na wadau mbalimbali wakiwemo wahisani wetu juu ya maslahi na utaratibu mzima wa miradi hii ya *TASAF,* hivyo hii ni moja ya agenda ambayo inakwenda katika mjadala. Juu ya jambo la udogo wa pesa inayotolewa; niseme Serikali imesikia jambo hili na katika mjadala unaoendelea kama nilivyoeleza katika swala la kwanza la nyongeza, ni kwamba Serikali nao wanajadiliana kuona jinsi gani tunaweza kuangalia kuongezea ruzuku kidogo kwa wafaidika ili kuweka mazingira mazuri ya wao kufaidika na mradi huo; ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi kuuliza swali la nyongeza. Katika halmashauri ya Wilaya ya Manyoni tulitenga kujenga Zahanati katika Kijiji cha Udimaa ambacho hakina Zahanati kupitia mradi wa *TASAF*.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Zahanati ya Udimaa kwa kupitia mradi wa *TASAF?* Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Chaya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi inaibuliwa na wananchi, na sisi kama Wizara au Ofisi ya Rais inayosimamia miradi ya *TASAF* majukumu yetu ni kuchukua miradi hiyo na kuingiza kwenye mipango ya bajeti. Pale itakapopatikana bajeti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi wake huo tutakwenda kuufanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunashukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge wa Chambani sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Kujenga upya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani**

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukijenga upya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Mambo ya Ndani Mheshimiwa Sagini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani ni chakavu na halifai kwa matumizi ya kutoa huduma za polisi. Mwezi Desemba, 2022 Serikali ilitoa kiasi cha fedha shilingi milioni 700 kwa ajili ya kujenga kituo cha polisi kipya cha Daraja B eneo hilo na taratibu za ujenzi

zimeshaanza. Ujenzi unafanywa na Kikosi cha Ujenzi cha Polisi na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti, 2023. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeza sana Serikali kwa hatua ambayo wamechukua na nina masuala mawili tu ya kuuliza.

(a) Kwa kuwa fecha zilitolewa Desemba, 2022 na mpaka leo imefika hatua ya kusafisha kiwanja hicho, je, ni tatizo gani ambalo linasababisha hilo?

(b) Ni lini Mheshimiwa Waziri atakwenda kuangalia ujenzi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohabed Mwinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kuhusu tatizo la kuchelewa, ni kweli umetokea uchelewaji baada ya kubaini kwamba utaratibu uliokuwa umewekwa wa kutumia *force account* ulikosewa na baadhi ya watekelezaji wa jukumu hili. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi alianza mfumo wa kuwaelimisha Makamanda wote wa Polisi wa Mikoa juu ya mfumo huo unaofanya kazi ili wauzingatie wakati wa utekelezaji, kwa hiyo ndio sababu ya kuchekelewesha. Sasa hivi wote umeshapitishwa ndiyo maana utekelezaji unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu lini nitakwenda, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunao utaratibu wa kufatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaofanywa

na maofisa wetu lakini na sisi viongozi wa kisiasa tunapata nafasi tunaenda huko. Kwa hiyo itakapokuwa pengine Bunge hili linamalizika kabla ya mwezi Agosti Mbunge akiwa tayari niko tayari kuongozana nae kuangalie maendeleo ya ujenzi huo. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo chetu cha Polisi cha Somanga kimechakaa sana.

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo kipya katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndulane kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba ni kweli kituo cha Somanga ni cha muda mrefu na kimechakaa kama ilivyokuwa vituo vingi maeneo mbalimbali nchini. Tutakachofanya kabla ya kuki-*condem*n kituo hiki kwamba hakifai kwa matumizi ya binadamu tutaenda kufanya tathmini ya uchakavu wa kituo hiki. Iwapo itaonekana kuwa gharama za ukarabati ni kubwa au zinakaribia kulingana na gharama za ujenzi kitaingizwa kwenye mpango wa ujenzi wa kituo kipya, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Kituo cha Makambako kimewakuta wananchi na wananchi walitoa eneo hilo kwa roho nyeupe;

Je, ni lini sasa Wananchi hao watalipwa ela zao kwa sababu mwaka jana Rais alipopita mwezi wa nane aliahidi na Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri alikuwepo, ni lini watalipwa wananchi hao ili wasiteseke fedha zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kweli kwamba kituo cha Makambako kimekuta wananchi na uthamini ulishafanywa, na kuna takriban shilingi milioni 240 kwa ajiri ya kuwalipa fidia na kwa maagizo ambayo yameshatolewa na Mheshimiwa Rais wetu. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni ahadi ambayo lazima itekelezwe. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafatilia Wizara ya Fedha ili kupata fecha hizo za kulipa fidia ili wananchi hawa waweze kupata haki yao wapishe ujenzi wa kituo hiki, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, sasa namwita Mheshimiwa Anatropia Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 99

**Sheria za Tanzania kuhusu mahusiano ya jinsia moja**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, Sheria za Tanzania zinasema nini kuhusu mahusiano ya jinsia moja?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Katiba na Sheria Mheshimiwa Gekulu, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, na kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Theonest kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Tanzania haziruhusu mahusiano ya jinsia moja. Kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria ya Ndoa kinatafsiri ndoa ni mahusiano ya hiyari kati ya mwanaume na mwanamke. Aidha kwa mujibu wa kifungu cha 154 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 kinabainisha kuwa kufanya mapenzi kinyume na maumbile ya jinsia ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni kifungo cha maisha jela au kifungo kisichopungua miaka 30 jela.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sheria iko wazi kuzuia mahusiano na mapenzi ya jinsia moja, lakini tunaona kwenye vyombo vya habari watu wakitangaza na kujinasibu kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Je, ni hatua kiasi gani zimefanyika kufikishwa Mahakamani ili tuweze kuzibiti kwa mujibu wa sheria? *(Makofi)*

Swali langu la pili, licha ya kuwepo kwa Sheria bado tumeona utekelezaji wake, pengine utekelezaji ndiyo umesababisha haya tunayoyasema.

Je, ni lini Serikali italeta mabadiliko ya sheria ili kila anayejihusisha, mwenye dalili na mwenye kufikiria aweze

kuchukuliwa hatua ili tuweze kulinda maadili ya nchi yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia Theonest kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amependa kufahamu kwamba makosa hayo yanapojitokeza na watu wakijinasibu hadharani kwenye vyombo kama hatua zimekuwa zikichukuliwa? Hatua zimekuwa zikichukuliwa na ninyi ni mashahidi kwenye Bunge hili tumekuwa tukikemea jambo hili, nitoe rai kwa jamii kwamba jambo hili si la Serikali peke yake ni la jamii kwa umoja wetu ndiyo maana pale zinapokuwa zimebainika tumekuwa tukichukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua kama tunaweza kufanya marekebisho ya sheria hizi? Sheria hizi zinafanya kazi kuhakikisha kwamba wale wanaobaninika wanachukuliwa hatua na ninyi ni mashahidi ndugu zangu hivi karibuni mahakama zetu zimetoa hukumu kwa watu ambao wamebainika wamefanya hivyo na wamekiri na wamefungwa miaka zaidi ya thelathini. Kwa hiyo, ni jukumu letu sote. Hata hivyo, pale ambapo utafiti utakuwa umefanyika Mheshimiwa Spika alielekeza kwamba utafiti wa kina ufanyike ili matendo haya yakibainika basi tuwe na kauli ya pamoja. Wakati huo ukifika kama marekebisho ya sheria yatahitajika Serikali ipo tayari.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Niabu Waziri kwa majibu. Namwona Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kuongeza katika majibu yake mazuri.

Kwanza, hakuna matangazo ya mapenzi ya jinsia moja kwenye *main media* ambayo yanaruhusiwa na Serikali iko *very strictly* kwenye hili. Tulikuwa na chanagamoto kwenye *online media* ambayo mpaka sasa hivi jumla ya tovuti 334, akaunti za *Facebook* 361, *Instagram* 168, *Twitter* 12 na vikoa vya *gay* zaidi ya 2,456 vimefungiwa kwa sababu ya hatua hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na hatua ambazo Serikali inachukua kufungia baadhi ya hizi *online platforms* lakini nadhani jambo hili bado liwe ni jukumu la jamii kuchukua hatua kuanzia kwenye familia na kuendelea sasa kwenye maeneo mengine. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge tunaingia sasa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, namwita sasa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 100

**Uboreshaji wa bei ya ardhi inayotwaliwa migodini**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaboresha bei ya ardhi inayotwaliwa na Migodi ili iendane na thamani ya ardhi ya eneo husika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya soko la ardhi huandaliwa kwa kuzingatia Kifungu Na. 70 cha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016 pamoja na Kanuni Na. 53 ya Kanuni za Uthamini na Usajili wa Wathamini za mwaka 2018. Kanuni hiyo imeelekeza bei ya soko la ardhi kuzingatia visababishi vinavyoathiri bei ya soko la ardhi kati ya eneo moja na jingine na namna ya kufanya tafiti kwa kukusanya taarifa za soko la ardhi katika maeneo mbalimbali. Aidha, Kifungu cha (2) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kimetafsiri kuwa petroli na aina zote za madini yanayopatikana chini ya ardhi siyo sehemu ya ardhi bali ni mali ya umma na hivyo umiliki wa ardhi hutolewa tofauti na leseni ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi na mali ili viendane na wakati, viwango vya bei ya soko la ardhi vimeboreshwa kwa kuzingatia sheria na kanuni za ardhi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nina maswali mawili ya nyongeza. Wananchi wa maeneo yote ambayo yanazunguka mgodi wa *Barrick North* Mara hawajui kwamba ardhi ndiyo ya kwao kilichopo chini siyo cha kwao.

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kwenda kufanya mkutano katika eneo lile ili kutoa elimu hii kwa wananchi ili

wajue kwamba hawahusiki na dhahabu iliyoko chini ya ardhi ile?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, pamoja na manung'uniko makubwa sana ya eneo hilo ni nili wananchi wa eneo la Nyamichele, Murwambe, Nyabichune na Kiwanja watalipwa fidia yao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Waitara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwenda kwenye eneo, yaani uwandani Wizara tuko tayari kwenda na tutawasiliana nae kwa ajili ya kupanga utaratibu wa jinsi ya kufika kule kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia ya maeneo aliyoyataja nitawasiliana nae kujua viwango vya hatua zilizofikiwa hadi sasa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati, namwita Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 101

**Utafiti wa uvunaji mafuta Ziwa Tanganyika**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza: -

Je, nini matokeo ya utafiti wa mafuta uliofanyika katika Ziwa Tanganyika na lini mafuta yataanza kuchimbwa?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma, Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa mafuta katika Ziwa Tanganyika umegawanyika katika vitalu viwili ambavyo ni Kitalu cha Kaskazini na Kusini. Kitalu cha Kaskazini kina ukubwa wa kilomita za mraba 9,430 ambapo mwaka 2015/2016, *TPDC* iliweza kukusanya, kuchakata na kutafsiri taarifa za uvutano wa sumaku ili kugundua maeneo yenye uwezekano wa kuwepo kwa mashapo ya kuhifadhi mafuta. Kitalu cha Kusini kina ukubwa wa kilomita za mraba 7,163 ambapo *TPDC* kwa kushirikiana na Mwekezaji - Kampuni ya *Beach Petroleum* waliweza kukusanya, kuchakata na kutafsiri taarifa za uvutano wa sumaku ili kubaini maeneo yenye uvutano na uwezekano wa kuhifadhi mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa viashiria vizuri vya uwepo wa mafuta katika vitalu vya Ziwa Tanganyika, matokeo ya mwisho kuhusu uwepo wa mafuta katika Ziwa hilo bado hayajapatikana kwa kuwa kazi ya utafiti bado inaendelea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninataka kujua kwa sababu viashiria vya uwepo wa mafuta

kwenye Ziwa Tanganyika vimeonekana katika utafiti wa awali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha utafiti huo ili kuweza kupata taarifa kamili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni lini wananchi wa Kigoma watarajie kupata taarifa za mwisho za utafiti huo ambao umechukua zaidi ya miaka mitano?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika swali la kwanza, mbinu ambazo zinafanywa na Serikali na jitihada zinazofanywa na Serikali kama mnavyofahamu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifungua sana Tanzania kwa ajili ya wawekezaji, nasi Wizara ya Nishati tumekuwa tukishiriki katika maonesho mengi ya Kimataifa kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji kuja nyumbani kufanya kazi pamoja nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazofuata za utafiti ambazo zimebakia za *3D* ni za gharama kubwa na Serikali imekuwa ikitafuta mbia wa kimkakati wa kushirikiana nae kwenye maeneo hayo ili kukamilisha utafiti huo ambao unatakiwa kufanyika. Mara tu baada ya kumpata na taarifa zikapatikana vizuri basi Ndugu zetu wa Kigoma na Watanzania kwa ujumla watapewa taarifa ya nini kimepataikana na lini uchimbaji wa mafuta katika Ziwa Tanganyika utaanza kufanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, namwita Mheshimiwa Goefrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 102

**Ujenzi wa Stendi Mpya ya Mji wa Masasi**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi mpya ya Mji wa Masasi ikiwa ni mradi funganishi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Masasi hadi Mnivata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Kesekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa ushirikiano wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara ya Mnivata – Newala – Masasi yenye urefu wa kilomita 160. Taarifa ya uchambuzi wa zabuni za kumpata mkandarasi zimekamilika na kuwasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* kwa ajili ya kupata idhini ya kuendelea na hatua ya kusaini mkataba *(no objection)*. Kwa vile mradi wa ujenzi wa Stendi mpya ya Mji wa Masasi ni moja ya miradi itakayotekelezwa kama mchango kwa jamii chini ya mradi wa ujenzi wa barabara hii, kazi za ujenzi wa stendi

mpya ya Mji wa Masasi itaanza baada ya mkataba wa ujenzi wa barabara kusainiwa na kazi za ujenzi kuanza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE.** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ninataka nijue ni lini basi Serikali ina uhakika wa kupata hii *(No objection)* kutoka kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika ili tujue kwa uhakika kabisa ni lini tutaanza utekelezaji wa mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ninataka kufahamu ni lini Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Wilaya ya Temeke itajenga stendi mpya kwa ajili ya mabasi ya kutoka Mtwara, Lindi na Ruvuma yanayoingia Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya *Dual Carriage Way* ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mkuranga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu, Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu za manunuzi zinakwenda vizuri na ni matumaini yetu kwamba kama wenzetu watakwenda kama tulivyopanga tunategemea tutapata *(No objection)* kwa sababu taratibu zote karibu zimekamilika. Sasa ni lini? Kwa kweli tutanategemea wenzetu wa *African Development Bank* watakavyokuwa wamefanya kazi yao kwa uharaka na kutoa hiyo *(No objection)* na sisi tutaanza kutangaza hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kujenga stendi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama wizara kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI ambao hasa ndio wanaoshughulikia stendi hizi za mijini, tutakaa pamoja tuone uwezekano wa kujenga hiyo stendi na hasa tu nikimhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa upande huo tayari tuna utaratibu wa kuja na mpango wa kujenga *dual carriage way* ya kutoka Mbagala – Kongowe na ikiwezeka mpaka Vikindu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE D. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, je, ni lini barabara ya kutoka Waso kwenda Loliondo yenye urefu wa kilometa 10 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Arusha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ilikuwa ni ahadi na agizo la Mheshimiwa Rais, hivi tunavyoongea tayari tenda ilikwishatangazwa ya kujenga kilometa hizo 10 za kutoka Waso hadi Loliondo kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Tadayo swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii, kwa kuwa ipo ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa stendi ya kisasa katika Mji wa

Mwanga, swali langu ni je, ni lini ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa kwa wananchi wa Mwanga? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Tadayo, Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Tadayo aniruhusu niweze kupata maelezo sahihi ya kuhusu utekelezaji wa hii ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa *TANROADS* kujenga hii stendi ya kisasa katika Mji wa Mwanga baada tu ya kutoka kwenye kipindi hiki. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu swali la Nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya kutoka Bariadi – Itilima – Meatu – Sibiti mpaka Singida iko kwenye ilani. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ni sehemu ya Barabara ambayo ni ya kutoka Maswa – Sibiti Kwenda Haidong ambayo ipo kwenye mpango wa *EPC+F* na nimekwisha itolea maelezo mengi kwamba tayari taratibu zinaendelea na sasa tayari upande wa Wizara ya Ujenzi

tumemaliza sasa tumekwishapeleka kwa wenzetu Wizara ya Fedha kuweza kupitia mapendekezo yetu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Mwenge kuelekea Bagamoyo imekuwa na msongamano mkubwa na kusababisha Shughuli za kiuchumi Mkoa wa Dar es Salaam kusimama. Ni lini sasa Serikali itajenga barabara ya Mabwepande kuelekea Mbezi Jimbo la kibamba ili kuweza kupunguza foleni hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya kutoka Mwenge kwenda Mabwepande ni *BRT number Four* ambayo iko katika hatua za manunuzi, lakini barabara aliyoitaja itakuwa ni moja ya barabara za kupunguza msongamano lakini pia kwenda kwenye hii stendi mpya na iko kwenye mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo sasa aulize swali lake.

Na. 103

**Fidia kwa wananchi wa Sitalike**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Kata ya Sitalike waliopisha ujenzi wa barabara ya Sitalike hadi Mpanda Hotel watalipwa fidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Kata ya Sitalike hadi Mpanda wanaodai fidia ni wale walio kwenye eneo la nyongeza la upana wa hifadhi ya barabara la kutoka mita 22.5 kwenda mita 30.

Mheshimiwa Spika**,** Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuwalipa fidia wananchi hawa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunpa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi hawa wamesubiri muda mrefu, wamepisha barabara hii takribani sasa tokea 2012 ina maana sasa hivi takribani miaka 11 mpaka leo hawajapata fidia zao na kuna wengine

wamefariki. Je, kupitia hii kero Waziri yuko tayari kuja kuzungumza na wananchi wa Kata ya Sitalike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa hii imekwisha kuwa shida. Je, Serikali inajipangaje sasa kupitia tatizo hili la fidia kuhakikisha kabla hawajawatoa watu wahakikishe wamewalipa kwanza ili isiwe kero kupitia Serikali?

**MWENYEKITI** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo yote kwa pamoja kwa ifuatavyo :-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la fidia hasa kwa mita 7.5 limekuwa linajitokeza mara kwa mara, na mimi napenda tu nitumie nafasi hii kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba hii ni Sheria ya kuongeza upana wa barabara kutoka Mita 45 kwenda mita 60 ya mwaka 2007. Kufanyika huku kulikuwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na hifadhi kubwa ya barabara ili tunapotaka kufanya shughuli zozote ikiwa ni pamoja na kuongeza upana wa barabara ama kupitisha mifumo mingine yote iwe ya maji, ya mikongo ya mawasiliano tuweze kuwa na hifadhi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na hifadhi kubwa ya barabara ili tunapotaka kufanya shughuli zozote, ikiwa ni pamoja na kuongeza upanda wa barabara, ama kupitisha mifumo mingine yoyote iwe ya maji, na mikongo ya mawasiliano, tuweze kuwa na hifadhi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tutakuja na taarifa sahihi ya utaratibu ambao tutaufanya kwa sababu ni nchi nzima ambapo tumeongeza huo upana wa barabara,

namna bora na sahihi ya kuweza kuchukua hayo maeneo na kuwalipa fidia, ama kama kutakuwa na maelekezo mengine ambayo Serikali itakuja kuyatoa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Anna Lupembe pamoja na Wabunge wengine wote ambao wana changamoto hizo kwenye majimbo yao kwamba, Serikali itakuja na utaratibu mzuri wa namna bora ya kufidia wananchi ambao barabara imewafuata, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopisha barabara ya *Bypass* ambayo ni mpya ya Uyole mpaka Songwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyotaja Mheshimiwa Njeza Mbunge wa Mbeya Vijijini, ni mpya, inajengwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zinaendelea na barabara ambazo tunazijenga wananchi watafanyiwa tathmini na wakati tunaanza ama kabla hatujaanza, wananchi hawa watalipwa fidia zao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Regina Ndege, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Ngoni, Himiti, Singe hadi Komoto ambao wamepisha ujenzi wa *Bypass* katika Mji wa Babati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Regina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu mengine, ni kwamba wananchi hawa wameshafanyiwa tathmini na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuweza kuwalipa fidia yao wananchi ambao wamepisha mradi huu wa barabara wa *Bypass* katika Mji wa Babati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA RAMAMDHANI SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa mradi wa *bypass* unaanzia Kata ya Kisaki - Nyamikumbi - Unyambwa mpaka Utipa umeshafanyiwa upembuzi yakinifu: Ni lini ujenzi huu utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilishafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa *Bypass* ya Singida. Kitakachofanyika sasa ni kufanya mapitio upya na kupata gharama ya sasa ya ujenzi. Kwa hiyo, barabara hii baada ya fedha kupatikana tutaanza kuijenga ili kupunguza msongamano katika Mji wa Singida, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hawa, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali imekuwa na changamoto kubwa sana ya ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha miradi mbalimbali ya maendeleo. Je, Serikali haioni sasa kuna

umuhimu wa kufanya tathmini baada ya kuwa mmepata fedha ili kuondoa usumbufu kwa wananchi ambao wanapisha miradi kwa hiari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya miradi ya barabara, fidia inakuwa ni sehemu ya gharama ya ujenzi wa hiyo barabara. Kwa hiyo, tunapokuwa tunafanya ujenzi ni pamoja na fidia. Kwa hiyo, tunaposema gharama ya barabara hii, ni pamoja na fidia ya wananchi ambao wanapisha hiyo miradi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa ya swali dogo la nyongeza. Kutokana na mvua kubwa inayonyesha Bonde la Ziwa Rukwa, madaraja takribani sita yamesombwa na mafuriko: Je, ni lini kauli ya Serikali juu ya kurudisha mawasiliano kwa dharura katika eneo hili la Bonde la Ziwa Rukwa ambalo na Mheshimiwa Naibu Waziri unalijua fika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika kipindi cha mvua, barabara nyingi huharibika na madaraja mengi kusombwa likiwemo daraja la Mheshimiwa Sangu ambalo ni

eneo la bondeni. Naomba tu nichukue nafasi hii kumjulisha ama kumpa maelekezo Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Rukwa ahakikishe kwamba anapeleka timu ya wataalam kuanza kufanya tathmini na ikiwezekana kurudisha mawasiliano ya muda na pia aweze kuleta taarifa Makao Makuu kuomba uwezesho wa fedha ili kurejesha mawasiliano haya ya kudumu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, namwita Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Kamonga.

Na. 104

**Kuadimika kwa mbolea na kusababisha hasara**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA K.n.y. MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, nini kimesababisha mbolea kuadimika na kuleta hasara kwa Wakulima na Wawekezaji nchini katika msimu wa mwaka 2022/2023?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi katika msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023 hatukuwa na uhaba wowote wa mbolea. Vilevile Serikali haijapokea malalamiko yoyote

kutoka kwa wakulima na wawekezaji yanayohusu kupata hasara kutokana na kuadimika kwa mbolea. Changamoto pekee ilijitokeza ilikuwa ni mwamko mkubwa wa wakulima kuhitaji kununua mbolea kuliko uwezo wa mtandao wa mawakala, ambapo Serikali imeendelea kuipatia ufumbuzi na kuongeza idadi ya mawakala kutoka 1,392 mwezi Agosti, 2022 hadi 3,265 mwezi Machi, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mahitaji ya mbolea kwa msimu wa 2022/2023 yalikuwa ni tani tani 667,730 na hali ya upatikanaji wa mbolea hadi kufikia mwezi Machi, 2023 umefikia tani 748,890 sawa na asilimia 112 ya mahitaji ya mbolea ndani ya nchi, ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Mpina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa tumbaku? Hilo swali la kwanza. Swali la pili: Je, Serikali inajipangaje kuhakikisha wakulima wanapata mbolea mapema ili kuweza kuwaruhusu mazao yote yale ya umwagiliaji yaweze kupata mbole kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mpango wa msimu uliomalizika, wakulima wa zao la tumbaku hawakuwepo katika mpango wa ruzuku kwa sababu katika

utaratibu wa manunuzi ya pembejeo kwenye sekta hii ya tasnia ya tumbaku wamekuwa na utaratibu maalum ambao ulianza kabla ya mfumo wa ruzuku. Hata hivyo, tumeendelea kukaa nao kuangalia pia utaratibu bora ili na wao waweze kunufaika na utaratibu wa ruzuku ambao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la kuhusu mbolea kupatikana mapema; tumeshakaa na waagizaji na wazalishaji wa mbolea wote hapa nchini kuhakikisha kwamba kuanzia mwezi wa Saba mbolea ianze kuingizwa nchini ambayo itawakuta wakulima wakiwa bado na uwezo wa kununua kwa kuwa watakuwa wamevuna ili wakulima wetu itakapofika kipindi cha kuanza msimu mbolea iwepo yote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumebaini upungufu katika msimu uliopita, tumeyarekebisha, tutahakikisha kwamba wakulima wanapata mbolea kwa wakati katika msimu ujao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA HASSAN TAUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu ina mifugo mingi ya kutosha, hivyo uwezekeno wa kuwa na mbolea ya samadi ni mkubwa, nini mkakati wa Serikali katika kuboresha na kuhamasisha matumizi ya mbolea ya samadi ili ilete tija? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kwa hapa Dodoma tunacho kiwanda cha mbolea kinaitwa *ITRACOM* ambacho kinazalisha mbolea inayoitwa *Organo Mineral* ambapo zaidi ya asilimia 50 wanatumia samadi na imekuwa kichocheo kikubwa na soko la uhakika kwa wafugaji wetu wengi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ilikuwa ni mkakati wa Serikali, na kiwanda kipo hivi sasa na kinatumia malighafi hiyo kama sehemu ya kutengeneza mbolea hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Venant, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Uchache wa mawakala ulileta usumbufu wa upatikanaji wa mbolea kwa msimu uliopita. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka mawakala angalau kwa kila kijiji ili wasiendelee na usumbufu walioupata wakulima kwa msimu uliopita? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya changamoto ambazo pia tulizibaini wakati wa msimu uliopita ilikuwa ni hiyo ya uchache wa mawakala. Tumeshatoa maelekezo kupitia *TFRA* kuongeza idadi ya usajili wa Mawakala ili wakulima wapate mbolea katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tumeamua kuyatumia maghala yote makubwa ya Serikali kwa ajili ya uhifadhi na kupeleka mbolea karibu na wakulima; na tatu, tumeruhusu

Vyama vya Ushirika pia kuwa sehemu ya Mawakala ili kufanya huduma hii ifike kwa ukaribu zaidi kwa wakulima

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Uhalisia wa upatikanaji wa mbolea kwa wakti kwa wakulima wetu bado ni changamoto kubwa; na inasemekena mbolea hizi zinatumika kusafishia madini kwenye migodi. Sasa nilitaka kujua, ni Serikali itafanya tafiti za kina kujua matumizi ya ziada ya mbolea hizi nje ya kilimo ili kuweza kuwa na bajeti halisia ya kuwafikia wakulima kwa wakati kulimo ilivyo hivi sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya msingi ya mbolea yanafahamika, ni kwa ajili ya kilimo. Kama kuna jambo lingine la ziada kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, sisi na wenzetu wa madini tutakaa tushirikiane ili kuweza kulifanyia utafiti wa kina na kuweza kupata majibu stahiki katika eneo hili ili mwisho wa siku tuwe na mbolea kwa mahitaji halisi yanayohitajika katika kilimo chetu cha msingi Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti maalum, sasa aulize swali lake.

**17 APRILI, 2023**

Na. 105

**Kubaini madawa na vihatirishi vyenye madhara**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mapitio ya kubaini madawa na vihatirishi vinavyosababisha madhara na vinaendelea kutumika katika Kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania hutekeleza utaratibu wa kubaini viuatilifu na vihatarishi vinavyosababisha madhara kwa mazao, mimea na afya ya binadamu na wanyama. Utaratibu huo hufanyika kulingana na kifungu cha 54 cha Sheria Na. 4 ya Afya ya Mimea ya mwaka 2020 kinachompa Mamlaka Msajili wa viuatilifu nchini kufuta usajili wa viuatilifu vinavyosababisha madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 hadi 2021, Serikali ilifanya mapitio ya kubaini viuatilifu vyenye madhara makubwa kwa afya ya binadamu na mazingira vijulikanavyo kama *Highly Hazardous Pesticides*. Mapitio hayo yalibaini aina ya viuatilifu 44 vyenye viambata amalifu vyenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hatua hiyo, Serikali kupitia *TPHPA* imeanza kuchukua hatua za kusitisha matumizi

ya viuatilifu 44 vilivyobainika na inaendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara katika maghala na maduka ya viuatilifu ili kubaini uwepo wa viuatilifu vingine vyenye madhara.

**MWENYEKITI:** mheshimiwa Asha, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Serikali; pamoja na kitu kizito alichopigwa nacho Mheshimiwa Naibu Waziri jana Mkapa, lakini anaweza kutoa majibu ya kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imefanya uhakiki kwamba viuatilifu hivi 44 vilivyobainishwa vimeweza kutokomezwa na kwamba *notice* ya katazo au ya ku-*deregister* au zuio inabainika kwa uwazi na kwa ufasaha kabisa kwa wanunuzi, watumiaji na wanaohusika wote? *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, swali lingine: Je kuna mpango gani wa Serikali kupima mboga mboga zinazoingia sokoni na kuwajulisha watumijai na walaji kama vile tunavyofanya kwa mazao yanayouzwa nchi za nje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya Afya ya Mimea ya Mwaka 2020, ni wajibu wa kimsingi wa mamlaka kuhakikisha kwamba inafanya kaguzi za mara kwa mara ili kuweza kubaini viuatilifu ambavyo vimesitishwa na kuweza kuchukua hatua

sambamba na kutoa taarifa kwa watumiaji ili isiweze kuleta madhara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la kuhusu upimaji wa mazao ya mboga mboga, Serikali inapima uwepo wa masalia ya viuatilifu vilivyotokomezwa katika mazao yote. Hivi sasa tumenunua *Rapid Test Kit* ambayo pia itasaidia kupima masalia ya viuatilifu katika mazao ya mboga mboga ili kuweza kumlinda mtumiaji. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia tunahamasisha na kilimo hai, kuondokana na changamoto hizi ambazo zinajitokeza na matumizi ya viuatilifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kumekuwa kuna changamoto kwa wakulima hasa wa zao la mahindi msimu huu, mahindi yamevamiwa na wadudu lakini mkulima anatumia dawa nne, sita mpaka nane, anazichanganya lakini bado hazi-*react* kwa wadudu hao na elimu kwa wananchi wetu bado ni ndogo: Nini mkakakti wa Serikali kuhakikisha kwamba dawa sahihi kulingana na wadudu husika ambao wamevamia mazao inapata tiba kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na viuatilifu (*TPHPA)* Serikali imekuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba viuatilifu vyote vinavyoingizwa nchini ni vile ambavyo vinakidhi mahitaji na matakwa ya changamoto ambazo zinawakabili wakulima wetu. Hivyo ambacho tutakifanya zaidi, ni kuendelea pia kutoa elimu kwa wakulima wetu juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu hivi ili viweze kuleta matokeo chanya na viweze kumsaidia mkulima katika kupambana na uhalibifu wa mazao.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali inatambua changamoto zilizojitokeza na kuendelea na ukaguzi ili tukibaini kwamba kuna changamoto kama hiyo katika baadhi ya maeneo, tutaweza kuchukua hatua stahiki na tuweze kufuta mpaka usajili katika wale ambao wanahusika. Sambamba na hili, uhakika tu ni kwamba tutahakikisha kwamba mkulima wetu anapata viuatilifu ambavyo ni sahihi kwa wadudu sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa namwita Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, aulize swali lake.

Na. 106

**Viwango vya ufaulu kwa mitihani ya kidato cha nne na sita kati ya Bara na Zanzibar**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA K.n.y. MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuondoa tofauti ya Viwango vya Ufaulu kwa Mitihani ya Kidato cha Nne na Sita Kati ya Bara na Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA,** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa jumla wa matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne na Sita uliofanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2022 ulibainisha kuwa Zanzibar ilikuwa na ufaulu wa juu zaidi kwa kidato cha nne na sita kuliko Tanzania Bara katika mwaka 2013, 2015 na 2016. Aidha, Tanzania Bara ilikuwa na ufaulu wa juu zaidi ya Zanzibar kwa mwaka 2014 na mwaka 2017 hadi 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na uendeshaji wa elimu ya msingi (awali, msingi na sekondari) siyo suala la Muungano, ingawa kwa Kidato cha Nne na cha Sita wote wanafanya mtihani mmoja wa Baraza la Mitihani la Tanzania. Kwa msingi huo, kila upande wa Muungano una mikakati yake ya namna ya kuongeza kiwango cha ufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mitaala ya Elimu. Zoezi hili linafanyika kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha kuwa tunakuwa na Sera na Mitaala inayolenga kutoa ujuzi zaidi kwa wahitimu na pia tunaoanisha kwa kiwango kikubwa elimu inayotolewa Tanzania Bara na ile inakayotolewa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na mikakati ya Serikali ambayo imeianisha lakini bado kuna changamoto ya ufaulu hasa katika masomo ya sayansi na hisabati. Ni nini mkakati wa Serikali kupandisha ufaulu huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, najua kuna mchakato unaendelea wa kuiangalia mitaala. Je, ni lini hiyo mitaala mipya itatumika katika sehemu zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, anataka kufahamu juu ya mkakati wa Serikali hasa hasa katika masomo ya hisabati na sayansi. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali tumejipanga vizuri kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuweka kipaumbele hasa hasa kwenye ajira za walimu wa masomo haya ya sayansi pamoja na hisabati;
(ii) Kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga maabara katika shule zetu ambazo zinazotoa masomo haya ya sayansi;
(iii) Kuhakikisha kwamba tunapeleka vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa ajili ya ufundishaji wa masomo haya; na
(iv) Kuendelea kuhakikisha walimu wale wa masomo ya sayansi basi tunawapeleka kwenye mafunzo ili

kuhakikisha kuwajengea uwezo wa kuweza kufundisha masomo haya kwa umahiri, kwa umahiri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anataka kufahamu utaratibu wa mitaala. Ni kweli tumezungumza hapa kwamba tunaendelea na uratibu pamoja na maboresho ya mtaala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu, mitaala yetu pamoja na sera tayari tuna rasimu ya nyaraka hizo na hivi sasa taratibu zinazoendelea ni kuendelea kupata maoni ya wadau ikiwemo na ninyi Waheshimiwa Wabunge. Tutaleta rasimu hiyo katika Bunge lako Tukufu ili kuweza kupata ridhaa na baadaye kwenda kwenda kwenye mamlaka zinazohusika na ithibati au kupitisha mitaala hii pamoja na sera ili iweze kuanza kutumika. Kwa hiyo, mara baada ya mchakato huu kukamilika, mitaala hii itaanza kutumika rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa, Wizara hii hii Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, Mbunge wa Kwimba, aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Nyamoga karibu.

Na. 107

### Ukamilishaji ujenzi Chuo cha VETA Ngudu

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y MHE. SHANIF J. MANSOOR** aliuliza:-

Je, ni lini Chuo cha VETA Ngudu Kwimba kitakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shanif Jamal Mansoor, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kukamilisha ujenzi wa vyuo vya VETA Nchini. Kwa sasa inakamilisha hatua ya uwekaji wa samani pamoja na kuandaa rasilimaliwatu kwa lengo la kuviwezesha vyuo vya VETA ikiwemo Chuo cha Ngudu kuanza kutoa mafunzo kwa mwaka wa masomo 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Chuo cha VETA Ngudu upo katika hatua ya ukamilishaji na umefikia asilimia 97. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imeshapeleka kiasi cha shilingi 189,607,486.00 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa chuo hicho, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justine, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTINE L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Ujenzi wa chuo hiki pamoja na kwamba umefikia hatua hizo lakini kuna shida ya huduma ya maji na gharama yake ni shilingi milioni 90. Je, ni lini Wizara itapeleka fedha milioni 90 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa chuo hicho na ili huduma ziweze kutolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tunaishukuru Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga chuo katika Wilaya ya Kilolo. Je, ni lini ujenzi huo utaanza katika Wilaya ya Kilolo ili wananchi waweze kunufaika na huduma za chuo cha VETA.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Justin Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anataka kufahamu swala la maji katika Chuo cha Ngudu. Ni kweli tumepeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji kwa maana ya majengo lakini kwa maana ya uunganishwaji wa maji bajeti ile iliyokuja baada ya kuifanyia tathmini tuliona kwamba iko kubwa sana, ilikuwa *inflated* kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, tumeifanyia maboresho na sasa fedha zimekuja kama milioni 57 hivi kipindi kifupi kijacho tutapeleka fedha hiyo kwa ajili ya ukatishaji wa maji katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali lake la pili anataka kufahamu ujenzi wa chuo cha VETA Kilolo. Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge tayari timu ya wataalam imeshafika Kilolo na tumeshafanya *topographical survey, geotechnical survey* pamoja na *environmental and social impact assessment* na baada sasa ya matokeo haya ya vipimo hivi tutakwenda kuanza ujenzi mara moja, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Busekelo tunaomba sana Serikali itujengee chuo cha VETA na Mheshimiwa Mbunge

yuko tayari kusaidia kupata eneo kwa ajili ya kujenga chuo hiko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vyuo vya *VETA* unajengwa katika kila wilaya na wilaya zote zilizobaki ambazo hazina vyuo vya VETA katika kipindi hiki cha 2023/2024, tunakwenda kujenga katika wilaya zote zilizobaki. Kwa hiyo, kama Busekelo ni wilaya ambayo haikuwa na chuo cha VETA nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge tunakwenda kufanya kazi hiyo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, ni lini Chuo cha VETA kilichojengwa Wilayani Lushoto Eneo la Mlola kitaanza udahili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha *VETA* Lushoto ni miongoni mwa vile vyuo 25 vya awamu ya kwanza, ambapo ujenzi wake umeshakamilika kwa asilimia 100. Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kama nilivyokwishajibu kwenye majibu ya swali la msingi vyuo hivi

vyote 25 vya awamu ya kwanza, tunapeleka samani, vifaa vya kufundishia pamoja na kuandaa rasilimali watu. Ni matumaini yetu katika mwaka wa fedha 2023/2024 vyuo hivi vyote 25 vya wilaya na vile vinne vya mikoa vinaenda kuanza kutoa mafunzo rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Kigamboni katika Hotuba ya Bajeti ya Mwaka jana ilitajwa kwamba ni moja ya wilaya ambayo mtakwenda kujenga chuo cha *VETA* na imebakia miwezi miwili. Ni lini sasa ujenzi ule utaanza ili wananchi wa kigamboni waweze kunufaika na chuo hiko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kigamboni ni miongoni mwa wilaya 64 zilizobaki katika ujenzi wa vyuo 64 zilizobaki. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *geotechnical survey, topographical survey, environmental impact assessment* tayari tumeshafanya. Tunasubiri majibu kwa maana ya *results* ya tafiti hizo na baada tu ya majibu hayo, tunaenda kuanza ujenzi katika mwaka huu wa fedha, nimuondoe wasiwasi kazi hiyo inakwenda kufanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naipongeza Serikali kwa kujenga vyuo vya *VETA*

lakini kwenye vyuo hivi vingi vya VETA vilivyopita, masomo yanayotolewa mengi hayana soko kubwa kwenye ajira ya sasa lakini kuna masoma kama ufundi bomba, ufundi umeme wa magari, umeme wa majumbani unakuta kozi nyingi hazipo kwenye vyuo vya VETA mathalani Makete. Ni lini Serikali itaanza kuongeza masomo hayo ambayo yanaajira nyingi kwa vijana wetu ili waweze kupata kusoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejibu katika swali nadhani namba 96 la kuhusiana na suala la upitiaji wa mitaala. Tumeanza upitiaji wa mitaala katika elimu yetu ya msingi lakini tunafanya mapitio ya mitaala katika elimu ya sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vikuu pamoja na vyuo vya VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio hayo ya mitaala vile vile katika maeneo haya ya vyuo vya VETA tunakwenda kuongeza idadi ya masomo lakini vile vile kufanya *review* ya hata hayo masomo yote tunayoyatoa kuhakikisha kwamba tunakwenda kweli kujibu changamoto za wananchi zile ambazo katika maeneo yao ambao wanahitaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Yapo matangazo machache hapa.

Tunaanza na wageni; wapo wageni waliopo jukwaa la Spika; ambao ni wageni saba ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Usafirishaji kutoka Bunge la Sudan Kusini wakiambatana na Maafisa kutoka Bunge hilo. Naomba niwataje kama ifutavyo; Mheshimiwa Gloria Philemoni ambaye ni kiongozi wa msafara; Mheshimiwa Juma Amiro ambaye ni Mbunge; Mheshimiwa Felix Edward Bali, Mbunge; Mheshimiwa Agnes Ikaya, Mbunge; Mheshimiwa Emanuel Tito, Afisa wa Bunge; Ndugu Nunu Chantal Doris, Afisa wa Bunge; na Ndugu John Sumaki, Afisa wa Bunge. Wageni wetu hawa wako na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa wanne wa Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge, ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Iringa, wageni hawa wa Mheshimiwa Ritta wameambatana na mwanafunzi wa kidato cha kwanza anaitwa Fedrick ambaye ametunga kitabu chenye maudhui ya ulinzi na usalama kwa mtoto na mtoto huyu ana miaka 13, ahsante sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Martha Gwau, Mbunge, ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Singida, Ndugu Munira Nkango. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mbunge ambaye ni Katibu Msaidizi wake, Ndugu Kija Masunga. *(Makofi)*

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Shamsia Mtamba, Mbunge ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Ujasiriamali na Kilimo cha Jijini Dodoma wanaotokea Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wageni watano kutoka Kampuni ya Bima Mtawanyo *(Grand Reinsurance Tanzania)* wakiongozwa na

Ndugu Micheck Sithole, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala anayemwakilisha Mtendaji Mkuu, ameambatana na Ndugu Charlesh Chanya, Meneja Biashara; Ndugu Kwandu Kipilyango, Meneja Madai; Ndugu Augustino Ndabaha, Afisa Biashara, Ndugu Prisla Soka, Afisa Mwandikishaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)* imeandaa Iftari maalam kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. *Iftar* hii itafanyika katika Viwanja wa Bunge, leo siku ya Jumatatu tarehe 17 Aprili, 2023 kuanzia saa 12:30 jioni. Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote wanaalikwa futari hii bila kukosa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 hapa nimeletewa orodha wachangiaji ni wengi kweli kweli. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tutapeana dakika 8.

Tutaanza na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuanza kuchangia TAMISEMI. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa afya njema aliyotujalia na nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa miradi mingi sana ambayo kwa kweli ameipeleka kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo la Kiteto pekee yake, miradi ya miaka miwili hii ni karibu bilioni 18. Kwa kweli amegusa karibu kila mahali, *VETA* sasa tunazungumza inajengwa Kiteto. Tumepata vituo vya afya viwili bilioni 1, Daraja la Sunya karibu milioni 800, shule shikizi madarasa karibu 57, shule za sekondari madarasa 44, mradi wa maji pale Kaloleni, *digital x-ray* milioni 900 kwa ajili ya kukarabati hospitali ya wilaya. Ambaye sasa sisi tuliomba na hii ni *renovation* ya Mkurugenzi aliomba kwamba tunajenga jengo la mama na mtoto, jengo la upasuaji na maabara. Sisi tulikataa kukarabati majengo yale na nashukuru TAMISEMI kwa sababu tumeomba na wametuambia, wametupa *go ahead*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iniseme TAMISEMI walituambia ili kuweza kujenga majengo hayo sisi tunahitaji karibu bilioni moja na milioni 300 na wao wametupata mia 900 lakini sisi tukasema tutajenga kwa hiyo mia 900. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mkurugenzi kwa *renovation* hiyo nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah, Naibu Waziri Dugange na Ndejembi, Katibu Mkuu, wote na timu nzima hii kwa kazi nzuri ambayo wanajaribu kufanya. Mheshimiwa Waziri kila wakati tukikuandikia, umekua mwepesi sana na timu yako nzuri sana. Nashukuru pia kwa ziara aliyoifanya Naibu Waziri Kiteto kwa kweli timu ya TAMISEMI mmejipanga vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru vile vile kwa pesa tuliozipata kwa ajili ya shule kongwe zile. Shule za Kijungu, Sunya, Ndosidosi, Kibaya na nashukuru kwa sababu tumeona mmetuongezea pesa tena kwa ajili ya shule hizi kongwe. Mheshimiwa Waziri tulikutana, ile *idea* yako ya kukutana na Wabunge wa Mikoa ilikuwa ni *renovation* nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wewe unafahamu tarehe 12 Februari, tulikutana na timu ya Manyara na tukaleta maandishi yetu ya kujaribu kuonyesha miradi. Eneo kubwa ni *TARURA*, *TARURA* tulishakubaliana hapa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi iko bayana sana, tulisema ni lazima sasa TARURA iongezewe pesa kwa sababu ya mtandao wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilisema hivi na tuliahidi kwamba ni vyema sasa tuanze kuangalia ile *formula* ile kati ya TARURA na *TANROADS* kwa nia ya kuongezea *TARURA* pesa. Kwa mfano, kwa Kiteto pekee yake, mtandao wa barabara ni kilometa 1,291. Bajeti tunayoihitaji ni bilioni 11, lakini uhalisia tunapata bilioni mbili na milioni 800 haitoshi na siku ile Mheshimiwa Waziri unafahamu tulisema kama mtatuongezea sisi bilioni tatu walau tuwe tunapata bilioni 5.8 ama sita itatusaidia kuendelea kujenga mtandao huu wa barabara, ili wananchi waliopo vijijini wakapate kusafiri bila shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ombi langu lipo pale pale, tunategemea kwa kweli hizi pesa ziongezeke. Na kwa kweli nimpongeze Mkurugenzi wa *TARURA* hata kwa sura simfahamu lakini nimemsumbua kwenye simu, Kiteto ilikua haina gari na sasa tumepata gari. Kwa kweli nampongeza sana. kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mtuongeze pesa kwa ajili ya *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri, alikuja Katibu Mkuu wa CCM Jimbo la Kiteto,

ametuahidi kilometa 1 ya lami na taa za barabarani na maombi tumeshaleta. Taa za barabarani pale mjini ni karibu milioni 250 tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaendelea kumbushia, *ambulance* kwa ajili ya Engusero aliahidi Mheshimiwa Rais, Sunya gari lao lilipata ajali na hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, kwenye zile *ambulance* mnazogawa Kiteto utupendelee. Kiteto ni kubwa kila siku nasema hapa, *square* kilometa 1,700. Mheshimiwa Waziri ukituongezea itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la walimu wanaojitolea; Mheshimiwa Waziri tunashukuru mmetangaza ajira, fuatilia tunataka walimu hawa wanaojitolea wapewe kipaumbele kwenye ajira. Kila mtu anapojitolea nia yake, kwanza ni suala kizalendo, kujitolea. Kwa hiyo, kwenye nafasi hizo kwa kweli uwachukue na inasadikika nchi hii sasa wapo walimu wanaojitolea karibu 70,000/80,000 hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakianzisha mjadala wa kuwachukua hata kama ni kubadilisha sheria, kwamba vigezo ni *merit, yes* lakini mtu anayejitolea na yeye hicho ni kigezo ambacho ni muhimu sana, hawa watu wanafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo tunategemea kwamba tutaona vijana wengi wa Kiteto wanaojitolea wakipata ajira kwenye nafasi ambazo wametangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Madiwani. Madiwani wetu wanafanya kazi kubwa sana. Wanasimamia miradi na nataka niseme kuna *link* kati ya fedha hizi zinazopotea labda na kwa sababu Madiwani hawako *full time*. Labda tuangalie huko mbele baadaye maslahi ikiongezeka na posho na stahiki kwa ajili ya Madiwani labda usimamizi utakuwa wa bora sana na pengine hizi fedha zinazopotea potea, haitatokea. Hebu waangaliwe sana Madiwani wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la maboma ama miradi ile ambayo inafanywa na wananchi. Kiteto, wananchi wa Kiteto ni wachapa kazi sana. Kuna miradi mingi sana, kwa mfano zahanati tu peke yake karibu miradi 14 ipo kwenye lenta, wananchi wale wamefanya kazi kubwa sana. Kwa mfano, Zambia, Mbigiri, Mbeli, Taigo, Chapakazi, Engusero, Sidan, Logoet, Chekanao, Olduvai na mengine mengi. Zahanati zao ziko kwenye lenta. Tulikaa hapa mwaka jana, tukasema tujenge vituo vya tarafa, Kiteto bado nadai vituo vitatu vya tarafa. Tarafa ya Makame, Dosidosi na Kibaya. Tulisema tukipeleka huduma hizi kwenye tarafa itasaidia sasa zahanati tunazozijenga walau tutakuwa tumepeleka huduma karibu na wananchi. Kwa hiyo, kwa kweli tusikubali hili Bunge liishe hatajamalizana na habari ya vituo vya tarafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Waziri akatafute fedha. Hili halina mjadala hata kidogo, nataka vituo vitatu vya tarafa na tulishapitisha hapa. Haiwezekani watu wengine wanaendelea kujenga za kata wakati sisi wengine tunazungumza habari ya tarafa hapa *and I am serious, very serious about this,* kwa kweli. *This is not negotiable,* tumeshakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majengo haya, Kiteto hospitali yetu ikipata tena majengo ya *maternity,* dharura *(emergency), RCH* na jengo la *X-Ray* ile mpya ambayo tunaitumia sasa, itasaidia kuweka Wilaya ya Kiteto kwenye hadhi ya Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la watumishi. Kuna Mkurugenzi yuko pale Same. Unajua siyo kila wakati lazima tukutane hapa tuna-*complain* kuhusu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Olelekaita, muda wako umekwisha.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wangu anachapa kazi sana abaki na aendelee kumaliza majengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsanteni sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Olelekaita. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mheshimiwa Bonivetura Kiswaga ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazofanya hasa katika utoaji wa fedha kwenye majimbo yetu. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana Waziri wa TAMISEMI pamoja na wasaidizi wake na watumishi kwa ujumla katika Wizara ya TAMISEMI kwa kazi kubwa wanazofanya. Sisi tunapata faraja sana kwa kazi wanazofanya. Pia kipekee niipongeze na kuishukuru sana Timu ya Simba kwa kazi kubwa iliyofanya jana. Kwa kweli ilifanya kazi kubwa kwa ajili ya nchi na nchi imetulia kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana gani? Labda Mheshimiwa Waziri Jenista aiandike hii. Tuliwafunga Horoya goli saba na jana wamefungwa Yanga goli mbili jumla tisa. Maana yake nini? Magoli manne ni ya uongozi wa Mama kuelekea 2025, zawadi na magoli mengine matano ni zawadi ya Mama 2025 – 2030, ndiyo maana ya yale magoli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Rashid Abdallah Rashid.

**T A A R I F A**

**MHE. RASHID ABDALLAH RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe mchangiaji taarifa kwamba asije kulalamika na muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu ya Yanga ndiyo maana kasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye kuchangia. Pamoja na mambo mazuri ambayo yamefanywa na Serikali, pamoja na fedha ambayo tumepokea kwenye majimbo yetu sasa kuna mambo ambayo pia tunaomba kuiomba Serikali iweze kuyafaya ili tuweze kuwa na tija zaidi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie eneo la afya. Katika Jimbo la Busega tuna vituo vya afya ambavyo vilipandishwa hadhi kutoka kwenye zahanati; Kituo cha Afya Kiloleli na Kituo cha Afya Lukungu kwa maana ya Lamadi. Vituo vya afya hivi bahati nzuri sana vilipandishwa na Dkt. Dugange akiwa *RMO* wa Mkoa wa Simiyu, anavijua vizuri, lakini mpaka sasa hivi havina wodi yoyote. Kwa mfano Lukungu tuna *theatre* pale, haifanyi kazi kwa sababu hamna wodi. Ukimfanyia mtu *operation* hamna pa kumpeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Wizara ilione hili, vituo vya afya hivi viwili kwa maana ya Kiloleli pamoja na Lukungu kule Lamadi, viwekewe miundombinu ya majengo ili vianze sasa kufanya kazi kama vituo vya afya na kama vilivyopandishwa hadhi na Dkt. Dugange akiwa *RMO* kule Simiyu. Kwa hiyo anavifahamu vizuri kwa sababu yeye ndiye

alivipandisha hadhi kutoka kwenye zahanati kwenda kwenye vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuyachukue haya kuwasaidia wananchi wa Kiloleli ili wapate majengo ya wodi kwa maana ya wodi ya wanaume, wodi ya watoto na wodi zingine pamoja na kule Lukungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba nichangie eneo la *TARURA*. Najua kazi kubwa imefanywa na *TARURA*. Kazi kubwa tumefanya kwenye miundombinu ya barabara. Naomba nami nipige kura ya ndiyo kama Mheshimiwa Waziri atakubali, *Engineer* Seif awe mfanyakazi bora *TARURA* mwaka huu Mei, kwa sababu kwa kweli anatutia moyo sana kwenye majimbo yetu. Anafanya kazi kubwa, ukimpigia simu anapokea, ana-*respond* na fedha zinakuja kwa wakati na wakandarasi wanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe Mheshimiwa Waziri na ndugu yangu Seif, pale Busega tuna Daraja la Lutubiga kwenda Mwasamba, daraja ambalo linahitaji shilingi milioni 900. Tunaomba sana huruma ya Mheshimiwa Waziri tupate shilingi milioni 900 kwenye bajeti ya maendeleo ili tuweze kuwatengenezea daraja wananchi wanaotoka Lutubiga kwenda Mwasamba, kwa sababu imefikia sehemu sasa wanafunzi hawawezi kuvuka pale, imebidi tuwaombee kwenda kusoma kwenye kata nyingine ya jirani kwa sababu kile kijiji hakina mawasiliano na kijiji kingine cha Mwasamba. Kwa hiyo, tunaomba sana tupate shilingi milioni 900 za dharura ili tuweze kuwasaidia watoto wanapotoka Lutubiga kuelekea kule Mwasamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nataka nichangie, ni habari ya 20% za maendeleo kwenye mapato ya ndani kwenye halmashauri 56. Fedha hizi ambazo ni 20% katika mwaka wa fedha unaokuja ambao leo tunauzungumza hapa. Wamepanga 20% kwa baadhi ya

halmashauri ambazo ziko 56 ikiwemo Busega, Bariadi *DC,* Bahi, Siha pamoja na zingine lakini jumla ziko 56. 10% ndiyo tunazopeleka kwenye maendeleo na 10% nyingine ni kwa ajili ya makundi maalum kwa maana vijana, wanawake pamoja na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, hii 40% ilikuwa ni msaada sana kwenye halmashauri zetu kwa ajili ya mikakati na maendeleo ambayo tulikuwa tunafanya kupitia mapato ya ndani. Tunaomba waturudishie hizi fedha ili tuweze kufanya miradi ya kimkakati kwenye halmashauri zetu. Hii 10% haitatosha kufanya kazi za kimkakati kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Busega ni zaidi ya shilingi milioni 300 ambazo zimetolewa kwa ajili kupelekwa kwenye matumizi ya kawaida. Nimshawishi sana Mheshimiwa Waziri, hizi halmashauri tuzirudishie hizi fedha ili ziweze kufanya maendeleo. Kwa mfano, una shilingi milioni moja, sasa kwenye maendeleo tunaenda kupeleka shilingi laki moja. Kwa kweli kwa halmashauri zetu hizi haiwezekani na hizi ndiyo siasa zetu na hizi ndiyo zinazosaidia kazi za dharura kwenye majimbo yetu. Ikitokea kazi ya dharura fedha hizi ndiyo tunatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sisi kuna maboma mengi ambayo wananchi wamejenga, tukiwa na fedha hizi itatusaidia kupeleka kwenye miradi ya wananchi ambayo wananchi wetu wameanzisha. Kuna sehemu nyingine pia tunafikiria hata kuanzisha masoko ya kimkakati kutoka kwenye halmashauri. Fedha hizi wakitusaidia zitatusaidia kuweza kufanya kazi za kimkakati kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeona halmashauri hizi hazina fedha tuwaongezee *OC* ili waweze kupata fedha za kufanyia kazi za matumizi ya kawaida, lakini hizi fedha za maendeleo tunaomba zirudi 40%, 10% iende kwenye

makundi maalum na 30% ibaki kwenye miradi ya kimkakati ili tuweze kufanya kazi kupitia majimbo yetu na kupitia fedha hizi. Tumwombe sana Mheshimiwa Waziri, atafakari tena pamoja na wasaidizi wake. Ikibidi kama inafaa waweze kuturudishia hizi fedha na kama wakiona haifai basi waturudishie za Busega ili tuweze kufanya kazi za kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo pia limekuwa likizungumzwa hapa. Maboma ya wananchi na miradi ya kimkakati ambayo imeanzwa na wananchi. Wananchi wetu wana maboma mengi ambayo wameyaanzisha. Kwa mfano Busega tuna maboma 69 ya madarasa, tuna maboma 10 ya nyumba za Walimu. Wananchi wametoa fedha, wananchi wamejibana wameanzisha miradi hii, lakini bado iko kwenye maboma. Tumekuwa tukipata fedha tunapeleka kuanza miradi mipya. Tunaomba sasa TAMISEMI iangalie ifanye sensa nchi nzima ili kusudi tupate tupewe zaidi kwa ajili ya fedha za mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kukushukuru kunipa nafasi nami niweze kuchangia na nichukue fursa hii. Pia nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niwapongeze sana watumishi wa Wizara ya TAMISEMI kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya kuhakikisha mnatimiza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashauri sehemu ya miradi inayoendelea. Sisi Wabunge tunapokuja kwenye Bunge lako

Tukufu tunakuwa na mipango ambayo tumeiandaa kwenye halmashauri zetu. Tumehamasisha wananchi kuhakikisha kwamba tunajenga madarasa, tunajenga zahanati, tunajenga vituo vya afya na tunaambiwa tutakapokamilisha miradi hiyo Serikali kuu itakuja kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo sasa linatupa changamoto, fedha za Serikali kuu zinapokuja badala ya kumalizia zinakuja na maelekezo ya kuja kuanza miradi mipya. Tayari majukumu yetu kama Wabunge yanakuwa yamepotea kwa sababu ile miradi inakuwa ni chakavu, haitekelezeki, lakini vile vile na miradi mipya tunayoianza ndiyo sasa inayokuja na hoja za *CAG* hapa inakuwa na gharama kubwa badala ya kwamba yale majengo tuliyoyaanzisha na yale majengo yamesimamiwa na halmashauri. Viongozi watendaji wako pale, ma-*engineer* wako pale, hatua zote za kitaalam zimefanyika, lakini inapokuja fedha kutoka Serikali Kuu inasema tunaanzisha majengo mapya, tunaanzisha zahanati mpya, hii tunaiacha na hizo ramani zinabadilika tena zinakuja ramani zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe TAMISEMI iangalie tathmini ya nchi nzima kwenye maboma yote. Zile fedha zinapokuja ziende zikamalizie maendeleo ya wananchi waliyoyaanzisha. Lazima hatutakaa tufike malengo tunayoyatarajia kwa sababu miradi mingi inatakiwa isimamiwe na wananchi, miradi mingi inaenda kuwahudumia wananchi wanaotoka kwenye maeneo husika. Ni vyema tunapofika mahali miradi tukaona inafaa tukaongeza miradi hiyo ili maendeleo yaende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano na niombe sana Wizara ya TAMISEMI, kwenye wilaya yangu nimejenga zahanati zaidi ya 32. Zahanati 10 zimeshakamilika, lakini bado mipango midogo midogo ya kumalizia, tumewachangisha wananchi mpaka kuchoka. Sasa niiombe TAMISEMI hizi Zahanati za Dasini, Gambasingu, Nkololo, Mwagimwagi,

Nhobola, Kidula, Muhalale, Golambeshi, Laini na Inalo, zina changamoto chache na hizo changamoto sisi kwenye halmashauri tumejibana tumebakiza fedha kwenye jengo la utawala. Waturuhusu zile fedha ziende zikamalizie ili kusudi wananchi waweze kupata huduma ya afya kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyotuelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwenye hizi fedha za *BOOST*. Niombe, wamefanya kazi nzuri kubwa sana Wizara ya TAMISEMI na wanafanya kazi kubwa kuhakikisha tunapeleka elimu kule vijijini, ni jambo jema. Niombe kwenye yale maboma ambayo yako kwenye mipango mizuri, basi zile fedha waangalie utaratibu wa uwezekano wa kuhakikisha kwamba tunaenda kumalizia miradi mikubwa ambayo italeta *impact* kubwa kuliko kupeleka shilingi milioni 540, unaenda kujenga shule mpya na kuna shule zingine shikizi zaidi ya shule 30 au 40 kwenye eneo hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe tu Wizara wakae kuhakikisha kwamba tunatatua hii changamoto ili wananchi kwenye maeneo yale tuwape morali ya kufanya kazi zile. Vinginevyo tutakuwa tunaelekeza michango yetu, lakini mawazo yetu hayatatekelezeka kwa sababu wanajua hata tukianzisha mradi huu hakuna kitakachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze *TARURA*. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa na nzuri sana na ndiyo watakaotubeba kwa sababu barabara kila mtu anapita hata kama ni mgeni kutoka nchi ya wapi. Atapita kwenye barabara atasema Tanzania iko safi kwenye barabara. Niwaombe waendelee tu kuongeza nguvu ili kusudi tuendelee kuboresha barabara zetu, madaraja yetu na wilaya zetu zikutane wilaya kwa wilaya. Niombe kwa Mkurugenzi wa *TARURA* atusaidie sana, kuna maombi ambayo tumepeleka lakini ni ahadi za Mheshimiwa, Viongozi Wakuu waliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mto Gamaloha ambao unaunganisha Kata ya Nkuyu, Mwaswale na Laini. Niombe sana kwenye mpango wa maendeleo na yenyewe iwepo. Vile vile kuna Mto Sanjo tunakutana na Wilaya ya Meatu, nako niombe sana Wizara ichukue hili jambo iweze kutusaidia wananchi wa kutoka Meatu na kutoka Itilima waweze kuunganika kufanya kazi za maendeleo katika maeneo hayo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mto unaitwa Ntagosa unaungana na Ipililo, wilaya mama katika Mkoa wetu wa Simiyu. Niombe sana Wizara ichukue nafasi hiyo kuhakikisha kwamba inatusaidia kwenye maeneo hayo. Jambo hili likifanikiwa tutakuwa tunafanya kazi kubwa na nzuri zaidi kuhakikisha kwamba tunapeleka maendeleo kwa wananchi wetu. Vile vile tutaendelea kutoa hamasa kwenye maeneo haya kwamba Serikali sasa inafanya kazi yake kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, niombe, tuna miradi mikubwa ya maendeleo yetu ambayo tunaifanya, lakini kubwa zaidi tunaomba kupata watumishi. Serikali watuambie na tulishawahi kusema humu ndani kwamba kama tunajenga hizi zahanati tunajenga shule na yote inalenga maendeleo ya wananchi, kwa nini hatupati watumishi wa kwenda kuhudumia zile kada? Tunaamini sasa hivi wameshatoa nafasi hizi, tuombe, kuna vijana wengi wamemaliza vyuo muda mrefu tangu 2018, 2019, 2020, lakini cha ajabu tunasubiria sasa hivi kitakachokuja kutokea unaweza ukakuta wa 2022 ndiyo anachukuliwa, wa 2016, 2017, 2018 anakuwa hayupo. Wanatupa wakati mgumu kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe Wizara inayohusika ihakikishe kwamba sasa jambo hili la utumishi linatatuliwa la sivyo watueleze Serikali, kwa sababu tunajenga miradi inasimama kwa kukosa wale wahudumu wanaohusika. Watuambie kama uwezekano haupo tujipange sisi kwenye

halmashauri zetu tujue jinsi gani ya kutoa huduma kwenye maeneo haya na wakifanya hivyo Mheshimiwa Waziri atakuwa anafanya kazi kubwa na nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kazi ya Wizara ni nzuri wanayoifanya na kule na sisi tunawaunga mkono kwa 100%, kwa sababu tunaamini yale ambayo tumeyaahidi na wao wanatusaidia hawalali usiku na mchana kuhakikisha wanachapa kazi ya kuhakikisha wanawahudumia Watanzania. Sasa tuwaombe wachukue mawazo yetu waende wakayafanyie kazi ili tufike hatma ambayo tunaitarajia na kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyotuelekeza kwamba tutakamalisha yale yote ambayo sisi tumekuwa tukiyafanya ndani ya muda wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho niombe nina miji yangu michache ambayo inakuwa kwa kasi sana. Mji wa Lugulu naomba nitengenezewe barabara za mitaa kwenye maeneo hayo, Mji wa Migato barabara kwenye maeneo ya mitaa, Mji wa Laini na Mji wa Mwamapaa na Suzula yote maeneo haya ni ya kiuchumi. Niombe sana Serikali iyachukue na kuyafanyia kazi na kuendelea kuboresha barabara zilizoko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii miradi inayofanyika halmashauri za miji na manispaa, lakini miradi hii haiji kwenye halmashauri zilizoko vijijini. Sasa Serikali ichukue wanapokutana kwenye mipango ya kuratibu wajue wanaporatibu mipango maendeleo yale makubwa watu wanaotoka vijijini ndiyo wanaokwenda mjini kukaa pale kwenye halmashauri na kwenye manispaa. Sasa na kule kijijini ili mazao yatoke vijijini kwenda mjini ni vizuri barabara ziboreshwe. Kwa hiyo kwenye miradi inayokuja ni muhimu sana wakahakikisha wanaangalia mazingira yale ili kusudi jamii inayoishi kwenye halmashauri za vijijini na yenyewe ijitambue kwamba kuna umuhimu wa kukaa kule.

Tunapoirundika kwenye manispaa na kwenye halmashauri za miji, tayari tunanyima haki kwenye halmashauri zilizoko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniventura Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere wajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara muhimu sana ya TAMISEMI ambayo inawagusa wananchi. Niipongeze Serikali kwa namna ya pekee Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ya pekee inavyoleta fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kihuduma kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja kwa *TARURA*. *TARURA* kila mmoja hapa anahitaji iongezwe fedha, ni kwa sababu kwamba ili maendeleo ya kiuchumi yaweze kuwepo barabara zinahitajika. Mtu ambaye alikuwa anasafiri masaa manane aweze kusafiri masaa mawili. Mtu ambaye alikuwa anakwenda kupata huduma ya kiafya asafiri kwa haraka ili aweze kufika kwenye huduma za kiafya. Kwa hiyo *TARURA* ni muhimu sana kwa kweli tukaona namna ambavyo tunaweza kuiongeza fedha ili iweze kuhudumia barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara ambazo kwa kweli zinahitaji madaraja tu kuunganishika, hakuna mawasiliano ambayo yanapatikana bila kuwepo na daraja. Nyuma kule tulikuwa na Mradi wa *Bottleneck* ambao ulisaidia sana barabara ambazo zilikuwa haziunganiki, kata kwa kata, kijiji kwa kijiji, wilaya kwa wilaya. Kwa hiyo niombe tena, kwa mfano kule kwangu Barabara ya Kahangala, Mwamanga

kwenda Kisesa B pale huwezi kwenda mahala popote kama mvua imenyesha; na kuna vijiji vitatu ni kama viko visiwani. Kwa hiyo niombe sana, kwa mfano Inolelo, juzi nilikuwa na mikutano ya hadhara kule, nimemaliza Kijiji cha Kisesa B ikabidi nizunguke Kata ya Nyanguge, Kata ya Kitongo Sima, Kata ya Kahangala ndipo nifike tena kwenye Kijiji cha Inolelo. Kwa kweli ni mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tumekwishaiomba siku nyingi TAMISEMI, na tulikaa na Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki nikaiomba hiii Barabara ya Kahangala, Mwamanga, Kisesa B; mwaka huu nipeni fedha ili iweze kutengenezwa na wananchi tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siishii hapo, kuna Barabara ya Kisamba Sayata Mkurugenzi wa *TARURA*, Ndugu Seth, nimeshakuomba mara nyingi kwamba huwezi kufika salama kuelekea Bariadi bila kuwa na daraja pale Kinsalama kuja Sayaka; ninaomba sana mwaka huu. Mheshimiwa Waziri umeanza utaratibu mzuri wa kukaa na Wabunge. Hata tulipokaa na wewe nilikutajia hii barabara. Kwa kweli nakupongeza sana Waziri endelea kuwa na upole huo, sisi tunatoa matatizo yetu ndani tukiwa tuna uhakika kwamba haya yote yatafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Barabara ya Isolo kwenda Isawida kule Itirima. Barabara hii ni ya muhimu sana, inahitaji tu *bottleneck* kuweza kukamilika ili wananchi wa Itirima, Isolo, Kabila kuja Wilaya ya Magu waweze kusafiri kwa haraka sana. Niombe sana hili jambo liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli miji yetu inakuwa, Mji wa Magu unakuwa ni wa siku nyingi tangu mwaka 1974 ni wa umri wangu. Lakini Miji ya Kisesa na Bujora nayo unakuwa, nimekuomba Waziri wa TAMISEMI, tulipokaa pale Msekwa,

kwamba angalau nipate kilometa sita za lami zitengeneze Magu Mjini, zitengeneze Bujora na Kisesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni miji inayokua; ili miji iweze kuendelea tusaidieni. Wenzetu wanapata *TaCTIC* sisi hatupati; tusaidie Mheshimiwa Waziri hili litakuwa ni mkombozi kwa wananchi wetu. Tumetengeneza barabara za mitaro ni vizuri zikawekewa lami ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia wananchi. Niombe sana jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya, tunayo majengo maboma 20 tumeezeka kwenye Wilaya ya Magu. Kule Jijimiri ni mbali sana na huduma, kule Isolo ni mbali sana na huduma, kule Ndagalu ni mbali sana na huduma, kule Bwamanga ni mbali sana na huduma, kule Kisamba ni mbali sana na huduma, kule Lutale ni mbali sana na huduma. Ninaomba Mheshimiwa Waziri tupatieni; hizi milioni 50 mnazotupatia kwa zahanati tatu tunashukuru lakini bado hazitoshi kwa sababu mahitaji ni mengi. Ukienda pale Walina wana jengo kubwa sana lakini hatuna fedha za kuweza kulimaliza. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tukuombe basi zile zahanati tumeziezeka tupatie tu fedha ni milioni 50, ni bilioni moja kwa zahanati 20, tunakamilisha maboma haya Magu na wananchi wanaanza kutindua. Niombe sana jambo hili tuweze kupewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vituo vya afya vya kimkakati. Kule Ng’haya tumeishukuru Serikali milituletea fedha za ukarabati wa zahanati, lakini tukajiongeza Halmashauri ya Wilaya ya Magu tukaleta ombi mkatubalia kuanza kujenga kituo cha afya, tupeni fedha za kumalizia pale Ng’haya ili kituo hicho kikamilike. Sambamba na Kata ya Mwamanga ambayo imezungukwa na mito mingi tusaidie sana Mwamanga nayo tuweze kupata kituo cha afya, pamoja na Lutale tuweze kupata kituo cha afya. Tuangalie pia kukikarabati kituo cha afya cha Nyanguge ili kiweze

kukamilika. Ninaomba sana hili kwa Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iweze kutupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira hizi zilizotoka, ajira za afya na ajira za walimu. Kuna *intake* ya walimu kuanzia 2016 hawajachaguliwa. Huu mfumo unawasoma akina nani? mfumo ambao hauwasomi watu waliotangulia? wa 2016 hawajachaguliwa, wamechagua 2019, hawa watoto wa maskini ambao wamebaki wanasaidiwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe na niweze kushauri, kwa kweli kama inawezekana ajira hizi zilenge wilaya, kila wilaya ipewe watu wake ili tuangalie waliotangulia kumaliza na wanaoendelea. Kwa kweli tunawakatisha tamaa wazazi hata kusomesha. Niombe sana kwa kweli, hili linaumiza sana. Sasa hivi kwenye begi langu nimejaza *CV* za vijana, sina hata pa kuzipeleka. Kwa hiyo ushauri wangu, tutafute namna ya kuwezesha kila wilaya ni nafasi kiasi gani ipelekewe iajiri watu wake ili watoto hawa tuweze kuwasaidia. Niombe sana jambo hili Waheshimiwa Wabunge mliunge mkono, pigeni makofi ili Serikali ijue kwamba leo mmeniunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingi zinaendelea kufanyika, lakini niombe; kuna mapunjo na madai ya watumishi wetu kwenye halmashauri, wanalalamika hawajaweza kupewa mapunjo hayo. Niombe Serikali ione ili kumpa moyo mtumishi huyu anayemsaidia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipwe haki zake, alipwe madeni yake na mapunjo ambayo wanaendelea kushughulika nayo wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono hoja na nikupongeze sana pia kwa kuendesha Bunge kwa *standard* kama hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, Waheshimiwa Wabunge kuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Mary Masanja Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ni Stella Bukuru kutoka Mwanza; ahsante karibu sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafatiwa na Mheshimiwa Bonna Kamoli, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara yetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mimi mchango wangu nitauelekeza kwenye maeneo makubwa mawili. La kwanza ni kwenye mapitio ya bajeti kwa sababu ni utaratibu kabla ya kuchangia bajeti mpya kuangalia bajeti ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jiji letu la Arusha tuna changamoto kubwa sana ya ubadhirifu na usimamizi mbovu wa fedha za halmashauri. Hapa nitapenda nitoe mifano michache kabla sijaenda kwenye uhalisia. La kwanza tunajenga jengo la utawala la ghorofa zaidi ya sita, lakini bado wametafuta fundi mjenzi bila kutangaza *tender*, taratibu za manunuzi hazijafuatwa, wamemtafuta rafiki yao wamweka pale wamesaini mkataba wakampa kazi kwa kiasi cha shilingi 199,750,000. Lakini bado pia wamenunua vifaa vya shilingi 132,000,000, ambavyo havijadhibitika kufika eneo la *site*. Ukiangalia pia bado wameenda kuongeza nondo ziada ya tani 6.48 yenye thamani ya shilingi 17,000,000 ambazo ni kutokana na uzembe wa wataalamu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameweza pia kuongeza malipo ya 21,000,000 kwa fundi kutokana na uzembe pia wa watalaam wetu. Wameweza pia kuanza ujenzi huo bila kuwa na mtalaam mshauri katika ujenzi huo ambao ninaouzungumzia wa jengo la utawala. Pia bado kumekuwa na malipo *fake,* kumekuwa na risiti *fake* za *EFD* za kiasi cha shilingi 699,945,471, hela zimetoka wamefoji risiti wamepeleka

halmashauri na tumekosa kupata huduma. Bado pia wameenda kutengeneza *quotation* za kughushi za shilingi 580,545,900 kwa kutumia kampuni ya *Pedna Limited* ambayo ni shilingi 543,000,000 na kampuni ya *Arusha Hotel Ltd* kiasi cha shilingi 36,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia wamefanya malipo ya shilingi 36,580,000 kwa wazabuni ambao hawakutoa huduma yoyote katika Jiji la Arusha na Mbunge akizungumza unasema huyu Mbunge anagombana na watu. Kwenye mambo kama haya lazima tugombane mpaka mambo yaweze kueleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na manunuzi ya shilingi 12,822,400 kupitia dokezo ambalo wanasema liliandikwa na mtu anaitwa Optat Ismail; lakini baada ya kuitwa amekana dokezo hilo, kwa hiyo hilo dokezo linaonekana ni *fake* lakini mchakato uliendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia kumekuwa na matumizi ya fedha za masurufu ya kiasi cha shilingi 62,000,000 ambayo yana viashiria vya ubadhirifu na kutokana na matumizi pia mengine ya shilingi 132,000,000 ambazo gharama zake hazina *support* yoyote ya matumizi. Wanachukua hela wanatumia na wala hawajali kwa sababu wanajua ngazi ya mkoa na wilaya wala hawana cha kuwafanya na pengine inawezekana ikawa ni sehemu ya changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na matumizi ya fedha taslimu kwa manunuzi ya bidhaa mbalimbali kiasi cha shilingi 2,000,000,000 ambayo hayana udhibitisho na wala matumizi yake hayaelezeki. Sasa haya masuala ni makubwa sana nadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na timu yake wakafanya utaratibu wa kwenda kuweka jicho la ziada kwenye Jiji letu ili mwisho wa siku tuweze kuokoa hizi fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matumizi pia akaunti ya amana, yaliyokosa udhibitisho ya shilingi 92,692,714. Nimesema nianze na utangulizi huo kwa sababu Jiji letu limekuwa ni shamba la bibi, watu wameungana Serikali Kuu pamoja na Serikali ya Mtaa kuimaliza Halmashauri yetu. Mimi nimejitoa kafara kuhangaika na msuala haya ili kulinda maslahi mapana ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo suala langu la pili, nimesoma Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI yenye *page* zaidi ya 281 lakini sijaona kama wamachinga wamepewa uzito unaostahili. Ukiangalia tu kwenye *page* ya tisa amezungumzia kwenye (viii) kwamba kuratibu shughuli za wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara wadogo basi, ukitoa hapo hakuna sehemu nyingine yeyote ambayo wamachinga wamezungumziwa na wamachinga ni kundi kubwa. Ukiangalia sisi tulitenga fedha mwaka jana kiasi cha 1,000,000,000 kwa ajili ya kuboresha maeneo yao, lakini zile fedha asilimia kubwa zimeliwa, wameenda kujenga eneo moja linaitwa Ulezi, ukiwaambia kule hakuna biashara watu hawawezi kwenda wakapeleka shilingi 86,000,000 baadaye wamebomoa hasara imepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameenda kujenga jengo namba 68 baada ya kujenga bati yenye *gauge* 28 wametumia bati za *gauge* 30. Ukienda pale mvua ikinyesha tope tupu wananchi wanapata tabu, hata nia na lengo la Mheshimiwa Rais inakwenda kuwa kero kwa watu wakati dhamira ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kuwawekea watu mazingira mazuri ili waweze kufanya shughuli zao vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye upande wa machinga sisi pale tuna machinga namba 68, tuna eneo la Machame, tuna eneo la Ulezi na eneo la Mbauda. Ukienda maeneo yote changamoto ni kubwa sana; hakuna mitaro ya kupokelea maji, hakuna mataa ya uhakika. Ukiangalia

wenzetu wa Dodoma hapa wamejenga jengo zuri sana ambalo linawapa fursa wafanyabiashara na maeneo mazuri zaidi. Ukienda kule Arusha ni utani na masihara ya hali ya juu. Nikuombe tumwombe na Waziri wetu na timu yake wakaongeze jicho ili wale wamachinga wapate mahali pazuri pa kufanya shughuli zao na mwisho wa siku dhamira na nia njema ya Rais wetu iweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna changamoto pia ya wenzetu wa mgambo; mgambo wanawasumbua sana wafanyabiashara wanawanyanganya vitu vyao, mama wengine hata wakifunga ushungi wanavuliwa ushungi wao, wanafanyiwa vurugu kila mahali kiasi ambacho inaongeza kero na manung'uniko kwa watu wetu. Mimi niombe mgambo hawa, kwa sababu wao hawana hatia, wao wanatumwa na Serikali katika ngazi ya mkoa na ngazi ya wilaya na wanamshinikiza Mkurugenzi ili kupambana na hawa watu. Naishukuru Halmashauri kwa namna moja au nyingine tukizungumza nao wakati wanapowanyanyasa wale watu wamekuwa wanawarudishia baadhi ya vitu vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe hawa mgambo wawekewe utaratibu maalum, hawa machinga pia wawekewe utaratibu maalum ili pasiwe na sintofahamu na vurugu kwenye jiji letu. Ukienda soko kuu wanaonewa pale, wafanyabiashara wamachinga, ukienda namba 68, ukienda Kilombero, ukienda kila mahali vurugu kila mahali. Kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri pia aongeze jicho kubwa kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulikuwa tuna ushauri, kama kama kuna baadhi ya masoko ya Machinga yanafungwa saa kumi na mbili na yanafungwa saa moja, tutafute baadhi ya barabara jioni ambazo hazitumiki sana na watu tuzifunge zile barabara, wale wafanyabiashara wadogo wadogo kuanzia saa kumi na mbili waruhusiwe kufanya biashara pale wapate riziki zao; maana mgambo

wanawanyanganya vitu mpaka saa tano usiku. Hebu mniambie ukimnyanganya mtu muda huo unavipeleka wapi ilhali mtu anatafuta riziki kwenye maeneo yale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna watu wanahusika na masuala ya *parking*. Wako wanaofanya biashara ya *parking* na kila mwananchi analipia *parking* kila siku, lakini wanashindwa kulipwa mishahara yao mwezi mmoja miezi miwili. Ukiangalia leo tangu Februari na Machi hawajalipwa ilhali ukiangalia fedha imeshaingia Serikalini. Kwa hiyo tuwaombe Serikali mkae na yule mzabuni kila mwisho wa mwezi wale wafanyakazi Watanzania wenzetu wa Arusha maskini wapate haki yao ya ujira wao kama wakati unavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kumalizia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gambo, muda wako umeisha.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sekunde chache kumalizia.

**MWENYEKITI:** Sekunde moja malizia Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza wewe binafsi, pia naishukuru Serikali yetu kwa kutenga shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kukarabati Soko la Samunge, shilingi 1,000,000,000 kukarabati soko kuu na shilingi 1,000,000,000 kukarabati soko letu la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana na namtakia Mheshimiwa Waziri…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Gambo Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, atafatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Neema William Mgaya ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mchango wangu katika Wizara ya TAMISEMI. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na kutembelea katika majimbo yetu kuja kufanya ziara kwa ajili ya kuangalia changamoto ambazo ziko katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Mkoa wa Dar es Salaam na ninatoka Wilaya ya Ilala ambapo majimbo yetu majimbo mawili, Jimbo la Segerea pamoja na Jimbo la Ukonga yako pembezoni mwa mji. Katika majimbo yetu haya mawili kuanzia juzi na jana hali sio nzuri na kwa sababu Mheshimiwa Waziri anaijua vizuri Dar es Salaam na yeye mwenyewe ametokea Dar es Salaam kwa kweli anakielewa ninachokiongea. Nimekuwa nikichangia hapa kwa muda wa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2020, 2021, 2022 na leo 2023 kuulizia mradi wa *DMDP* ambao ulikuwa utekelezwe 2021 na haya matatizo yote yanayoendelea Mkoa wa Dar es Salaam na mpaka sasa hivi unamwona Mbunge mwenzangu Jerry Slaa hayupo hapa, si kwa sababu hayuko anatembea, yuko katika Jimbo lake kuna mafuriko makubwa sana, na pia Mheshimiwa Zungu naye hayupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam hata mvua ikinyesha Kisarawe maji wa Kisarawe yote yabakuja katika Wilaya ya Ilala *especially* kwenye Majimbo ya Segerea, Ukonga pamoja na Jimbo la Ilala. Na ni kwa nini haya maji yanakuja pale? ni kwa sababu kuna miundombinu mibovu; ukianzia mifereji mpaka barabara zetu ni mbovu. Kwa hiyo tulikuwa tunautegemea sana sana Mradi wa *DMDP* ambao

tumeambiwa kila mwaka unatekelezwa, kila mwaka unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaongea hapa, tumeshampeleka Mheshimiwa Waziri tumemwonesha sehemu tunazotoka, hali ni mbaya sana. Kwa mfano katika Jimbo la Segerea Kata ya Buguruni, Kata ya Bunyokwa, Kata ya Vingunguti; na kwa Kata ya Vingunguti juzi wananchi pamoja na Mnyamani wananchi wameshindwa kutoka ndani, imebidi tuombe usaidizi kutoka kwa kampuni ya *SGR* ambao wanatengeneza barabara ili waweze kutusaidia kutoa yale maji. Hali ni mbaya; na yote hiyo sio kwa sababu yoyote ni sababu ya mifereji mibovu na michakavu ambapo kila wakati mmesema kwamba mnakuja kuturekebishia hii mifereji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana wewe ulikuja katika Jimbo letu la Segerea pia ukaenda mpaka Jimbo la Ukonga kuangalia hali ilivyo. Wananchi wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam hakuna biashara yoyote wanayoifanya kama mvua ikinyesha. Mvua ikinyesha siku mbili, mfano kama jana na juzi, pamoja na leo nimesikia mvua inanyesha, hakuna watu wanaoenda kufanya kazi, hakuna mama ntilie anayepika chakula, hakuna bodaboda wanaofanya biashara na hawa wote wanaingiza kipato pia wanaiingizia kipato Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mkoa wa Dar es Salaam ni mji maarufu pamoja na kwamba si makao makuu. Watu wote wanaoishi Dar es Salaam wanategemea kufanya biashara lakini pia kuna wawekezaji wanatoka sehemu mbalimbali. Kwa jana na leo mwekezaji yeyote akija pale hawezi kufanya biashara yoyote wala hawezi kutamani kuwekeza, maana yake mazingira ya miundombinu hayamvutii. Maji ni machafu, mirundikano, mifereji michafu, barabara mbovu, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba sana sana, sisi tunaomba sana sana na kwa niaba ya Wabunge

wenzangu hawa ambao hawapo tunaomba Mradi wa *DMDP* uanze, ambao ndio mmekuwa mnatuahidi kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama huu mradi ungekuwa umeanza na Mto wetu wa Msimbazi umetengenezwa basi haya mafuriko yangekuwa hayapo. Kwa hiyo tunaomba, umetuahidi kwamba huu mradi utaanza mwezi wa sita tunaomba uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka niongelee ni jambo la fidia. Katika Jimbo la Segerea kuna wananchi ambao walipisha *airport,* ninamshukukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Mkurugenzi wa *TAA* wamelisimamia hili jambo limefikia sasa sehemu nzuri, nilichokuwa ninaomba hawa wananchi wameishafanyiwa tathmini pia pamoja na biashara zao ambazo zilikuwa zinaendelea katika hilo eneo, kama walikuwa wana wapangaji, kama walikuwa wana nini, hao watu wote wameishaondoka, tunaomba sasa Mheshimiwa Waziri hawa watu walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea hapa na Mheshimiwa Waziri kasema kwamba wameishamaliza wanachukua sasa daftari kulipeleka Wizara ya Fedha, sasa tunaomba litakapofika huko Wizara ya Fedha lisije tena likakaa, likakaa tena miezi Sita, kwa sababu sheria inasema baada ya miezi sita tunaanza upya na mtakuwa Serikali mmepata hasara kwa sababu kwenda kufanya tathimini mnawalipa watu wa ardhi, nasi ikifika baada ya miezi sita tunafuta, tunaanza upya kwa sababu vitu vinapanda na sheria inasema kila baada ya miezi sita.

Kwa hiyo, niwaombe kwamba hawa wananchi sasa wamevumilia vya kutosha, tathmini tayari mmeishafanya na imeishamalizika tunaomba ikichelewa sana mwezi ujao wawe wameishapata hela zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusiana na Walimu *especially* ambao wanatoka Jimbo la Segerea. Kuna walimu wengi sana Mheshimiwa Waziri ambao wanapata likizo lakini hawalipwi malipo yao. Mfano, katika Jimbo langu la Segerea kuna karibu Walimu 150 wanadai pesa zao za likizo tangu 2015 mpaka sasa hivi hawajazipata. Sasa walimu wetu wanafanya kazi kubwa sana tunawavunja moyo, tunaomba hawa watu wapewe pesa zao za likizo ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Kwa sababu kumuacha Mwalimu anaendelea kufanya kazi hii halafu akipata likizo hapewi pesa siyo jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri, nawapongeza sana watu wa *TARURA* kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini sasa *TARURA* bajeti yao imekuwa ni ndogo sana. Kwa mfano, katika Wilaya yetu ya Ilala tunaomba kabisa kwamba *TARURA* waongezewe bajeti, bajeti ni ndogo sana na ndiyo maana barabara zao nyingi hawawezi kutekeleza. Kwa hiyo tunaomba katika mambo ambayo yatafurahisha Mheshimiwa Waziri ni kuiongezea bajeti *TARURA,* tumeishasema hatuitaji barabara za changalawe tena Mjini, tunahitaji tupate barabara za lami, kwa hiyo mtakapo waongezea itakuwa ni vizuri hata kwetu sisi ili tuweze kuangalia sehemu ambazo, kama ulivyopita Mheshimiwa Waziri, kwenye Jimbo langu jiografia ya Jimbo langu ina Kata…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umeisha.

**BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninaomba nimalizie suala moja. Mheshimiwa Waziri jambo lingine tunaomba mthibitishe Mkurugenzi wetu ili aweze kufanya kazi akiwa *comfortable. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na

Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara ya TAMISEMI.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wawili, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa TAMISEMI wanafanya kazi nzuri, tunajua kwamba wengi wao ni wageni kwenye Wizara hiyo na ninaamini kwamba wanatafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa utekelezaji wa bajeti kwa kutupa hela nyingi Wabunge wengi likiwemo Jimbo la Bunda ambapo tumepata bilioni 1.650 kwa miradi mbalimbali ya barabara ya Nyamswa – Bunda, barabara ya Sanzati – Nata, barabara ya Makutano – Sanzati na miradi ya afya na miradi ya zahanati. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu ukienda pale mitaani au ukiwa nje ya Bunge wanakuuliza mbona Wabunge, masaa yote mnampongeza Rais? Nadhani elimu iende kwa wananchi, tuwaambie kwamba Wabunge kazi yetu ni kupitisha bajeti, anayetekeleza bajeti na kuamua akusanye fedha ziende kwenye Majimbo yetu ni Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, yeye ndiye ana tekeleza bajeti, kwa hiyo tunamshukuru kwa sababu anatekeleza bajeti vizuri, anakusanya fedha na zinakuja kwenye Majimbo yetu. Kwa hiyo, lazima tufike hapa tuseme huyu tumekupa kazi ya kufanya na hiyo kazi unaifanya vizuri lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kazi anayoifanya nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba sasa tuna Wizara ya TAMISEM) ina Viongozi wengi wapya lakini nawaomba watazame Jimbo la Bunda. Halmashauri ya

Wilaya ya Bunda inajengwa hospitali ya Halmashauri ya Bunda – Nyamswa – Ikizu pale Bukama, tumepewa Bilioni Tatu na Milioni Mia Sita Hamsini toka 2018 mpaka leo hospitali ile ni gofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza maswali mengi sana, huwa nasema hivi Rais anapochaguliwa na wananchi, Rais anaetokana na Chama cha Mapinduzi na Wabunge wa CCM ndiyo wengi humu ndani, halafu akateua Mawaziri ni wa kwake, akateua Wakuu wa Mikoa ni wa kwake, akateua Wakuu wa Wilaya ni wa kwake, Wakurugenzi na Idara mbalimbali ni wa kwake, sasa anapowateuwa wanakwenda na analeta hela kwenye Halmashauri zetu na hela azisimamiwi hivi wanamjengea kura au wana mharibia kura? Najiuliza maswali mengi sana, nasema kama mtu amemteuwa kwenda kusimamia Idara fulani maana yake aliyeniteua anataka nijenge, nifanye kazi nzuri ya ufanisi ili kazi yake na yeye mwisho wa kuomba kura watu wampe kura vizuri. Niwaombe Mawaziri, niwaombe Wateule wa Rais, watekeleze kile walichopewa na Mheshimiwa Rais, kuwateuwa kwa madhumuni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi yanayolalamikiwa na wananchi ni maeneo yanayotekelezwa na Serikali. Chama cha Mapinduzi kipo vizuri sana na tunaamini kipo vizuri masaa yote na muda wowote na miaka yote, lakini utekelezaji wa CCM kwenye upande wa Serikali kuna matatizo yake 3,650,000,000 zipo pale zimelala, amekwenda pale Waziri Ndugange nakushukuru ulikuja pale, umeyatazama pale ilivyo, hali ni mbaya. Juzi wananchi wa Nyamswa – Ikizu, vifaa vimeletwa vimefungwa na Halmashauri wenyewe wamefunga usiku, baada ya siku tatu vimeibiwa! Aliyekuja kufunga ni mwenyewe, aliyetoa taarifa ya wizi ni mwenyewe. Hizo taarifa tumewapa najua mtazifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana, Jimbo la Bunda Kituo cha Afya Mgeta, Kituo cha Afya Onyari, Sekondari ya Vilina na Halmashauri ya Bunda Hospitali naomba mtazame sana. Mheshimiwa Angellah Kairuki wewe unafanya kazi vizuri naomba uende utazame, lakini najiuliza swali moja hivi amezungumza hapa Mheshimiwa Kishimba, anasema tuunde Wizara ya Kero, mi najiuliza kwani Mheshimiwa Waziri na ofisi yako ukisema ukaleta hapa tathimini ukaleta karatasi humu ndani fomu, ukasema Wabunge wote wenye kero jazeni fomu halafu ukatukutanisha kama ulivyofanya Mkoa wa Mara juzi juzi hapa, kwani kuna ubaya gani? Si Waziri wa Kero ni wewe huyo huyo unataka nini sasa? Ni wewe huyo huyo Waziri wa Kero. Kwa hiyo, nikuombe kwamba sasa hili nalo ulitazame vizuri ili uweze kulitazama.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi haya sasa naingia kwenye maombi maana naweza nikaanza nikasahau haya yaliyotokea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Halmashauri ya Wilaya Bunda. Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wengi wamepita pale sana, Wabunge nataka niwaeleze Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ni kama vile mtu anakaa Mkoa wa Morogoro halafu katika hapa Mkoa wa Dodoma halafu mbele yake ni Mkoa wa Singida, Halmashauri ya Bunda iko Jimbo la Mwibara iko Singida, Bunda wako Morogoro, wakitoka Morogoro wafike Dodoma wafike wachukue nauli waende Singida warudi tena Morogoro. Mazingira machafu sana, kelele nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko nchi zimeundwa kutokana na Jiografia yao. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, iliundwa kutokana na Jiografia yake, tunaomba Halmashauri ya Bunda majengo tunayo iliyokuwa Halmashauri ya Bunda ya zamani ya Mzee Wasira, iko pale ina majengo yale tumeyaacha yanateketea, majengo mazuri sana tusaidieni

sisi hatuhitaji majengo tunahitaji Halmashauri na Mkurugenzi awepo pale tuweze kupata Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi mengine niliyonayo ni Zahanati ya Kijiji cha Bigegu sasa naomba haya viongozi wote mnao husika msilikilize vizuri. Hali ya hewa hapo ni mbaya sana, Zahanati ya Kijiji cha Bigegu, Zahanati ya Salakwa, Zahanati ya Mawanga, Zahanati ya Nyaguzume haya ni maeneo hatarashi sana wananchi wa pale watoto wanakufa na malaria umbali wa kituo ni mrefu sana, naomba hilo nalo mlichukue. Naomba Kituo cha Afya Mihingo, Kituo cha Afya Nyamang'uta, Kituo cha Afya Kitale na Salama. Hali ya hewa hapo siyo nzuri kwa upande wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba barabara ya Kambugu – Nyabuzume – Vigutu – Butiama tumeishaiomba sana na Mheshimiwa Sagini, tuunganishe hizo barabara iweze kupita wananchi wa maeneo hayo ambayo wanafanya kilimo cha alizeti. Barabara ya Mikomarilo – Mirwa – Buhemba kule soko la Butiama barabara hiyo inahitajika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara ya Mavunga – Mtaro kwenda Jimbo la Bunda Mjini, barabara ya Mgeta – Salakwa – Maliwanda – Kilawila. Sisi tunazungukwa na Hifadhi ya Serengeti, Grumeti imetuzunguka pale lakini wananchi hawana uwezo wa kwenda kuuza mazao yao kwenye hoteli zile mle ndani, kwa hiyo tunaomba hiyo barabara tuipate ili wananchi waweze kufanya biashara kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije suala nyeti sana, Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusijifanye vichaa, tunaomba tuelewane hali ya madawati kwenye shule zetu za msingi ni mbaya sana, Bunda peke yake madawati 11,840 hayapo! Jimbo la Bunda la kwangu 4,815 hayapo, hata ningetengeneza madawati kwa Mfuko wa Jimbo Milioni 51

nitakaa miaka 11 ambayo wananchi hawawezi kusema kwamba wanakubali au hawakubali, kwa hiyo hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya madawati kwenye nchi yetu siyo kwamba imeanza leo, Awamu ya Tatu ilikuwepo, Waziri Sumaye alitangaza kila mwananchi alitengeneza, wananchi waliungana wakatengeza dawati moja, 2018, 2019 nadhani humu humu Bungeni hata Bunge letu lilichanga tukatengeneza madawati mengi sana kwenye shule, haiwezekani watoto wakakaa chini, haiwezekani watoto wa nchi hii huru wanakaa chini haiwezekana! Tunaomba Serikali mtuunganishe mnaweza mkafanya mambo mawili:

Jambo la kwanza tangazeni kwamba wananchi watengeneze madawati tushirikiane nao tutengeneze; Pili tutumie Taasisi zetu na maeneo ya Serikali kutengeneza madawati. Naomba sana Waziri haiwezekani tukawa Wabunge, humu ndani watoto wa maskini wanakaa chini, haiwezekani! Kwa hiyo, tuangalie hali ya madawati siyo nzuri sana kwenye maeneo yetu.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere ahsante sana muda wako umeisha, nakushukuru sana.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Neema William Mgaya, atafuatia na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kusimama katika Bunge hili la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao hii ya TAMISEMI, kipekee kabisa nimpongeze Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya katika suala zima la kuongeza bajeti ya *TARURA*. Ukiangalia Rais alipoingia madarakani bajeti ya *TARURA* ilikuwa bilioni 275 lakini mwaka wa kwanza wa bajeti ya Rais wa Awamu ya Sita bajeti ya *TARURA* iliongezeka kwa zaidi ya asilimia mia moja na hivi leo tunavyozungumza bajeti hii ya *TARURA* imeongezeka hadi kufika bilioni 778, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ndani ya muda mfupi wa miaka miwili. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwita Getere.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hili neno mnyonge Mheshimiwa Mwenyekiti huwa linatumiwa vibaya, haijawahi kutokea duniani Rais akawa mnyonge. Ahsante. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Neema taarifa unaipokea?

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Naomba niendelee. Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya *TARURA* imeongezeka mpaka kufikia hiyo bilioni 7,78 lakini bado kuna changamoto katika utekelezaji kwa baadhi ya maeneo katika suala zima la Wakandarasi. Kuna baadhi ya Wakandarasi wanapewa kazi

maeneo mengi lakini ili hali uwezo wao wakufanya kazi unakuwa mdogo, hivyo ufanisi wa kazi unakuwa hauonekani lakini vilevile kunakuwa hakuna tija kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba tuwape Wakandarasi kazi kutokana na uwezo waliokuwa nao, mwenye uwezo mdogo apewe kazi ndogo, mwenye uwezo mkubwa apewe kazi kubwa, isiwe mtu anafanya kazi kijanjajanja akisikia Songea wanalalamika anahamisha mitambo kutoka Lindi anapeleka Songea, hapo hatutafika kwakweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nichukue nafasi hii sasa kuomba maombi katika Halmashauri zetu za Mkoa wa Njombe. Nikianzia na Halmashauri ya Wilaya ya Makete, naiomba Serikali ituongezee pesa katika barabara inayotoka Kipengele kwenda Lupila barabara ya zaidi ya kilomita 30 *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu mvua inanyesha miezi nane theluthi mbili ya mwaka mvua zinanyesha tu, ukizingatia kule Lupila ndiyo wazalishaji wakubwa wa viazi pamoja na mbao. Kuboreshwa kwa barabara hii kutasaidia mlaji wa mwisho wa kule Dar es Salaam ninyi mnaopenda kula *chips* Dar es Salaam watapata kwa bei nafuu. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba barabara hii inaboreshwa kwa maslahi ya Watanzania kwa ujumla pamoja na wananchi wa Makete. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba pia Serikali ituongezee pesa katika kuboresha barabara ya Makete – Isaplano kilometa 12 kule Halmashauri ya Makete, vilevile katika Halmashauri ya Wanging'ombe naiomba Serikali ituongezee pesa kama milioni 870 hivi kwa ajili ya kuboresha barabara inayotoka Malangali kwenda Wangama kilometa 15 kwenye mradi mkubwa wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TARURA* wasisahau Waziri Mkuu alikaa na Watendaji wote wa *TARURA* Tanzania nakuwapa maelekezo kwamba namna ya kuboresha barabara za Vijijini Nyanda za Juu Kusini, ichukuliwe kwa namna ya kipekee kutokana na wingi wa mvua katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini. Napenda niwakumbushe hilo na wazingatie hayo maelekezo ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye afya msingi. Nimpongeze Rais wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kujenga Vituo vya Afya, Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Zahati zetu lakini naomba nitoe ushauri kutokana na changamoto hii Wauguzi na wafanyakazi wa Kada ya Afya ambao kila Mbunge anaesimama anaizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Wizari hii ya TAMISEMI ikae pamoja na Wizara ya Utumishi waone namna ya kuongeza wafanyakazi, watumishi wa Kada hii ya Afya katika vituo vyetu vya afya, zahanati zetu, hospitali zetu ili kuweza kuleta tija katika suala zima la majengo haya ambayo tayari tumeishayajenga katika maeneo mbalimbali ya Kata zetu, Wilaya zetu na Mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Wanging'ombe mahitaji ya watumishi wa Kada ya Afya ni 1,051, mpaka sasa hivi waliokuwepo ni watumishi 342 sawa na asilimia 32.6 kupungufu ya watumishi 709 ambayo ni sawa na asilimia 67.4. Tunaiomba Serikali ituangalie Halmashauri hii ya Wanging'ombe kwa jicho la huruma tuweze kupata watumishi hawa hili tuweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi wetu, sambamba na katika Halmashauri ya Makete kuna upungufu, Halmashauri ya Njombe Mji, Njombe Vijijini, Halmashauri ya Ludewa pamoja na kule Makambako. Kwa ujumla Mkoa wetu wa Njombe tuna upungufu mkubwa wa watumishi wa Kada ya Afya, tungeiomba Serikali ituongezee watumishi hawa wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye elimu msingi. Niseme tu kazi kubwa imefanyika katika Awamu hii ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, mtakumbuka ndani ya mwaka mmoja alijenga madarasa karibia 15,000, madarasa 12,000 kwa shule za sekondari, madarasa 3,000 kwa shule za msingi na hii ilitusaidia hata watoto wetu kutokwenda *second selection* kwa wale wa sekondari lakini vilevile kwa wale wa elimu ya msingi ule umbali wa kutembea kwenda kutafuta shule umbali mrefu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amejitahidi sana kupunguza umbali kwa watoto wetu kutembea kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto, changamoto inarudi palepale kwenye wafanyakazi. Walimu hatuna wa kutosha ndani ya Mkoa wetu wa Njombe, Halmashauri zote Sita, hasa changamoto ya walimu wa sayansi imekuwa kubwa sana katika Mkoa wetu wa Njombe katika Halmashauri zetu zote Sita kwa maana Halmashauri ya Wanging'ombe, Makete, Ludewa, Njombe Mjini, Njombe Mji na Makambako. Kama unavyojua ulimwengu wa sasa hivi ni ulimwengu wa sayansi ni vyema tukawandaa watoto wetu waweze kukabiliana na ulimwengu huu wa sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika suala la mikopo ya asilimia kumi. Nampongeza Mheshimiwa Rais…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Amar.

**T A A R I F A**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba upungufu wa walimu wa sayansi siyo wapi huko anakosema Njombe, ni

kwa nchi nzima upungufu huu upo ikiwemo pia na Nyang'hwale.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Neema, muda umeisha basi malizia sekunde mbili.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Kwa kumalizia napokea taarifa yake na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema, ahsante sana. Nimuite Mheshimiwa Restituta Mbogo atafuatia na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Dunia kwa kutujalia uhai, leo hii tuko hapa Bungeni tunachangia hoja ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya kuwatumikia Watanzania. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Angellah Kairuki na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Festo Dugange na Naibu wake Mheshimiwa Deo Ndejembi. Wote kwa pamoja nawapongeza kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuzungumzia kazi alizozifanya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda wa miaka miwili katika upande wa TAMISEMI. Mheshimiwa Rais kwa upande wa TAMISEMI ameshughulikia sana masuala ya afya ya binadamu kwa maana anawapenda Watanzania. Mheshimiwa Rais amehakikisha zahanati 1,066 zinajegwa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hajaishia hapo, ameweza kuhakikisha Hospitali za Wilaya 135 zinajengwa nchini Tanzania. Mheshimiwa Rais hajaishia hapo, ameweza kuhakikisha vituo vya afya 713 vinajengwa. Mheshimiwa Rais hajaishia hapo, ameweza kuhakikisha majengo ya dharura *(EMD)* 80 yanajengwa nchini Tanzania. Mheshimiwa Rais hajaishia hapo, ameweza kuhakikisha vyumba vya dharura *(ICU)* 28 vinajengwa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hakuishia hapo, ameweza kuhakikisha kwamba nyumba za watumishi 450 zinajengwa nchini Tanzania. Mheshimiwa Rais kwenye suala la afya hajaishia hapo, ameweza kutoa vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 250. Mheshimiwa Rais hajaishia hapo, ameweza kuhakikisha kuna ajira 10,324 nchini Tanzania. Makofi kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo imefanya jumla ya Shilingi bilioni 600 kutumika kwenye masuala ya afya nchini Tanzania. Hili ni jambo kubwa, Mheshimiwa Rais amejali afya za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu vitu hizi Mheshimiwa Rais amevifanya kwa muda wa miaka miwili tu tangu alipoingia madarakani. Mheshimiwa Rais hajaishia hapo, kwenye suala la elimu nchini Tanzania amehakikisha kwamba zinajengwa Shule maalum mpya za Sekondari za wasichana kwenye mikoa yote, na kila mkoa umepewa shilingi bilioni nne na shilingi bilioni 10 zimeshatolewa, na shule nyingine zinaendelea kupata fedha hizo, kwa maana ya kwamba, kila mkoa utapata shilingi bilioni nne kujenga shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hajaishia hapo, kumekuwa na ujenzi wa vyumba vya madarasa 23,000 nchini Tanzania. Hili ni jambo la kumpongeza Mheshimiwa

Rais. Pia kumekuwa na ujenzi wa shule za sekondari na msingi ambazo zinaendelea nchini Tanzania chini ya juhudi za Mheshimiwa Rais. Ni *obvious* lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kasi hii ya miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, kwenye suala la miundombinu tumeona barabara za vijijini zikijengwa na zikiimarishwa kwa maana kwamba tumeona *TARURA* wakipewa pesa kuimarisha barabara za vijijini na mijini. Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba akina mama kutoka vijijini wataweza kufika mjini kupata huduma zao za afya au kama wana mahitaji zaidi.

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye Mkoa wangu wa Katavi. Kwenye suala la elimu, naiomba Serikali…*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Restituta, mimi ni Mwenyekiti sio Makamu Mwenyekiti.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Samahani Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la elimu kwa Mkoa wangu wa Katavi tunaipongeza Serikali, madarasa yanaendelea kujengwa. Nina ombi kwa Serikali. Ombi langu ni moja, ninaiomba Serikali iangalie suala la madawati. Nitoe mfano, pale Mpanda Mjini tuna Shule ya Msakila, ina upungufu wa madawati 400. Watoto wa darasa la kwanza wanakaa chini, chekechea wanakaa chini, darasa la tatu wanakaa chini na darasa la nne wanakaa chini. Pia wana Mwalimu wao Mkuu; Mwalimu Didas anajitahidi kuwafundisha watoto hawa, mpaka hii shule ni miongoni mwa shule bora kwenye Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Shule ya Shanwe ina upungufu wa madawati 447. Naiomba Serikali, inapotupatia vyumba vya madarasa iangalie utaratibu wa kuziambia

Halmashauri ziweze kuchonga madawati. Napenda kusema kwamba, niliwahi kumwuliza Makamu Katibu Mkuu Mheshimiwa Musonda, alisema kwamba suala la madawati ni suala la Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba basi Halmashauri zipewe Waraka ziweze kuchonga hayo madawati kwa sababu ukichukua mfano Shule ya Shanwe ni shule ya miaka mingi, imeanza toka mwaka 1961 lakini ina miundombinu mibovu, madawati hamna, na ina vyumba vitano. Ina uhitaji wa vyumba 12 vya madarasa, lakini sasa hivi ina vyumba vitano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia pia, ni suala la matundu ya vyoo. Shule zetu nichukulie mfano, Shule hii ya Msakila, ambayo ni shule nzuri sana pale Mpanda Mjini, ina wanafunzi 2,300, lakini shule hii ina matundu ya vyoo 10 tu. Unaweza ukafikiria mwenyewe uhitaji wa wanafunzi 2,300 kwenda kwenye matundu ya vyoo 10, hali inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, wakati tunakwenda kupata majengo mazuri ambayo tunajengewa sasa hivi, na Mheshimiwa Rais wetu amejitahidi kupata fedha za kujenga majengo hayo, tunaomba pia miundombinu ya vyoo izingatiwe. Darasa linapokwisha, madarasa yanapoongezeka, tunaomba pia masuala ya vyoo, maana ndio afya ya msingi ya shule, yazingatiwe. Pia masuala ya madawati yazingatiwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda wako umeisha Mhehsimiwa.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza na Mheshimiwa Ally Makoa, ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nishiriki na Wabunge wenzangu kuanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha anatupatia fedha nyingi za miradi ya maendeleo. Sisi Wabunge kama Wabunge pamoja na Madiwani na wananchi kwa ujumla angalau sasa tunasimama kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote wa TAMISEMI kwa kazi kubwa wanayoifanya kusimamia fedha hizi na kuhakikisha angalau yale makusudio na matamanio ya wananchi ya Mheshimiwa Rais yanafikiwa kwa wakati wake. Nachukua nafasi kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa fedha ulizonipa hasa kwenye upande wa elimu na *TARURA*. Mwezi uliopita nilikuwa naadhimisha uzinduzi wa madaraja ya kihistoria ndani ya Wilaya yangu, ni kwa sababu ya utendaji mzuri wa Mheshimiwa Rais, pia na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu walionitangulia kukuomba Mheshimiwa Waziri uone namna ya kuongeza fedha kwa watu wa *TARURA* hasa kwenye miradi ya kimaendeleo. Fedha hizi Mheshimiwa Waziri, *TARURA* ndiyo msingi wa kila kitu kwa wananchi, inatusaidia kutuunganisha kati ya Kijiji na Kijiji, Kata na Kata, na pia inasaidia sana wananchi wanyonge pale wanapotaka kusafirisha na kufanya shughuli zao za kiuchumi. Naomba ulione hili na namna ya kuwaongezea fedha hasa kwenye miradi ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia hapa Mheshimiwa Waziri, kwangu kwa Mkoa wa Mara wote ukiacha Wilaya ya Rorya tu peke yake, sijaona fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa upande wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninayo madaraja mawili pale yanaunganisha kati ya Kata na Kata kwa maana Nyakorogo, kuna Komaswa na pia inaunganisha Kata ya Kigunga na Kata ya Nyaburongo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, haya madaraja mawili tuliyoyaomba sisi watu wa *TARURA*, na watu wa TARURA tukayaweka kwenye *file* la miradi ya kimaendeleo, unipe fedha ili niweze kutimiza haya madaraja mwishoni niunganishe na yale madaraja ambayo umeshanipa fedha ili tuweze kutekeleza yale ambayo yanatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anatimiza wajibu wake. Kazi yetu sisi kama Wabunge, viongozi wa kisiasa pamoja na watumishi, katika wajibu wa Mheshimiwa Rais wa kupeleka fedha ni kuhakikisha fedha inapokwenda kwenye miradi inasimamiwa ipasavyo na inazaa matunda. Tutakuwa Bunge ambalo halitakuwa lina matunda mazuri kama itakuwa kila tukisimama tunamsifia Mheshimiwa Rais kwa kupeleka fedha, lakini kule inapokwenda, usimamizi wa miradi ya maendeleo; moja, haikamiliki lakini mbili, inapigwa na inaliwa hadharani na watumishi ambao kimsingi wameamua kutoendana na kasi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kupitia Bunge hili kama viongozi wa kisiasa, pamoja na kusifia fedha nyingi zinazopelekwa na Mheshimiwa Rais, tutimize wajibu wetu kwa kuhakikisha angalau zile fdha zinazaa matunda. Kabla hata ya kusubiri taarifa ya *CAG*, Sisi tuwe ni watu wa kwanza kuhakikisha zile fedha angalau zinazaa matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Profesa, Mbunge wa Kahama, alisema neno zuri sana. Mbwa mzuri ni yule anayebweka kabla mwizi hajaiba, lakini mbwa ambaye anabweka baada ya mwizi kuwa ameiba, yule anakuwa sio mbwa. Kwa kifupi ni kama wale mbwa tunaowaita mbwa koko. Sisi hatutaki kwenda kwenye masuala ya mbwa, tunataka twende kwenye udhibiti wa fedha za umma zinavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Mheshimiwa Waziri unisikilize vizuri. Tunayo Hospitali ya Wilaya pale, imejengwa toka mwaka 2017. Awamu zote hizi, fedha imekuwa ikienda tumepelekewa jumla ya zaidi ya Shilingi bilioni 3.1 kwa ajili ya kujenga majengo 14 na ile Hospitali iweze kufanya kazi. Mheshimiwa Rais, Mama Samia kwa awamu yake peke yake, ametupatia shilingi milioni 500 na akatupatia tena shilingi milioni 800 kwa nia njema kabisa kuhakikisha yale majengo yanakamilika na yanawasaidia wananchi. Leo ninavyozungumza na wewe, majengo yote 14 hakuna jengo hata moja lililokamilika kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukajiuliza, hizi fedha zinakwenda kwa ajili ya kutimiza, na hii ni bajeti ambayo inapangwa kwenye maeneo mengine ya Halmashauri nyingine; kwa nini Halmashauri nyingine wakipewa shilingi milioni 500 wana uwezo wa kukamilisha majengo matatu, lakini Wilaya ya Rorya haiwezi kukamilisha majengo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili Mhehsimiwa Waziri alitizame kwa jicho la upana. Umemsikia Mbunge Mheshimiwa Getere anazungumza hapa; ukimsikiliza Mkuu wa Mkoa na nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Mara, toka amefika ni miongoni wa Wakuu wa Mkoa ambao wamekuwa wakisema miradi ya maendeleo kwa Mkoa mzima wa Mara haikamiliki. Fedha zinakuja lakini hazikamilishi miradi. Moja ni hiyo Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, alikuja akaona. Katika sehemu ambazo zina vichekesho ukifika Mkoa wa Mara, ni Hospitali ya Wilaya ya Rorya. Inakuja fedha, shilingi milioni 500 ya kujenga madarasa matatu, mtu hajaanza kuchimba msingi, amenunua bati, na ananunua bati *over estimation* inayotakiwa. Kama bati zinatakiwa 100, anaomba bati 200. Anajenga shilingi milioni 500 inakuja; unamletea shilingi milioni 800, vile vilivyobaki stoo, hahami navyo kwenda kujenga kwenye miradi mingine, anakwenda kununua kwingine ili kupata 10%. Vitu vinabaki stoo, vinaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba mpaka mwisho fedha zinakwenda, miradi haikamiliki. Tunasubiri taarifa ya *CAG* ili aje aseme, ndiyo tuanze kuzungumza ndani ya Bunge wakati tuna uwezo wa kwenda na kudhibiti na kuchukua hatua kwa mtu yeyote ambaye anaharibu na anaharibu jina la Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri na nimekuwa nikikuomba sana, kwanza ufanye ziara ya kutembelea Hospitali ya Wilaya ili uweze kuona haya yanayofanyika pale, kwa nini Hospitali za Wilaya hazifanyi kazi? Kwa nini tumepewa zaidi ya shilingi bilioni tatu, maeneo mengine Hospitali za Wilaya zimezinduliwa, kwa nini Mkoa wa Mara na Rorya Hospitali hizi hazifanyi kazi? Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri hili aweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwenye kichekesho hicho hicho, sisi tulikaa na Baraza la Madiwani. Tumeanzia Kamati ya Fedha, tumekaa Baraza la Madiwani, tumepitisha Bajeti ya makadirio na makusanyo ya mapato ya ndani. Sisi ndio tumedhamiria kwamba kiasi hiki tunakusanya kama fedha za mapato ya ndani. Tumejiwekea shilingi bilioni 1.7,

inakuja huku kwenu, inapunguzwa, mnasema hawawezi kukusanya 1.7, wakusanye 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, kwa hiyo, tunamfurahisha nani? Kama sisi tumefanya tathmini ya Baraza la Madiwani ambalo liko kikanuni na kisheria, limepitisha shilingi bilioni 1.7 ambayo tutakusanya kwa mwaka, na ninyi ndio mnawaambia Baraza la Madiwani wasimamie mapato na matumizi na mianya inayopoteza mapato; wameazimia kwamba sisi tunataka tu tukusanye shilingi bilioni 1.7, inakuja huku mnasema, hapana, tunawawekea shilingi bilioni 1.5. Nimeona hapa mnatuwekea shiligi bilioni 1.5 ya mapato ya ndani. Najiuliza, hii mmeitoa wapi? Inatoka wapi kama Baraza la Madiwani lenyewe limekaa na wataalamu, wamedhamiria kukusanya shilingi bilioni 1.7? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa madhara yake ni nini? Mwishoni ndiyo mnakuja kutuweka kwenye asilimia 20 ambayo alikuwa anaizungumza Mbunge mmoja hapa, kwamba fedha ya maendeleo itaenda asilimia 10, fedha ya mikopo ya vijana itaenda asilimia 10. Mmetutoa kwenye asilimia 40, mmetupunguzia fedha ya mapato yetu na kuwa madogo na wakati sisi mapato yetu tumeweka shilingi bilioni 1.7, ninyi mmeshusha, mmeweka shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwaomba Mheshimiwa Waziri, kwanza, irudi shilingi bilioni 1.7 kama ilivyopitishwa na kikao halali cha Baraza la Madiwani, na pili asilimia 40 ambayo ilikuwa inaenda katika miradi ya maendeleo, iende kama ilivyopangwa ili kuimarisha na kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo ya wananchi wetu inazinduliwa na fedha ya Serikali inatumika vizuri.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka nimpe taarifa tu Mheshimiwa Jafari kwa anachokisema cha kuweka shilingi bilioni 1.7 *then* ikashuka kuja shilingi bilioni 1.5. Huo umekuwa ni ugonjwa ambapo wanajiwekea malengo madogo hafu baadaye wanakuja wanasema tumekusanya zaidi ya asilimia mia moja na kitu, kwamba tumefikia malengo zaidi ya asilimia na kitu. Kwa hiyo, ni ugonjwa ambao uko nchi nzima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Chege, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo. Hili ndiyo kusudio; na ukisoma taarifa ya *CAG* ameizungumza hii hadharani kwamba Halmashauri nyingi zinajiwekea mapato madogo ili mwishoni wakikusanya asilimia 50 wafurahi na kujipongeza. Tunajiuliza, tunamfurahisha nani? Kwa sababu kwa kufanya yale, siyo tu kwamba tunataka kumfurahisha mtu, tunapunguza fedha ambazo zingekwenda kwenye miradi ya maendeleo inayowagusa wananchi. Sasa angalia mnatuambia asilimia 10 ndiyo iende shughuli za maendeleo, haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwanza irudishe, lakini pili, kama siyo Wizara yako imefanya hili, kuna mtu ambaye ali-*temper* na maelekezo na maazimio ya Baraza la Madiwani, mchukulie hatua. Mheshimiwa Waziri kwenye hili nakuomba sana uwe mkali ili kuweza kurudisha haya tuliyokuwa tunayazungumza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Makoa, na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache juu ya hoja iliyoko mezani kwetu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara kubwa sana, ni *giant* na ndiyo inayohudumia wananchi katika maeneo ya elimu, afya na huduma nyingine. Tunaweza kusema kwamba TAMISEMI kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba inatimiza malengo ya Serikali Kuu, kuhakikisha kwamba basi huduma zinazopaswa kutolewa kwa wananchi zinatolewa na kwa usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara ya TAMISEMI sasa hivi ina timu nzuri; *with special compliments* kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Dugange, ahsante sana. Mimi niko kwenye Kamati ya *LAAC,* umekuwa ukizunguka na sisi; na huyu mwingine mgeni naye alikuwa kusini *this time*. Kwa hiyo, tumekuwa naye beneti kwa kweli. Kwa hiyo, mambo nitakayoyasema hapa ninaongezea kwa sababu amekuwa *part and parcel* ya kazi yetu, kwa hiyo, anaielewa na nina uhakika atakuwa ameshapeleka taarifa hizi ambazo tunazikuta huko chini katika Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niungane na Mbunge wa Rorya kuhusu miradi hii isiyokamilika na imepewa pesa nyingi. Anapoongelea tuseme Hospital ya Wilaya ya Rorya, ukienda Kusini Magharibi huku, Hospitali ya Mlele,

Hospitali ya Sumbawanga, Hospitali ya Mpanda, Hospitali zote hizi zimejengwa mwaka 2017/2018 mpaka leo majengo yametelekezwa, hakuna kazi inayofanyika, hakuna chochote. Yaani unaweza kuona ni kwa nini Serikali imepeleka fedha huko? Wameenda kujenga hospitali kwa ajili ya nani? Kwa hiyo, tunaomba hizo Hospitali zijengwe zikamilike na kama mnaona haziwezi kukamilika, basi toa pesa kidogo kidogo ili wajenge majengo matatu yatumike, waongeze mawili yatumike ili wananchi waweze kupewa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee mambo ya usimamizi wa fedha hizi. Vipo vitengo mbalimbali. Ndani ya Wizara ya TAMISEMI, kuna kitengo cha usimamizi na ufuatiliaji ambacho kingeweza kufanya kazi kabla ya Bunge Kwenda. Ukija kuangalia ni kwamba, taarifa hizi kama sio *CAG,* basi ni Bunge limeenda. Kwenye Wizara hizi, hasa Wizara TAMISEMI kipo kitengo cha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi na fedha za Serikali, lakini kitengo hiki hakipewi fedha. Tunaomba Wizara itoe fedha ili hawa watu watoke maofisini. Kwa mfano, *this time* tumekwenda nao, ni kama tumewanyanyua sisi. Tumesafiri nao, na wengine wamesafiri hata kwenye basi letu! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Jamanii!

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Ee!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inaonesha waziwazi kwamba hawa watu wanataka kufanya kazi lakini hakuna pesa inayotolewa ili waweze kufuatilia kazi hizi ambazo zinapaswa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kitu kinaitwa *force account* katika usimamizi. *Force account* iliundwa ili kupunguza gharama za utengenezaji miradi au uendeshaji miradi au ujenzi wake. Sasa hivi *force account*

badala sasa ya kupunguza gharama, imeongeza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama ule muongozo wa *PPRA* wa *2020* haujazuwia mkandarasi pale ambapo kuna *negotiation* Ukienda maeneo mengine hakuna mafundi na hili ndio, *local fundi* maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linatumika vibaya, unaenda kwenye maeneo mengine hakuna mafundi kabisa. *Local fundi* ni yule mtu ambaye ana uwezo wa kujenga, kusimamia na kuhakikisha kwamba, mradi unafanikiwa. Sasa ukienda kwenye maeneo mengine ili mradi wamesema *local,* wanasema labda anatoka kwenye Kijiji, Hapana. Huyu *local fundi* anaweza kutoka katika Halmashauri nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika *regulations* za *PPRA* hakuna mahali ambapo mkandarasi amezuiliwa. Wakandarasi wanatakiwa wakubaliane na zile pesa ambazo zimetolewa ndani ya halmashauri. Kama mna milioni 500 mnaweza kumwambia tunajenga majengo matatu, unafanyaje? Yeye atajikoki yeye mwenyewe, akisema milioni 400 mpeni 400, akisema 350. Lakini ninachotaka kutahadharisha ni kwamba, mtu anapoharibu jengo kwa kutumia *force account* huwezi kubomoa, lakini kwa mkandarasi atawajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba tufikirie, sijasema *force account* haijafanya kazi vizuri, inafanya kazi vizuri katika maeneo mengine, lakini mahali pengine imeboronga, miradi ni mibaya na kuna *crisis* huku mbele zinakuja kwamba, kama hii miradi ni mibovu baada ya miaka 10 au 20 nyumba zote zinaanza kuporomoka kwa hiyo, tunakuwa tunafanya kazi bure katika kuhakikisha kwamba, tunajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tukubaliane. Na ninaposema kumsifu Mheshimiwa Samia, mimi kwa mfano kama sisi tunaoitwa *Covid-19* watu wanaweza kufikiri tunajikomba, hapana, hatujikombi. Na tunatahadharisha mitandao huko sisi hatujikombi hata kidogo, tunamsifu mama amefanya kazi na ana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kazini na tunataka kuwaambia huko kwenye mitandao, *we are women at work,* tuko kazini, tunawakilisha Watanzania hatuwakilishi familia. Kwa hiyo, tunaposema ni lazima sisi kama wawakilishi wa nchi na tuko hapa kihalali, kama kuna mtu anatupinga tuko huko kwenye *Court Room,* eeh. Kwa hiyo, ni lazima tutachangia na tutasimamia miradi ya nchi na tutahakikisha tunafanya kazi inavyotakiwa, ili kuhakikisha kwamba, Watanzania wanapata huduma zinazostahili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Women at work.*

**MHE. CONCHSTER L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes, we are women at work* na tunakwenda na mama. Na alituambia wanawake mpo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mpo, alituambia tukiwa kule ametuita wanawake kwamba, asipofanya kazi vizuri hakuna mwanamke atachaguliwa katika nchi hii. Kwa hiyo, lazima tuunge kazi yake mkono kwa sababu tunaiona, hatuungi tu holelaholela, tunaunga uwezo wa mtu hata kama ni mwanaume na kama anauwezo tutamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nije kwenye TEHAMA. Sasa hivi kuna TEHAMA inatumika katika kukusanya mapato, katika matumizi. Na ninachotaka kuwatahadharisha ni kwamba, ni lazima twende na dunia inavyokwenda, lakini uko wizi mkubwa sana ambao unafanyika kutokana na TEHAMA. Nashauri Serikali na kama mmeanza huu Mfumo wa

TAUSI, kama mlivyosema, lazima kuweko na kitengo cha kudhibiti wataalamu ambao wanaweza kudhibiti. Kwa hiyo, tunaposomesha watoto wetu tuwasomeshe hata *TEHAMA* upande wa mambo ya *cybercrimes* na nini, ili kuwepo na Kitengo cha *Cybercrime* katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoamini, halmashauri haiwezi ikaiba au kufanya miamala iliyoeleweka kama kule TAMISEMI hamuelewi kwa sababu, TAMISEMI ndio inayo-*control* kila kitu. Kwa hiyo, hili jambo Mheshimiwa Waziri uende ulione kwamba, je, inakuwaje Halmashauri wana-*trespass,* wanaiba. Labda wanaharibu miamala huku wanachanganyachanganya miamala, huyu wa TAMISEMI amekaa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na yeye anakuwepo kwa hiyo, na kwenyewe huko muangalie kusudi muweze kusawazisha. Muda ni mfupi…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshikiwa Conchester muda wako umeisha.

**MHE. CONCHESTER L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru. Inatosha kwa leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Juma makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland. Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi, lakini na niungane kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maajabu anayotuonesha sisi Wabunge wa Majimbo katika kazi za maendeleo zinazofanyika. Baada ya kuyasema hayo niwapongeze Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,

Mheshimiwa Rais hajawahi kukosea kwenye Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tulianza na ndugu yetu Mheshimiwa Bashungwa, tunamshukuru tulienda vizuri na sasa tupo na dada yetu tunaamini kwamba, Mwendo uleule ataondokanao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuonesha kwamba, Wizara hii inafanya vizuri wanajiamini sana, hapa nimeshika *document* za kuonesha ni namna gani wametupelekea fedha kwenye majimbo yetu. Ninawapongeza nasema sawasawa, mko vuzuri, kule kujiamini kwenu kunasababisha na sisi kuwaamini ipasavyo, tunawaamini sana. Pamoja na mazuri na makubwa mliyoyasema, changamoto huwa hazipungui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alisikilize hili ninalomwambia na amwambie Katibu Mkuu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambaye naye pia tunamuanini sana, amuandikie mkurugenzi wetu wa Halmashauri ya Mji Kondoa, kufanya mabadiliko kidogo kwenye fedha hizi za *boost* kwa maana ya kwamba, tuna fedha ya kujenga madarasa shule ya msingi Mongoroma, shule hii ya Mongoroma imezidiwa sana, ina wanafunzi 987. Katika wanafunzi hao wanafunzi wanaotoka mtaa huo ni wanafunzi 502, wanafunzi 485 wanatoka mtaa mwingine na wanafunzi 29 kutoka kwenye mtaa huo tunaotaka tujenge hiyo shule wanatembea kilometa 6.5 na hawa wanaokwenda Mongoroma kutoka Selia wanatembea kilometa 4.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tuliona sisi wananchi wa Selia tuanze ujenzi wa shule ya msingi, tunasema shule shikizi, na tumeanza kujenga madarasa mawili na matundu ya vyoo vinne, ili kunusuru hawa watoto wanaotembea kilometa 6 kwenda kusoma shule ya msingi mtaa mwingine. Kwa sababu, naamini ni makusudio ya Serikali kila mtaa uwe na shule ya msingi ili kupunguza umbali, basi nimuombe aruhusu

haya madarasa sita ambayo yanakwenda Mongoroma yakajengwe pale Selia madarasa sita na yale ya kwetu wananchi, yatakuwa madarasa nane na vyoo vyetu vinne tukichukua na hivi vyoo tutakuwa tueweza kuwasaidia hawa watoto wetu na tutakuwa tumefanya jambo lenye tija sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mongoroma kuna madarasa kumi ya shule ya msingi ambayo yote yanatumika. Kwa hiyo, tukiwabakiza wakibaki 500 hawa 400 wengine tukawatoa, watakuwa na sehemu ya kubaki na madarsa yao yanayowatosha wao na wale wa mtaa mwingine tutakuwa tumewasaidia kupunguza umbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimuombe Mheshimiwa Waziri. Tumekwisha kamilisha shule kama mbili shikizi, zina sifa ya kusajiliwa, lakini

tumekuwa wazito sana kwenye kuzisajili hizi shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri hebu wape maelekezo tuzisajili, mbona tumejenga shule ya sekondari hii mpya, tumeisajili mapema na leo tuna kidato cha pili kwenye sekondari yenu ambayo tunawashukuru sana, mmetusaidia sana watu wa Kondoa kupunguza idadi ya wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa walimu pamoja na huduma ya afya, Wizara ya Afya, wauguzi, tuna tatizo kubwa kwenye shule zetu. Ukienda shule moja ya msingi Hachwi unakuta ina mwalimu mmoja na ni shule kongwe. Tunaomba msaidie, *specifically,* tupeleke walimu Shule ya Msingi Hachwi. Na ikiwezekana hizi ajira mpya tuchague sisi wenyewe, yaani sisi tuwapeleke walimu moja kwa moja kwenye shule na ikiwezekana tuwaambie tunatangaza ajira Shule ya Msingi Hachwi, tunatangaza ajira Shule ya Msingi Serengeni,

tunatangaza shule ya msingi hii kwa hiyo, anayeomba ajue kabisa anaomba kupelekwa shule ya msingi fulani na kama hataki akatae moja kwa moja atafutwe ambaye atakubali kwenda *as long* sasa hivi mmefanya kazi nzuri za miundombinu. Kondoa inafikika sehemu zote hakuna haja ya mwalimu kushindwa kwenda kufundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine kutokana na muda, niwapongeze kwa *TARURA*. Kwa kweli, mnafanya kazi vizuri sana, huyu *Engineer* Seif huyu anapaswa apewe hiyo haki yake kwa sababu, hatumsumbui sana isipokuwa kazi zake tunaziona, anapiga kazi sana. Kwa hiyo, tumshukuru, lakinis sasa pale kwetu kuna barabara moja muhimu sana ambayo ni ya kwake, inatoka Iboni kwenda Bilisa, ni barabara changamoto sana. Wananchi sasa wanatembea kwa miguu karibu kilometa saba kuja kutafuta mahitaji mjini, hapo mwanzo kulikuwa na gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madaraja mawili-matatu pale ya kwenda kuyajenga. Hebu tusaidieni tuyajenge madaraja yale mtakuwa mmetusaidia kwa sababu, kwanza barabara yenyewe kwa umuhimu wake ndio barabara pekee ambayo inaweza ikawa mbadala wa barabara ya kwenda mikoa yote, kuunganisha Mkoa wa Dodoma na Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa harakaharaka kutokana na muda, kuna haya mapato ya halmashauri. Sisi tuko Halmashauri ya Mji, Mheshimiwa Waziri usitufundishe uwoga wa kutafuta mapato, tunaomba uruhusu ile asilimia 40 ile ya maendeleo tuendelee kupambananayo kwa sababu, inatusaidia sana na hakuna mahali tunaweza kusema tumefeli, lakini leo kutupunguzia kutupelekea asilimia 20 maana yake hata mikopo ya wale vijana wanawake pamoja na mikopo ya wenye ulemavu itapungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaendelea kuwakopesha milioni tatu, milioni nne, sasa ukipunguza zaidi tutakuja kuwakopesha kiwango kidogo kutokana na hiyo asilimia 20. Tuna uwezo wa kuendelea kujibana tuisaidie Serikali Kuu kufanya miundombinu ambayo tuna uwezonayo, leo tumeweza kujenga angalao zahanati mbili kwa kipindi cha mwaka huu mmoja. Sasa ukipunguza hicho kiwango cha fedha tukawaachia tu watendaji wakaendelea kuzitumia hata Madiwani watakata tamaa katika kusimamia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri turudishieni asilimia 40 ya maendeleo ili wale wananchi tunaokwenda kuchukua kodi zao kule waweze kuona matunda ya fedha wanazolipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi huu wa *tactic,* watu wa Kondoa tunasubiri sana barabara za lami na Taa, tunasubiri sana. Sasa tunaomba utusaidie kwa sababu ni mji, tujenge barabara zetu kwa lami kama jinsi mpango wa Serikali ulivyo kwa hiyo, tufupishie ule urefu wa mradi huu ili tuweze kuupata kwa pamoja na tukienda 2025 tuwe tayari tumekwishaweza kuweka lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia. Mheshimiwa Waziri nikuombe, kabla bajeti hii haijaisha tuwe tayari tumeanza ujenzi wa sekondari mpya ya Bolisa kwa sababu, tuliomba sekondari mbili, moja ile mmetupa tumekamilisha, lakini sasa hii ya Bolisa tunaomba na yenyewe ianze kujengwa kabla ya bajeti hii kuisha. Hilo ukilifanya utakuwa umetutendea haki sana wana-Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, ikumbukwe kwenye hizi sekondari mpya ambazo tumezijenga, ilikuwa ije shilingi milioni 600 mpaka leo zimekuja milioni 470. Tumekamilisha na watoto wanasoma, lakini bado katika yale ambayo tulikuabaliana kwamba, shule hizi zinatakiwa ziwe pia na

nyumba za walimu. Kulikuwa na milioni 130 hatujajua zimekwamia wapi mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri, Serikali ifanye kila la kufanya shule zilizojengwa ni mnzuri sana zitakuwa na fursa zaidi endapo walimu wetu hawatatembea mbali. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri zile milioni 130 ili tumalizie miundombinu, nyumba za walimu, pamoja na mfumo wa maji ambao unasoma katika shule ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana na niendelee kuipongeza Serikali. Shukrani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Makoa. Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katimba…

**MHE. ALLY JUMA MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. nimuite Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katiba. Mheshimiwa Prof. Aloyce Ndakidemi ajiandae.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya, lakini la pili nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambazo anazifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbele sana kwenye mchango wangu, naomba nitoe ushauri kwa dada yangu, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tunapokaa hapa ndani Bungeni tunapokea hizi taarifa za utekelezaji wa bajeti kwenye maeneo yetu na taarifa za mgawo wa fedha. Naomba nishauri kwanza kabla sijaenda

mbele kwenye mchango wangu; taarifa hizi ni nzuri tukizipata kabla ya fedha hizi hazijaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimepokea taarifa miradi kule yote imeshatekelezeka na imeshaisha, leo napokea taarifa, lakini ni vizuri tukiipata mapema inatusaidia na sisi kwenda kusimamia kwenye utekelezaji. Ni ushauri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri kwa kazi nzuri na namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza ilani yetu ya uchaguzi 2025, lakini pia sisi mpaka sasa Mvomero tumeshapokea bilioni 3 na milioni 700 ya kujenga vyumba vya sekondari 187. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake. Lakini nina ombi hapa, haya madarasa tuliyoyajenga shule nyingi hasa za pembezoni hazina walimu. Tumejenga madarasa mazuri, lakini walimu ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, tuna uhaba mkubwa wa madarasa kwenye shule zetu za msingi. Pamoja na fedha tulizozipokea, lakini tuna uhaba mkubwa wa madarasa, lakini pia tuna uhaba mkubwa wa madawati, tuna uhaba mkubwa wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe sana, tunayo maboma ambayo tuliyajenga kwa nguvu zetu na ni maboma mengi sana. Tunaomba maboma haya Mheshimiwa Waziri utuangalie kwa macho mawili utuwekee kwenye bajeti yako mwaka huu kwa sababu, haya maboma mengine yameanza kuanguka. Yako maboma ambayo yamejengwa toka 2017 mpaka leo maboma yale yapo hayajamaliziwa, lakini tunawakatisha tamaa wananchi. Wananchi wanajitolea kwa kujenga wenyewe maboma, lakini Serikali inachukua muda mrefu kuyamalizia haya maboma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niishukuru Serikali, Mheshimiwa Waziri. Mmetupa fedha za kumalizia maboma ya zahanati pale Dihinda, mmetupa milioni 50 na boma lile tumemaliza na zahanati inafanya kazi, pale Ndole mmetupa milioni 50 tumemaliza boma na zahanati inafanya kazi. Chenzema mmetupa milioni 50, lakini mmetupa juzijuzi hapa shilingi milioni 50 pale Kidudwe na zahanati inaendelea na ujenzi. Mmetupa milioni 50 pale Manyinga ujenzi unaendelea. Lakini mmetupa milioni 500 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya pale Mziha na tumepokea milioni 600 kwa ajili ya kujenga pia, kituo cha afya pale Mlali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, bado tuna maboma mengi ya zahanati. Fedha tulizozipokea tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini tunaomba mwaka huu muendelee kututengea fedha kwa ajili ya kumalizia maboma ambayo tunayo katika Wilaya yetu. Pia tunazo nyumba za watumishi nyingi ambazo zimeanzishwa na wananchi, tunaomba pia mtusaidie ili tuweze kuyamaliza haya maboma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye *TARURA,* wenzangu wamezungumza hapa na wamempongeza *Engineer* wa *TARURA* na mimi nimpongeze. Tumepokea bilioni mbili na milioni 600 tumetengeneza barabara zetu, hasa zile za pembezoni, kule ambako ndiko wanatoka wakulima wetu, ndiko ambako tuna mazao ya kimkakati. Hizi barabara tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumezitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu na ombi langu kwenu, hizi barabara nyingine tumeshindwa kwa sababu ya bajeti kufika mwisho. Mfano, barabara ya kutoka pale Magunga kwenda Maskat, ile barabara ina urefu wa kilometa 15, lakini kwa awamu hii tumetengeneza kilometa nane. Bado tuna upungufu pale wa fedha ya kumalizia ile barabara kilometa saba. Kwa hiyo, nikuombe sana

Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yako safari hii usituache, endelea kutupa fedha tumalizie hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, tuna barabara ya kutoka Muhonda kwenda Kweuma. Hii barabara na yenyewe haijafika mwisho kuna kipande kama cha kilometa tatu-nne, tunaomba Mheshimiwa Waziri na hii barabara utuangalie, utupe fedha tuweze kuimalizia hii barabara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali, mmetupa fedha tumeweza kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami pale Dakawa. Tumetengeneza barabara kutoka Manyinga kwenda Madizini kwa awamu ya kwanza yumeishia pale stendi kwa kiwango cha lami. Tunategemea tutaendelea kupata fedha kwa ajili ya kumalizia hizi barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna barabara ambayo tumeitengeneza ya kutoka Sangasanga kwenda Lubungo, tunataka barabara hii iende ikatokee Kilosa. Hii ni barabara ambayo ikiisha itakuwa ni barabara kubwa ya *short cut* kwa wakulima wetu ambao wanazunguka umbali mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kwa sababu ya muda, Dakawa ni eneo kubwa sana la biashara, nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri safari hii mtupe fedha tuanze ujenzi wa soko la kimkakati, Dakawa. Na pale kuna wakulima wengi, kuna wafanyabiashara wengi, tukipata fedha tukajenga soko pale la kimkakati tutawasaidia sana wananchi wetu wa Mvomero, hasa wananchi wa Dakawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jingine nimalizie, fedha zote ambazo tunazipokea sisi Mvomero, hizi za miradi, hasa hii miradi ya sekondari, vyumba vya madarasa na hii miradi ya zahanati, hawa watumishi wetu kwa maana ya watendaji, fedha nyingi zinazokuja, hasa kwenye vituo hivi vya afya mfano pale Mziha tulipopokea milioni 500 fedha ile

haijatosha. Sasa hivi wanasema tuwaongezee bajeti kwa ajili ya kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hizi zahanati zetu ambazo tumepokea milioni Hamsini-hamsini wanasema tuwaongezee fedha za kumalizia baadhi ya maeneo, fedha hazijatosha. Mheshimiwa Waziri nikuombe, kama unataka kweli kumsaidia Mheshimiwa Rais, Imarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani. Kama kuna eneo ambalo tunapigwa na kama kuna mchwa ambao wapo kwenye halmashauri zetu, basi ni hawa wataalam wa haya majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila jengo ambalo limejengwa kwenye Halmashauri lazima utaambiwa fedha ziliongezwa. Mwanzo wanafanya tathmini jengo litaisha kwa milioni 50….

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** zikija milioni 50 wanasema tupe 30 tumalizie.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa maliza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND** Naomba Mheshimiwa Waziri imarisheni kitengo cha ukaguzi wa ndani, mtamsaidia sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Katimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake yote na wenyewe kwa kazi kubwa wanayoifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza maono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo napenda kuchangia ni kuhusiana na masuala ya usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sisi sote ni mashahidi na tunafahamu kwamba katika vihatarishi vikubwa vya kufikia malengo na utekelezaji wa mpango wa maendeleo ni kukosekana kwa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Sisi wote ni mashahidi wa jitihada kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais katika kutafuta pesa nyingi kwa ajili ya kuchochea maendeleo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaweza tukaona kwamba kuna fedha zile za *TCRP,* fedha za UVIKO ambazo zimekuja na zimechochea kwa kiwango kikubwa maendeleo katika sekta za afya, elimu, maji pamoja na wajasiriamali wadogo na tumeona kwamba kwa mfano Wamachinga wanajengewa masoko. Sasa hizi ni jitihada kubwa sana ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hizi tu, mfano mwingine kuna hizi pesa za *ECF (Extended Credit Facility)* ambazo na zenyewe zimeelekezwa kwenye sekta za uzalishaji. Kwa mfano sekta za kilimo, nishati, mifugo na uvuvi; hizi zote ni jitihada ambazo Mheshimiwa Rais anazifanya za makusudi ili kuhakikisha anachochea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili fedha hizi ziwe na tija kuna haja kubwa sana ya kudhibiti upotevu wa fedha hizi katika utekelezaji wa miradi. Natambua jitihada za Wizara, kwanza katika kusimamia halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, lakini pia katika jitihada za kudhibiti mianya ya kuvuja kwa pesa hizo na kudhibiti matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto ya matumizi ya fedha mbichi kwenye halmashauri zetu. Namna pekee au nzuri ya kukabiliana na changamoto hii ni kutengeneza utaratibu wa kutoa mkono wa binadamu katika ukusanyaji wa mapato na ili kutimiza lengo hilo au katika utekelezaji wa lengo hilo, kutengeneza mifumo thabiti ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa sababu imetengeneza mifumo ya TEHAMA, kuna Mfumo wa *TAUSI*, kuna Mfumo wa *MUSE*, kuna Mfumo wa *POS,* yote hii ni mifumo ya TEHAMA ambayo inakwenda kuondoa na ikisimamiwa vizuri itaondoa kabisa changamoto ya upotevu wa makusanyo, upotevu wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mifumo hii iwe na tija, kwanza lazima kuwe na mtandao *(connectivity)* kwa sababu matumizi ya TEHAMA yanahitaji mtandao wa uhakika. Sasa kama kukiwa kuna changamoto ya mtandao ina maana mifumo hii haitakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama huu Mfumo wa *MUSE* ambao ni mfumo wa uhasibu Serikalini ambao unawezesha Maafisa Masuuli kukusanya au kufunga mahesabu ya mwaka kwenye mtandao na uzuri wa mfumo huu ni kwamba zile nyaraka za malipo zinakuwa zinaambatishwa au zinawekwa kwenye mfumo, kwa hiyo inaondoa ile changamoto ya upotevu wa nyaraka ambayo mara nyingi ndiyo hoja za ukaguzi. Anapokuja *CAG* kufanya ukaguzi hoja nyingi zinatokana na upotevu wa nyaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mifumo hii ni mizuri.kwa mfano kuna huu Mfumo wa *TAUSI* ambao mteja anaweza kujihudumia yeye mwenyewe kwenye mtandao, kwa maana ya kuomba kwa mfano kama vibali vya ujenzi au tuseme kulipia viwanja vile ambavyo vinapimwa na halmashauri au kuomba leseni za biashara. Kwa hiyo ili mifumo hii iweze kuwa na tija na tuweze kudhibiti mianya ya upotevu wa hizi fedha nyingi ambazo zinatafutwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya maendeleo, ni lazima kuhakikisha kwamba mifumo inakuwa thabiti na kwamba kunakuwa na mtandao wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja amechangia amesema kuangalia mifumo iwe *airtight,* kusiwe kuna *loophole* yoyote ya upotevu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kuchangia, ni suala la asilimia kumi ile ya mapato ya ndani ambayo inakwenda kwa ajili ya kuwawezesha kimtaji vijana, wanawake pamoja na watu wenye ulemavu. Napongeza sana Serikali na Wizara kwa sababu walibuni ule mfumo wa TEHAMA ambao unaitwa *Ten Percent Loan Management Information System* ambao uliwezesha waombaji wa mikopo hii wafanye maombi hayo kupitia mfumo wa TEHAMA na mchakato ufanyike kupitia TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi bado kumekuwa na changamoto kwa sababu vikundi visivyostahili vimeendelea kupewa hii mikopo, lakini urejeshwa wa mikopo bado umeendelea kuwa ni changamoto. Sisi sote tumesikia maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambaye amesema sasa fedha hizi ziende kutolewa kupitia taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu katika kuboresha au tuseme katika utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais, suala la kwanza, taasisi za fedha ambazo

tutazipa kazi ya kusimamia Mfuko huu, Wizara iangalie kwamba zile gharama za usimamizi *(management fee)* au zile *commissions* za hizi taasisi zisitokane na Mfuko wenyewe zikaenda kupunguza mtaji kwenye Mfuko ule na Serikali iangalie chanzo kingine cha kulipa hiyo gharama ya *management fee.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, programu hii ya kuwezesha kimtaji vijana, wanawale na watu wenye ulemavu ni programu nzuri, lakini kuna *component* moja ambayo ni muhimu sana; kuwajengea uwezo hawa wanufaika wa Mfuko huu ili waweze kuanzisha na kuendeleza biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufanikiwa mfuko huu ni lazima kutenga fungu au kutengeneza programu maalum kwa ajili ya *capacity building,* kutoa mafunzo ya msingi ya namna ya kuanzisha na kuendeleza biashara na kutoa pia msaada wa kitaalam *(technical assistance)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, ni kuvilea vikundi hivi kibiashara, kwa sababu kazi kubwa wanayoifanya hawa maafisa wetu wanaokwenda kufuatilia hivi vikundi ni kufuatilia marejesho, lakini hakuna mtu anayekwenda kufanya *mentorship* kwa hivi vikundi ili viweze kusimama viwe vina biashara endelevu ambazo zitaweza kuajiri vijana, wanawake na watu wengine wengi zaidi, lakini ambavyo vitaweza kuwa na *multiplier effect* kwenye uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika mpango wa muda mrefu, naomba Serikali yote itengeneze utaratibu mzuri kwenye mitaala ya elimu, wanafunzi wanapokuwa wanasoma wapewe mafunzo ya msingi ya namna ya kuanzisha na kuendeleza biashara.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema machache hayo, naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Nianze moja kwa moja kwa kumpongeza sana Waziri wetu, Mheshimiwa Angellah Kairuki na wasaidizi wake wawili, Mheshimiwa Dkt. Dugange na Mheshimiwa Ndejembi na Mkuu wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mkuu wangu wa Wilaya Makori Kisare na *DED* wangu, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Jimbo langu la Moshi Vijijini. Ukweli watatutendea haki na tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ni Wizara mama ambayo ni muhimu sana kwenye maendeleo ya watu wetu, kwa sababu utaona bajeti yake imeongezeka kutoka trilioni 8.7 mpaka trilioni 9.0, karibu asilimia 20 ya bajeti yetu ya Taifa. Ni kutokana na umuhimu wa hii Wizara. Kwa hiyo niwaombe waende wakasimamie hii Wizara vizuri ili hizi fedha zinazotolewa na Rais wetu zitumike vizuri na ziletee wananchi wetu maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais haraka sana; kwamba mama anaupiga mwingi, ametusaidia sana kwenye kuboresha ajira. Tumeona juzi ametoa ajira 21,200. Miundombinu ya afya ni nchi nzima kuanzia hospitali za rufaa, za mkoa, za wilaya, vituo vya afya, zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye elimu; Mama amefanya makubwa sana, madarasa usiseme kitu, nami nimepata hospitali ya wilaya kule, kwa hiyo tunashukuru sana. Mambo ni mengi ambayo Mama amefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na muda, naona leo umebana sana, hivyo, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Katika mchango wangu ntaongelea tatizo la miundombinu ya barabara Jimboni kwangu Moshi Vijijini na pia ntaongelea mambo ya afya kama muda utaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Moshi Vijijini changamoto yetu kubwa ni barabara, ndiyo changamoto kubwa na kule Moshi Vijijini tuna bahati nzuri kwamba tuko milimani na mvua huwa zinanyesha. Hii mvua ni *agent* mkubwa wa kuharibu barabara zetu kule Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, tunaishukuru Serikali kupitia *TARURA* walitutengenezea barabara nyingi, Barabara ya Gate Fonga - Mabogini mpaka Kahe; Barabara ya Boro – Sangiti; Barabara ya Kiboriloni kwenda Mbokomu; Barabara ya Mandaka – Mnono; Barabara ya Uru Madukani – Materuni; Barabara ya Mweka *Junction* – Singa Hospitali; Barabara ya Samanga – Chemchem. Nina masikitiko kidogo, barabara hizi zimejengwa kwa kiwango cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakandarasi ambao wamepewa pesa nyingi kutengeneza hizi barabara kuacha ile ya Samanga – Chemchem, barabara hizi zipo kwenye kiwango cha chini kabisa. Kitu kikubwa ambacho kimetokea nilivyyosema mvua ni *agent* wa kuharibu barabara, ni kwamba hakuna mitaro. Barabara zimejengwa, zimechongwa vizuri, wameweka moramu. Kwa mfano ile ya Mabogini, tumewekeza shilingi milioni mia tatu na hamsini na kitu pale, lakini hata kabla haijaanza kutumika mvua

ilivyonyesha imesafisha ile moram yote kwa sababu hatukuweka mitaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe huu ujenzi ambao umefanyika nimwombe Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake, *Engineer* Seif, hii itawaharibia. Fedha za Serikali zinatumika vibaya na haijakaa vizuri. Tuwatumie ma-*Internal Auditors* wa kwetu wa Wizarani waende wakakague hizi barabara, siyo za kwenye jimbo langu tu, naona Wabunge wengi wanalalamika kwamba barabara hazijajengwa kwa viwango. Tutumie *Internal Auditors* wa TAMISEMI au ikibidi pia *CAG* aende kule aangalie, akague aone kama zile hela zimetumika vizuri. Ombi langu ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi lingine; katika barabara inayokwenda kwenye Kijiji cha Chemchem kupitia Samanga kule Jimbo la Moshi Vijijini, Kata ya Arusha Chini, tulikuwa tumeomba kujengewa daraja linalounganisha hivi vijiji viwili kupita pale Mto Ronga. Bahati mbaya hela zilikuwa ndogo tulitengewa shilingi milioni 475, na pesa hizi zimetumika kutengeneza ile barabara, lakini lile daraja bado haliko kwenye mpango. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, ikimpendeza tunaomba lile daraja litengenezwe ili tuweze kuunganisha Vijiji vyetu vya Chemchem na Samanga ili watu waweze kupita na kwenda kufanya shughuli za uzalishaji kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la pili, ni kuhusu kuiongezea *TARURA* fedha. Kama nilivyosema Jimbo la Moshi Vijijini tuna tatizo kubwa la barabara. Yaani sisi changamoto yetu kubwa ni barabara. Na kuna barabara nyingi ambazo hazijatengenezwa. Niombe kwenye zile hela za tozo, mimi sijatendewa haki pia kwenye hizi hela za tozo; mwanzo ule mgao wa kwanza ulikuwa sawasawa, lakini huu mgao wa pili nimepata shilingi milioni 700 tu na wengine wamepata bilioni moja, bilioni ngapi. Kwa hiyo niombe zile pesa za tozo

tuzigawe vizuri ili niweze kufanya ukarabati wa barabara ambazo nitazitaja hapa kwenye jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambazo ziko kwenye mfumo wa *TARURA* na hali ni mbaya. Barabara inayotoka pale Weruweru Sekondari kupanda Manushi mpaka pale Mrama *Estate;* barabara ya kule Mabogini eneo la Shabaha kwenda *Newland;* barabara ya kule Bonite Relini kwenda Chekereni, Weruweru; barabara ya Kisawio – Uru Seminari – Molangi; hizi ni barabara muhimu chache tu pamoja na nyinginezo. Naomba chonde chonde tusaidiane ili wananchi katika maeneo haya waweze kutengenezewa hizi barabara na wapite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la tatu ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Kuna barabara ambazo zilikuwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi mara tatu, nne, lakini bado hazijakamilika. Kule Moshi wanatuangalia wanasema tusipojengewa hizi barabara kama mlivyoahidi kwenye Ilani yenu ya Chama cha Mapinduzi tutakuwa kwenye matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, barabara ya Gate Fonga – Mabogini – Kahe iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hii ni mara ya tatu haijatengenezwa. Tunaomba Wizara iitengee pesa itengenezwe kwa kiwango cha lami kwani kule ndiko inakojengwa hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili, ni Barabara ya Uru – Mamboleo – Materuni na Uru – Mamboleo – Shingwe; ziko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, zimejengwa kwa mita 300, 400 tu. Niombe sana watufikirie na hizo barabara zijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni ile ya *Kibosho Shine…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa, muda wako umekwisha. Unga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Ndakidemi. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima na Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kupeleka fedha nyingi sana katika majimbo yetu. Kwanza anatafuta fedha, anapeleka fedha zikafanye kazi. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amsaidie Mheshimiwa Rais kusimamia watumishi waliopo katika Serikali za Mitaa lakini pia kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ndiyo nchi, tunamtegemea sana. Ningedhani ungeshona makombati kama wale wenzake wa Kilimo ili ionekane kwamba ni mtu kazi, kwa sababu shughuli iliyopo TAMISEMI ni pevu kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nimesoma bajeti hii sijaona mahali popote ambapo Mheshimiwa Waziri amesema kwenye bajeti hii kwamba anakwenda kukomesha shule kufungwa kwa sababu hakuna matundu ya vyoo, kwa watoto kukaa chini hakuna viti, madawati na meza, Walimu wanakaa mbali kwa sababu hakuna nyumba za kutumia watumishi wa kada za elimu na afya. Hii ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wanavyozungumza kwamba shule fulani imefungwa haina choo, maana yake ni kuonesha kwamba hawa watu siyo wastaarabu na kwa kweli siyo jambo jema sana. Ni ama TAMISEMI wapeleke fedha au yaende maelekezo mahususi kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zetu watenge fedha na jambo hili likomeshwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekuwa msikivu. Kulikuwa na makisio ya fedha ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwenye majengo yetu kuna mabweni hayajakamilika, kuna mabwalo hajayaisha, kuna shule hazijakamilika kwa sababu wali-*underestimate* makadirio ya matumizi ya fedha katika halmashauri zetu, lakini naona wamegundua kwamba walifanya makosa, wameleta *document* hapa kuonesha kwamba angalau darasa moja ni shilingi milioni 25 na matundu ya vyoo yameongezeka. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri kilichobaki hapa ni kupeleka maelekezo mahususi kwamba vile viporo vya mabweni, mabwalo, madarasa na nyumba, fedha zitengwe ili zikamilike ili wananchi waweze kutumia katika matumizi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri afanye ukaguzi maalum wa ile asilimia 40 kwa baadhi ya halmashauri na asilimia 60 ya mapato ya ndani. Miradi mingi kwenye majimbo yetu ambayo viongozi wakienda wanaoneshwa kwenda kukagua na Waziri na Naibu Mawaziri, Waziri Mkuu na Makatibu Wakuu, wanapelekwa kwenye miradi ambayo fedha imetoka TAMISEMI kutoka Serikali Kuu. Tunaomba wakague miradi ya mapato ya ndani ya asilimia 40 na asilimia 60 ambako huo ndiyo mwanya wa upigaji mkubwa sana. Fedha nyingi zimepotea, miradi haijakamilika na watu wanagoma kulipa kodi kwa sababu hawaoni tija ya fedha ambazo wanatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa miradi; nimeona kwenye andiko Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba zinaundwa Kamati ndogondogo za wananchi kwenye vijiji. Hapa kuna changamoto kubwa sana; zinakwenda fedha za miradi, zinaundwa Kamati za Ujenzi za Wananchi, zinaundwa Kamati z Mapokezi na Manunuzi, wanapewa vifaa kwa kuletewa, hawaendi kununua wenyewe wale wananchi. Hawana uwezo wa kuhoji, hawajui mambo ya manunuzi. Pia bahati mbaya sana katika hiyo shughuli hawana posho yoyote, kwa hiyo wanaishia kubishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mwananchi ambaye atashinda kwenye kijiji asubuhi mpaka jioni hakuna chai wala chakula, wanagombana na Wakurugenzi, wanagombana na Walimu, wanagombana na Madaktari. Kwa hiyo miradi haikamiliki kwa sababu hakuna fedha ya usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hapa imeonesha namna ambavyo viongozi wa TAMISEMI watakwenda mikoani, mikoa itakwenda kwenye wilaya, wilaya waende kwenye kata na kata kwenye vijiji, wale wa chini wasimamizi wa kila siku hawapo, lakini kwenye bajeti hii hakuna mahali popote ambapo panaonyesha kwamba kuna posho hata kidogo kwa Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Madiwani mishahara au posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zote hizi tirioni 9.1 zitasimamiwa na madiwani katika halmashauri. Wakurugenzi wamewapa mafunzo ya Kutosha, Wakuu wa Mikoa wamefundishwa, Ma *DC* wamekaa hapa Dodoma. Tunataka kuona semina kwa madiwani wetu wakijengewa uwezo ili waweze kusimamia fedha za halmashauri ili waweze kuhoji. Wanapewa fedha shilingi 40,000 wanapoteza mwelekeo kwa sababu ya mazingira hayo. Ni vizuri fedha itengwe wawezeshwe wawe na uwezo wa kusimamia na kuhoji ili miradi iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia usimamizi Mikoani, Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana ukamsaidia Mheshimiwa Rais, kama ambavyo umeangalia pia Baraza la Mawaziri, ni vizuri tukaanzia mikoani, hivi mkoa gani unaongozwa na nani kwa tija ipi. Kuna mwingine unamkuta ni mfanyabiashara unampeleka mkoa ambao ni wakulima au ni wachimbaji, haelewi. Lakini pia badala ya kushirikisha kumekuwa na *order* na amri mbalimbali. Katika maeneo yetu, amesema Mheshimiwa Jafar; kuna Migogoro pale Bunda ya ardhi haijatatatuliwa, kuna migogoro Rorya haijatatatuliwa, kuna migogoro Serengeti hakuna utatuzi, kuna Tarime hakuna utatuzi, Mkoa mzima ni vurugu *match*. Ukienda pale kwa Kurutambe na Magwe watu wanauana migogoro ya ardhi, viongozi hawaendi pale. Nenda Mnito Msege juzi wamechinjana, nenda Mnito Kibaso wameuana; hali ya utatuzi wa migogoro lazima…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Mheshimiwa Waitara kwamba ni kweli kwa Mkoa wa Mara migogoro ya ardhi imekithiri na Bunda kuna mgogoro mkubwa pale Nyatwali watu wanalazimisha kuhama kwa fidia ndogo na wakidai wanatishwa, kwa hiyo hilo jambo lipo na ni *very serious*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara taarifa unaipokea.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa muhimu sana kutoka kwa Ester Bulaya wa Bunda. Nilikuwa nasema kwamba hii migogoro isipo tatuliwa, Mheshimiwa Waziri anamsaidia Mheshimiwa Rais kutafuta

kura za Wabunge wa CCM, Madiwani wa CCM, Wenyeviti wa CCM wa Mtaa na Madiwani wa Chama Cha Mapinduzi. Ni muhimu sana jambo hili lipewe uzito kwa sababu wale wananchi wasiposikilizwa, wakaamrishwa, wakatishwa maana yake wanaleta hasira kwetu sisi. Kwa hiyo ni muhimu sana hili jambo likafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia usimamizi wa miradi; miradi mingi kwenye halmashauri, amesema Jaffar ukienda pale Bumela fedha imeenda milioni 500 imekwisha, ujenzi umesimama waliokula fedha wapo wanakula Maisha. Ukienda pale Magoma milioni 700 imekwisha kituo cha afya hakijaisha. Nenda Genkuru nenda Nyemwaga ukaguzi huu ni mwaka wa tano, timu zimeenda tisa ya ukaguzi maalumu hakuna ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge utaratibu wa kula fedha za umma za wananchi wakawaida hao maskini ambao tunawasemea Bungeni hapa halafu tunakaa kimya si sawasawa kwa kweli hawa watu wamejitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ningetaka nitoe ombi kwenye Bunge hili ni muhimu sana. Baada ya bajeti hii Bunge lipate muda wa kujadili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana, unga mkono hoja, muda wako umeisha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyeki, si nitaunga baadaye?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa maliza, muda wako umeisha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mapendekezo ambayo nimetoa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, na naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mungu lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Singida Mjini tumepata miradi mingi na sasa tumepata hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumshukuru Mheshimiwa Rais naomba nirejee maneno ya mwana mama aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza Magreth Fursher, aliwahi kusema, naomba ninukuu; *"In politics if you want something said ask a man, if you want something done ask a woman"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi ukitaka taarifa ya maneno muulize mwanaume lakini ukitaka tafsiri ya vitendo muulize mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wameumbwa kuwa watu watulivu wenye huruma lakini wanafanya kazi yao kwa vitendo sana, salamu hizi zimwendee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma vizuri *document* ya TAMISEMI wamejielekeza wanatekeleza kwamba majukumu

yao kupitia hati idhini *presidential instrument;* na mimi naenda kwenye kipengele cha kwanza cha ugatuaji, wanasimamia sera ya ugatuaji, kwa maana ya *D by D***.** Sera ya ugatuaji ilikuwa inazungumzia tuna gatua mamla kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za mitaa hatugatui kutoka Serikali kuu kwenda Wizara ya TAMISEMI. Kwenye sera ya ugatuaji imejielekeza hasa kwenye elimu kazi kubwa ambayo wanatakiwa wafanye kwenye eneo hili la *local government* ni kusimamia shule na si elimu; suala la elimu linabaki kwenye Wizara ya Elimu; na kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 imempa mamlaka Kamishina wa Elimu kusimamia elimu. Hata hivyo, nikiangalia hii *document* sijaona kama tunafuata Sheria ya Elimu sijaona kama tunafata Sera ya Elimu ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hayo? Sasa hivi inakuja miongozo na mikataba mbalimbali, sasa hivi kuna mkataba mmoja unaitwa *KPI, Key Performance Indicator* viashiria vya ufaulu. Mkataba huu umekuwa kero kwa walimu na watumishi. Kuanzia Afisa Elimu wa Mkoa, Wilaya mpaka mwalimu wa kawaida amesainishwa huu Mkataba, na mkataba huu asipoutekeleza unasema zitachukuliwa hatua kali dhidi yake. Sasa walimu wameacha kufanya kazi sasa hivi wanandaa mpango mkakati wa kutekeleza makataba, hili jambo sio sawa. Nataka niombe Wizara ya *TAMISEMI,* kama tunataka kuboresha elimu tuanze na mwalimu, na kama tunataka kuwe na viasharia vya ufaulu, kiashiria namba moja ni mwalimu wala si kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe, tulikuwa na *BRN* hapa ika-*fail*, tumekuja na *Open Performance Review Appraisal (OPRAS)* ika-*fail,* tukaja hapa na kalenda ya ufundishaji ilikaa *within six months* ika-*fail.* Sasa leo tunakuja na *KPI.* Kwa nini tunazunguka? Na hapa nataka nirejee maneno ya mwana taaluma Sign Harris alisema; *"The whole purpose of education is to turn mirrors into windows."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri nyepesi sana, madhumuni makuu ya elimu ni kugeuza kioo kuwa dirisha. Ana maanisha nini; elimu itusaidie kubadilisha mtazamo wetu wa kibinafsi tuwaangalie na wengine ambao wako kwenye mazingira magumu katika utekelezaji wa jambo hili. Sasa walimu tunapowaandalia kwa mikataba hii badala ya kuangalia mazingira yao; walimu leo wanahitaji *comfort* tu, wanahitaji faraja wanatakiwa walipwe mishahara yao, walipwe stahiki zao; sasa tunawapelekea mikataba ya kuwachelewesha kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, na bado matamshi mengine yanaendelea, tunataka kufuta *TAHOSA* tunataka kufuta sijui umoja wa Afisa Elimu sijui wa wakuu wa Shule. Hizi *forum* kazi yake kubwa ni mkono mrefu kumfikia mwalimu, sasa Serikali inataka kuukata huo mkono? kwa kweli si sawa. Nimeanza na hili niwaombe wenzangu wa TAMISEMI na ninajua Dkt. Msonde ananisikiliza kwa makini sana jambo hili lifike mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niangalie eneo lingine la Kilimo. Leo Wizara ya Kilimo imekuja na *BBT, Building Better* Tanzania. Mradi huu unakwenda kila mkoa na sisi juzi kwenye *ALAT* Mkoa Mkuu wangu wa Mkoa alikuja na mkakati mzuri sana; kwamba walau kila kaya ambayo wanalima wawe na nusu heka ya kulima alizeti jambo. Sasa, changamoto ninayoiona hap ani kwamba, ni nani anakwenda kutekeleza jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye afisa ugani; lakini huyu afisa ugani mwajiri wake ni Mkurugenzi, Mkurugenzi jukumu lake ni kusimamia mapato. Afisa Ugani kapewa pikipiki kutoka Wizara ya Kilimo lakini huku chini ameenda kukabidhiwa *poss* ya kukusanyia mapato, ndicho kipa umbele cha Mkurugenzi. Hatuwezi kufikia malengo kwenye Wizara yetu ya Kilimo. Nataka niombe Serikali hawa maafisa ugani tuwakabidhi Wizara ya Kilimo ili waweze kurudi huku

kusimamia Kilimo chetu. Tukiendelea na mpango huu maana yake hakuna mradi wowote ambao tutautekeleza ili kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo lingine la Afya, wamezungumza vizuri sana. Nataka nizungumzie maeneo mawili moja ni *CHF* iliyoboreshwa. Watanzania hapa tunapozungumzia *CHF* iliyoboreshwa maana yake tunazungumzia ukusanyaji wa maduhuli, hatuzungumzii huduma ambayo wanaipata. *CHF* iliyoboreshwa watu hawapati huduma stahiki kwa sababu anatakiwa ahudumiwe ndani ya hospitali ya Serikali, nje hawawezi kupata huduma; na humu ndani hawawezi kufanya hivi. Wenzetu wa *NHIF* wamefanya kazi nzuri, wana miongozo, wana sheria na wanafuatilia kuanzia ndani na nje kwa maana ya Serikalini na kwenye *private sector* watu wanapata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa nini hawa *CHF* tusiwa-*link* na *NHIF* ili kutoa huduma kwa pamoja badala ya sasa kuwa na *organ* mbili tofauti? Kwamba hawa wanatoa huku hawa wanatoa huku, lakini wote wanamhudumia Mtanzania mmoja. Ni vema tukatengeneza jambo hili likawa jambo moja watu wapate huduma kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mwisho , naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali, kazi kubwa ambayo wanatakiwa wafanye Wizara ya TAMISEMI ni utawala, *monitoring and evaluation* na *coordination*. Suala la usimamizi wa miradi wawaachie Wizara za Kisekta, wawaachie Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya. Watakapotunga sera na sheria zao na miradi yao waende wakaitekeleze wenyewe huku chini. Kazi ya TAMISEMI ibaki kufanya tathmini ya utekelezaji wa hiyo. Mfano mmoja mwepesi sana, Wizara ya Utumishi na Ofisi ya Rais lakini wanafanya kazi yao vizuri, sasa na hawa ni Ofisi ya Rais wafanye kazi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulizungumza hapa mwaka 2017/2018 juu ya Idara ya Maji; na nilishauri Idara ya maji hii iende kwenye mamlaka za maji. Leo tunaona *RUWASA* wanavyofanya vizuri. Miradi inatekelezwa vizuri mno kwa sababu wanajitegemea; na huku pia tufanye utaratibu huo watu waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaombe wenzangu wa TAMISEMI, Jimbo la Singida Mjini tunayo Hospitali ya Wilaya, hatuna watumishi na hatuna vifaa tiba, naomba viletwe. Lakini kata moja ambayo imebaki ni kata ya Kisaki, kata ambayo mimi na wananchi wangu tumefanya kazi kubwa ya ujenzi sasa tunahitaji fedha kwa ajili ya kukamilisha na tunahitaji watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima ahsante sana, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo atafatiwa Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Doctor Ritta Enespher Kabati ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya TAMISEMI, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, Naibu Mawaziri Waziri wawili pamoja na wetendaji katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi alizozileta katika jimbo la Mbagala. Elimu msingi tuna bilioni nne, tumejenga madarasa 142 na shule mpya za msingi nne. Elimu Sekondari tumejenga Shule mpya tatu, tumejenga madarasa 165 na jumla ya fedha zilizo letwa katika elimu sekondari ni bilioni 5.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya tumeletewa bilioni mbili kwa ajili ya kujenga hospitali ya Wilaya pale ya Zakem ambayo nimeipigia kelele muda mrefu sana. Tumepewa vituo vitatu vya afya na zahanati mbalimbali zimejengwa katika Jimbo langu la Mbagala. Kwa dhati yangu ya moyo nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na fedha alizozileta katika jimbo la Mbagala. Niwashukuru pia Mawaziri ambao wamesimamia na kutekeleza pamoja na viongozi wangu wa ngazi ya Wilaya, Mkurugenzi pamoja na Mkuu Wa Wilaya na Madiwani kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya barabara tumeletewa bilioni 24, imetekeleza barabara mbalimbali katika jimbo langu la Mbagala. Ni jimbo ambalo lilikuwa halina miundombinu kabisa ya barabara; tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo mchango wangu nataka nijikite katika suala zima la barabara. Serikali inatuletea mradi wa uboreshaji wa barabara katika jiji la Dar es Salaam, awamu ile ya pili na ya tatu. Mheshimiwa Waziri ametuahidi mpaka mwezi wa nane mradi huo utaanza, lakini sisi watu wa pwani tunasema dalili ya mvua ni mawingu. Tunatarajia mvua itanyesha kwa maana ya ujenzi uanze mwezi wa nane lakini mawingu hatuyaoni. Barabara hizi sehemu zote zinapokwenda kupita zinahitaji zilipiwe fidia. Hatujaona mpango wowote kwenye bajate iliyotengwa wala kutoka Serikali Kuu, kwa maana ya Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kulipia fidia katika maeneo yatakayo pisha ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tumuombe Mheshimiwa Waziri akija hapa atupe ufafanuzi, kama fidia hizi zitalipwa na halmashauri basi ni vyema halmashauri zikaambiwa mapema ili na tuweze kujipanga ni namna gani ambavyo tutalipa fidia; kuliko fedha zimekuja mradi unatakiwa uanze lakini fedha za kulipa fidia zinakuwa vikwazo vya utekelezaji wa miradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, miundombinu ya barabara katika Mkoa mzima wa Dar es Salaam ni tatizo; na hasa katika jimbo langu la Mbagala. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais ya kutuletea fedha za kujenga barabara lakini ni lazima sasa tuone Wizara kupitia *TARURA* wanatutengea fedha za kutosha kujengea barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza msongamano katika Jimbo la Mbagala ni lazima barabara za kuunganisha kati ya Wilaya na Wilaya zijengwe; ni lazima barabara za kuunganisha kati ya jimbo na jimbo zijengwe; ni lazima barabara za kuunganisha kati ya kata na kata zijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaotokea kusini wanajua pale kuanzia Kokoto mpaka Kongowe kunakua na foleni, ni kilometa mbili, lakini kama Madaraja yanayounganisha Mkuranga na Mbagala yakijengwa msongamano ule unaenda kuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kuna lile Daraja la Kidete ambalo liko katika Mtaa wa Bamia litaunganisha eneo la Kidete-Mkuranga pamoja na eneo la Mbagala. Kuna lile Daraja la Mbanga Kwalu ambalo liko katika mtaa wa Bamia, likijengwa linaenda kuunganisha Mbanga Kwalu, Mkuranga pamoja na Jimbo la Mbagala. Pia tunalo lile daraja la Churwi ambalo liko Kata ya Mianzini na Kata ya Chamanzi likijengwa linaenda kuunganisha jimbo la Mbagala pamoja na Mkuranga. Kwa kufanya hivi tunaenda kuondoa msongamano wa barabara ile ya Kilwa *road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunataka tujenge barababara ni lazima tuzingatie barabara zipi zinaenda kuondoa msongamano wa foleni katika barabara zetu. Tunazo barabara ambazo zinaunganisha kata kwa kata. Kwa mfano barabara ya Habari Zako hii inaunganisha kata ya Chamazi pamoja na kata ya Mianzini. Tunazo Barabara za

Mabwawa ya Samaki, Kona Tope, Maandazi *Road*, *Stanley*, kwa Ndunguru na Kwamakuka. Majina haya yanatokana na asili ya Kizaramo ambao ndio wanaishi sana maeneo yale; na ndiyo maana wananchi wa Mbagala miaka hii mitano wamenikabidhi mimi mtoto wao kwa kuwa wanajua nazifahamu kwa majina barabara hizi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, ahsante sana, muda wako umeisha.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,nakushukuru sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, na mimi nitachangia kwa uchache. Mosi nikitambua maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika mahitimisho yake Tarehe 13, Mwezi wanne mwaka 2023, kuhusiana na asilimia kumi ya mikopo ya Vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika utambuzi huo nilidhani Waziri wakati anajibu atusaidie mambo kadhaa. Kwa sababu siku zote huwa nasema hii ni Wizara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ninyi hapo mmepewa dhamana ya kumsaidia. Katika mazingira ya kawaida, Wizara ambayo ni ya Rais inategemewa iwe ni mfano kwa Wizara nyingine kuiga. Sasa, tumeambiwa kwenye taarifa mbalimbali za Mkaguzi Mkuu; ya mwaka jana, ambapo mwaka jana pamoja na mambo mengine ilifanya majumuisho ya fedha ambazo hazijarejeshwa katika kipindi

cha miaka mitano ya mfuko wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo ukijumlisha za mwaka jana ambayo ilikuwa ni bilioni 47.1 na za miaka ya nyuma yake minne inaenda kama bilioni 100 *plus*, ukijumlisha na za mwaka huu ambazo ni bilioni 88 maana yake unaenda *188 billion plus.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu ni moja, nimesoma maelekezo yako mahsusi ambayo umepeleka kwenye mamlaka za Mikoa na Halmashauri, maelekezo 14, hatuoni popote ulipotoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa, kwa Wakurugenzi kuhakikisha kwamba hizi fedha ambazo zimepotea huko chini inasemekana zimepotea huko chini, ziweze kupatikana zote. Sasa unapotoa maelekezo 14 lakini elekezo la upotevu wa *billions of money* hamtoi maelekezo mahsusi, unatupa jibu gani? Kwamba inawezekana kabisa hili jambo hamlichukulii *serious,* inawezakana kabisa hiyo miezi mitatu ikiisha ukaja mfumo mwingine mambo yatakuwa yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitaka Serikali kabisa na nikutake Waziri, ukiwa unajibu hapa utoe maelekezo ya fedha hizi zilizopotea huko chini kwa wajanja, zikusanywe. Ulizungumza hapa Bungeni ukiwa unajibu swali lakini kujibu swali hapa Bungeni ni jambo lingine, kutoa maelekezo mahsusi kuhusu suala la kibajeti ni jambo lingine, hamjaliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapopitia Kanuni za utoaji wa asilimia 10, unagundua kwamba hizi fedha hazijapotea, hizi fedha zimepotezwa. Sasa kama fedha zimepotezwa kuna *element* ya jinai hapa, lazima watu wawajibike kama wamehujumu uchumi, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu mnasimama hapa mnasema Rais wetu anazunguka mataifa kwenda kuomba fedha, hivi hamuoni aibu Rais anahangaika, fedha zinakuja halafu wajanja huko chini wanapiga? Kwa sababu ni kweli

hizi ni mapato ya ndani ya Halmashauri *yes,* lakini ni sehemu ya mapato ya ndani ya Halmashauri ambayo kutokana na Halmashauri zetu kutokuwa na uwezo wa kimapato tunategemea mikopo ya nje kuendesha mambo mengine ya kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kanuni hii nitarejea tu kwa mfano, Kanuni ya Saba inawataja Watendaji wa Kijiji, Watendaji wa Mitaa na Watendaji wa Kata kama watu wa kutawakilisha vikundi, kuanzia Kijiji. Kanuni ya 13 Afisa Maendeleo ya Jamii anatajwa yeye ni usajili na uratibu, Kanuni ya 14 kuna Kamati ya Huduma ya Mikopo kuna Mkurugenzi wa Halmashauri na timu yake yeye anachambua na anajadili na kufuatilia vikundi. Kanuni ya 17 inataja Kamati ya Kudumu ya Fedha na Mipango ya Halmashauri zetu, wao wanaidhinisha mikopo, wako Madiwani, tuko Wabunge huku ndani, Kanuni ya 18 ni Mkutano wa Halmashauri kupitisha kile ambacho Kamati imepitisha. Kanuni ya 20 Sekretatarieti ya Mkoa wana jukumu la ufuatiliaji, Kanuni ya 21 Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Bunge lituambie hapa eti kuna vikundi hewa huko chini? Nchi hii ilivyokuwa na cheo mpaka huko chini? Nchi hii mtu ukifanya hata uhalifu wa kawaida unavyoweza kutafutwa, kwa nini hapa kuna kitendawili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninapendekeza, *CAG* afanye kitu kinachoitwa *Forensic Auditing* yaani ukaguzi wa kiuchunguzi ili tuangalie kama kuna udanganyifu, kuna wizi ama kuna rushwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu hatuwezi kuviacha viende hivi. Mimi niseme wazi kabisa ili mradi Kiongozi wetu wa Muhimili Mheshimiwa Spika ametuamini kwenye Kamati ya *LAAC* tutafanya kazi yetu kwa uaminifu na kwa uadilifu mkubwa kulisaidia Taifa hili. Haiwezekani unaenda kuomba

omba huko halafu unakuja Bilioni zaidi ya 100 zinadondoka chini halafu na wewe unacheka cheka tu! *No, no, no!* Mambo hayaendi hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima muda wako umeisha. Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi muda ukiruhusu tutaendelea na Mheshimiwa Dkt. Pauline Nahato.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba nami nitoe pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu ambae amefanya kazi nzuri katika nchi hii, amekuwa Rais wa mfano, amekuwa suluhu ya matatizo katika nchi yetu, Watanzania kwa kweli kazi yetu ni kumuombea tu dua Mwenyezi Mungu aendelee kumuweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Halima Dendegu Mkuu wa Mkoa wa Iringa anafanya kazi nzuri sana katika Mkoa wetu tunampenda sana. Pia naomba nimpongeze Waziri Mwenye dhamana Angela Kairuki, Rais hakufanya kosa kumchagua nafasi aliyokupa chapa kazi nasi tuko nyuma yako Mwenyezi Mungu atakujalia, pia Naibu Mawaziri ambao yuko nao tunajua pia ni wachapakazi wazuri sana, endeleeni kuisaidia TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze *TARURA* kwa kazi nzuri sana, naomba kwa kweli waongezewe bajeti kwa sababu kwa kipindi kifupi tu wameonesha kazi nzuri anayoifanya. Niunge Mkono wale waliosema Seif apewe tuzo, chifu wetu apewe tuzo naunga mkono na apewe kweli kwa sababu kwa kazi nzuri ambayo barabara nyingi sana za

vijijini zimefunguka na hata vifo vya akina Mama na Watoto vimepungua, Mungu ambariki sana. Pia nimpongeze *TARURA* Mkoa wetu wa Iringa yuko vizuri anafanya kazi vizuri, Mwenyezi Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kumpongeza Rais wetu kwa pesa za UVIKO na pesa za tozo ambazo alizitoa katika Mkoa wetu wa Iringa zimeongeza bajeti, karibu asilimia 200 ya bajeti kutoka Bilioni 6.3 hadi Bilioni 16.7. Ongezeko hilo limefanya barabara nyingi kuweza kujengeka za lami hata za changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, bado zipo changamoto katika Mkoa wetu kutoka na jiografia yetu ina milima mimgi ambayo barabara zake nyingi zinahitaji madaraja mengi na wakati wa mvua huu barabara nyingi sana hazipitiki wakati wa masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya barabara ambazo zina changamoto kubwa sana naomba tu nizitaje kwa uchache. Katika Wilaya ya Iringa kuna barabara ile ya Izazi – Mboliboli kilomita 25, kuna Mtwivira – Ikongo kilomita 1.5, Mufindi kuna barabara ile ya Tambalang'ombe – Kwa Mtenga kilomita 41, Luganga – Itimbo – Isupilo kilomita 11. Wilaya ya Kilolo kuna barabara ya Muhanga – Mugeta kilomita 18, Ilula – Uhambingeto – Ulambilelo kilomita 17, Mtandika – Nyanzo kilomita 40, Itimbo – Kitelewasi kilomita 26, Ilula – Ibumu kilomita 20. Pia kuna barabara kutoka Kitowo kwenda mpaka Masisiwe hii barabara mpaka sasa hivi nilipita juzi tu ina changamoto nyingi sana. Kwa hiyo, ninaomba *TARURA* iziangalie hizi barabara hizi barabara ili Mkoa wetu wa Iringa uweze kufunguka kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao upungufu mkubwa sana wa watumishi wa kada zote katika Mkoa wetu wa Iringa. Nikichukulia tu kada ya afya watumishi wanaotakiwa ni 4,647 na waliopo 2,416 upungufu kama 2,111 kama asilimia

48. Tunaomba Wizara sasa katika hizi ajira mpya iangalie kwa jicho la kipekee Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tupongeze ujenzi na ukarabati wa shule zote nchini lakini sasa waangalie pia Walimu wetu waboreshewe nyumba zao zijengwe na hasa huko Vijijini na zikarabatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wenzetu pia wanachangamoto nyingi sana, Mimi ni mjumbe wa *ALAT*. Zipo changamoto ambazo tuliainisha tulitegemea sana zingefanyiwa kazi, wanafanya kazi kubwa kwa kweli changamoto ni nyingi waangaliwe na waboreshewe maslahi yao ili waweze kufanya kazi vizuri kwa sababu miradi yote ipo chini yao. Hata Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa pia waboreshewe posho zao kwa sababu wanasimamia miradi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitambue wadau wa maendeleo wanaochangia katika Mikoa yetu lakini wanasaidia pia katika bajeti yetu. Katika Mkoa wetu yuko mdau Mkubwa *MNEC* wetu mpendwa Ndugu Salim Asas, ameweza kutoa kwanza Shilngi Milioni 100 kwenye majengo ya Machinga, amechangia ujenzi wa jengo la Ustawi wa Jamii ambalo ni la mfano na Waziri Mkuu alilifungua. Pia amejenga jengo la damu salama, amejenga jengo Watoto Wachanga, ujenzi wa *ICU,* jengo la viungo bandia, jengo la wagonjwa maalum (*VIP)* lakini huwa anatoa maziwa kwenye shule zote. Mdau huyu ni wa kuigwa nchi nzima na siku nyingine aletwe hapo tumpigie makofi ili wengine waweze kumuiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya Wazabuni, wanapata shida sana, naomba kabisa Wazabuni hawa wamekopa benki, wanalipa riba, *TRA* wanatozwa zile *penalty,* usumbufu mkubwa sana wanakwenda huko hazina,

naomba waangaliwe kwa kweli na tuambiwe kwamba wazabuni wako wangapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu asilimia 10. Kuna watu hawakopesheki, kuna wamama ambao wamezaa watoto wenye ulemavu, hawa watu hatujajua wamewekwa kwenye kundi gani? Wanabeba watoto kuanzia asubuhi mpaka jioni, wanatafuta pesa kwa ajili ya kuwasaidia hawa Watoto, bado Serikali haijajua kwamba je, hawa watu wanakopa kule kwa watu wenye ulemavu au kwa hawa wamama wa kawida? Kwa sababu, hebu tuangalie mimi nakuomba Mheshimiwa Angela Kairuki wewe ni Mama mwenzetu naomba utakapokuja utujibu hawa wamama wapi wakope? Wako kwenye kundi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hautatoa jibu nitashika shilingi nitaomba Wabunge wote watuunge mkono ili hawa wamama wajue wanakopesheka katika fungu gani, kwa sababu wote humu ndani ni walemavu watarjiwa, lakini hawa wanawake wengine wamewakimbia na waume kwa sababu wamezaa watoto wenye ulemavu. Jamani hili jambo ninalisema kwa uchungu mkubwa ninaomba Bunge hili kwa kweli hebu liangalie na tutoke na suluhu. Tumeuliza sana maswali lakini hatupatiwi majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana na Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Amina ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ya TAMISEMI. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya katika nchi yetu, amejipambanua kwa jinsi ambavyo analeta

pesa nyingi katika Majimbo yetu. Ninaapongeze wasaidizi wake Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wanamsaidia na jinsi ambavyo wanakimbia kimbia huko kwenye Majimbo yetu kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Ilani unakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Watendaji wa Wizara ya TAMISEMI nikianza na Mheshimiwa Waziri Angela Kairuki na Wasaidizi wake wote na timu yake nzima wanafanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba kule Majimbani tunaweza kusimama kwa kujiamini kwa sababu miradi mingi inatekelezeka katika Majimbo yetu. Niwapongeze watumishi wetu wa Mkoa wa Kigoma wakiongoza na *CP*. Thobias Andengenye, hususani wale wa Halmashauri ya Kibondo kwa jinsi ambavyo wanapambana kutekeleza hii miradi inayokuja na kipekee kwa jinsi ambavyo wamekamilisha kwa wakati miradi iliyokuja ya madarasa na vituo vya afya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Muhambwe naomba nifikishe pongezi na shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa pesa nyingi alizoleta. Jimbo letu limepokea Bilioni 18 zikiwa ni pesa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hizi zimewezesha kutekeleza miradi mbalimbali katika Jimbo letu la Muhambwe. Tumetekeleza miradi mingi kwenye elimu afya na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pesa hizi bado Jimbo la Muhambwe lina changamoto. Nitaanza na changamoto kubwa ya ajira hasa ajira ya Walimu na Watumishi wa Afya. Mkoa wetu wa Kigoma una watumishi 1,955 wa afya ikiwa mahitaji yetu Mkoa wa Kigoma wote tunahitaji watumishi 7,699 kwa hiyo tuna uhaba wa asilimia 74 kwa kiwango cha juu cha uhitaji, lakini kwa kiwango cha chini cha uhitaji tuna uhaba wa asilimia 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Muhambwe lina mahitaji ya juu ya watumishi 977 lakini tuna watumishi 311

tu ikiwa ni upungufu kwa asilimia 76, Jimbo hili la Muhambwe tunazalisha wakinamama 50 mpaka 55 kwa siku. Kwa hiyo, kwa mwaka mzima tuna vizazi hai 17,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huu mzigo tuliokuwa nao jimbo la Muhambwe basi na Mkoa mzima wa Kigoma katika ajira hizi tunazotegemea kupata naomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma tukiwa ni Mkoa wa pembezoni, watumishi wengi wanakimbia, tupewe watumishi wa kutosha wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa walimu. Katika Jimbo la Muhambwe tuna shule ambazo zina walimu wanne kama ile ya Nyaruhaza na Ntoyoyo tuna walimu wanne tu shule ya msingi. Vilevile nimepata taarifa kwamba kwenye mgao huu wa walimu tumepata mgao wa Walimu 15 hawatoshi kabisa. Nimuombe Waziri, Jimbo la Muhambwe mtusaidie tupate walimu 60 ili angalau hizi shule ambazo zina *digit* moja moja basi angalau kutoka wanne wawe nane. Tuna shule zina walimu sita nyingi, naomba mtusaidie Jimbo la Muhambwe tupate walimu 60 wa msingi ili tuweze kupambana na uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile shule za sekondari tuna uhaba mkubwa sana, kipekee nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu kwa mgao wa madarasa tuliyopata Jimbo la Muhambwe tumefanikiwa kusajili shule tatu za sekondari mwaka 2022 na mwaka 2023 tumesajili shule nne, hivyo tuna uhaba mkubwa wa walimu. Niiombe Serikali tupate mgao mkubwa kwa ajili ya walimu wa sekondari angalau walimu 70 ili tuweze kukabiliana na uhaba huu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Shule 24 tulizonazo za sekondari tuna sekondari Tatu tu za Kidato cha Tano na cha Sita. Kati ya hizo, shule za sekondari moja ilikuwa ni Kambi ya Wakimbizi ya Mkugwa, ninamuomba Mheshimiwa Waziri siku

moja aje tukaitembelee hii shule inatia aibu haina madarasa. Ninakuomba shule hii ipatiwe madarasa pia ninaomba tupatiwe na mabweni mawili ili tuongeze shule mbili za Kidato cha Tano ikiwa ni ile shule ya Busagara na Kumgogo ili angalau tuwe na Shule za Kidato chaTano Tano katika Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa *TARURA* nami niwapongeze *TARURA* wanafanya kazi nzuri na *Engineer* Victor kwa kweli anastahili sifa zote tulizompa. Sisi tumepata utekelezaji wa madaraja ya mawe, tumepata madaraja ya mawe 19 katika Jimbo la Muhambwe. Kwa hiyo, baada ya kupata haya madaraja tunazo barabara ambazo zinahitajika kuunganishwa, hizi barabara zikiunganishwa basi wananchi wetu wataweza kupita. Tunahitaji kuunganisha Kitahara na Bunyambo, tunahitaji kuunganisha Luhunga na Bunyambo, tunahitaji kuunganisha Nengo na Mbizi, tunahitaji kuunganisha Nyakasanda na Mukarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Milioni 591 tumeomba, ninawaomba *TARURA,* nimuomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kupata hizo pesa ili hizi Kata na hizi barabara ziweze kuunganishwa kwa sababu tunayo tayari madaraja ya mawe ambayo yamejengwa na Shirika la *Enabel,* kwa hiyo, tunaomba tuunganishiwe hizi barabara ili wananchi waweze kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo bado pia tunauhitaji wa madaraja ya mawe ambayo pia tumeleta, tunahitaji madaraja ya mawe 20 ambayo tunategemea kujenga kule Kagoti na Nyaruranga ili kuwasaidia wananchi wanokwenda mashambani lakini na watoto wa shule wanaokwenda mashuleni wasipite kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali tuchukue teknolojia hii ya bei nafuu ya kutengeneza madaraja ya mawe ili tuweze kuwasaidia wananchi wa Muhambwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Muhambwe nalo lina maboma ambayo yanahitaji kumaliziwa ikiwemo lile boma la kituo cha afya cha Kizazi lakini madarasa ya karukambati, madarasa ya Kigina, niombe TAMISEMI waje na mpango mahsusi wa kumalizia haya maboma kwa sababu hizi ni nguvu za wananchi na wananchi wanapenda kuona utekelezaji ukifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuomba utekelezaji wa ahadi za viongozi. Niombe ahadi ya kituo cha Afya cha Mulungo na ahadi ya Milioni 200 kituo cha afya cha Nyaruyoba iweze kutekelezeka. Wananchi wanasubiri kuona utekeleaji wa ahadi hizi kwa sababu ni ahadi za viongozi wakubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Florence.

Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa michango yenu mchana huu wa leo. Nina tangazo moja la wageni wa Mheshimiwa Wanu Hafidh ambao ni Bi. Hajrat Zahra *Founder and Chairperson of Tawani Foundation*. Karibu sana. Yupo na Sheikh Hashimu Kamugunda ambae ni *Director* wa *Tawani Foundation*. Karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na michango jioni na tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Pauline Daniel Nahato, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Minza Simon Mjika na orodha itaendelea.

Baada ya kusema haya nasisitisha shughuli za Bunge hadi saa Kumi kamili alasiri.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

**17 APRILI, 2023**

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel na baadaye Mheshimiwa Hussein Nassor Amar atafuatia.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami nichangie katika Wizara hii ya *TAMISEMI*. Awali ya yote, napenda kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake nyingi sana na kubwa alizozifanya katika kuweka miundombinu mingi ndani ya miaka miwili katika sekta mbalimbali na hususan katika sekta ya afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuwapongeza Waziri pamoja na Manaibu Waziri wa *TAMISEMI* kwa kazi nzuri wanazofanya, wamekuwa wasikivu, wamekuwa wakipokea simu kwa wakati, wamekuwa wakitoa ushauri na ushirikiano uliotukuka. Nawapongeza sana. Naomba nielekeze mchango wangu katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza ni sehemu ya afya pamoja na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Rais wetu kwa miundombinu mizuri katika sekta ya afya hususani

majengo ya zahanati, hospitali na vituo vyote vya afya katika nchi yetu. Hiyo inaonesha dhahiri kwamba nia ya Rais kuwafanya Watanzania kuwa na afya, ni kubwa sana. Ni dhahiri kabisa kwamba wananchi wanapokuwa na afya, basi wanaweza kufanya shughuli zao za kuleta maendeleo. Kwa hilo nampongeza Rais sana kwa dhati pamoja na Mawaziri wanaohusika kwa kuliangalia hilo na kwa kulishughulikia kwa uangalifu na umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila mafanikio kuna changamoto ambazo ni vizuri sisi Wabunge tukatoa ushauri ili tuweze kufikia mafanikio makubwa zaidi ya hapa ambapo tumefikia. Ni imani yangu kabisa kwamba Mawaziri watayachukua na yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la ajira katika masuala ya afya. Ajira ni changamoto, hospitali zipo na wagonjwa wapo kila siku, lakini wafanyakazi ni wachache. Tukiangalia katika hospitali zetu nyingi kutokea zahanati mpaka hospitali kubwa, Madaktari hawatoshi, ni wachache; Manesi ni wachache; na Wataalamu wa Vifaa vinavyotumika hospitalini ni wachache au hawapo, wale ambao wanaweza kutunza vifaa na wale ambao wanaweza kufanya matengenezo pale ambapo vifaa vinaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu, nilikuwa naomba tu, katika suala hili la ajira, kwa kweli kada ya hawa watu ambao ni Madaktari, Manesi, Wataalam, Wafamasia na wengine wa Maabara kwa kweli waajiriwe kwa wingi ili wananchi wanapoenda hospitalini, hii isiwe ni changamoto kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba pia kuishauri Wizara kuangalia vifaa mbalimbali vinavyotumika katika hospitali. Kuna vifaa kwa mfano *hematology machines,* hizi ni chache, hebu Wizara iweze kuziangalia na kuziongeza. Kuna

*chemistry analyzers,* kuna mashine za *theater* kama *Anesthesia Machines, ventilators,* na mashine nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi mashine wananchi wanazitumia, na wanapozikosa katika maeneo yao na wanapopewa *referrals* kwenda katika hospitali kubwa, inakuwa ni changamoto kwa sababu wananchi wengi hata uwezo wa kupata nauli hakuna. Kwa hiyo, naomba *TAMISEMI* iweze pia kuzingatia hivyo vifaa viweze kupatikana katika hizo hospitali na zahanati ambazo zimejengwa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda pia kulishauri katika Wizara ya Afya ni eneo la mafunzo kazini. Manesi wengi wana umri mkubwa, wamesoma zamani, kwa hiyo, wakipata na nafasi ya kwenda kuhudhuria mafunzo yatawasaidia kwa sababu teknolojia inabadilika mara kwa mara, hata vitu mbalimbali vinabadilika. Kwa hiyo, naishauri Wizara iweze kutenga pesa ya watumishi kwenda kupata *refresher courses* ili waweze kuwa *updated* pamoja na mambo yanavyokwenda na magonjwa yanayoibuka mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda, naomba nigusie kwa haraka sana katika suala la elimu. Katika suala la Elimu ni dhahiri kabisa ya kwamba hata ukiwaweka wanafunzi katika hoteli ya *five stars,* kama wafanyakazi hawapo, kama walimu hawapo, watakaa, watakula na watapata kila kitu, lakini mwisho wa siku kama hawajafundishwa, ukiwa *compare* na wale ambao wamejifunza chini ya miti lakini walimu wapo, ni ukweli kabisa kwamba wale wa chini ya miti watafanya vizuri kuliko wale wanaokaa katika *five stars hotel. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Namshukuru sana Rais kwa kujenga madarasa, kwa kujenga miundombinu, lakini waongezeke ili kuwe na *balance* ya

wanafunzi wetu kufurahia mazingira na kufurahia walimu ili waweze kufaulu kwa kiwango kinachohitajika katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pia niweze kushauri juu ya miundombinu ya walemavu katika shule zetu. Walemavu wanapata shida hasa katika miundombinu kama vile choo. Kwa hiyo, naomba pale tunapoendelea kufanya kazi yetu vizuri, tuzingatie vyoo hasa kwa wale ambao wana ulemavu wa viungo. Vile vyoo kwa kweli usafi wake kuu-*maintain* ni ngumu. Kwa hiyo, *at least* wawe na vyoo vyao *special* ili nao waweze ku-*enjoy* fursa kama wanafunzi wengine ambao hawana ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kusema jambo moja kuhusu uzio. Naomba Serikali iweze kufikiria kujenga uzio katika shule zetu ili wanafunzi wetu waepuke vishawishi katika shule hasa wanapokuwa shuleni. Ule uzio utaweza kusaidia wasiweze kupata vishawishi nje ya maeneo ya shule. Wanapokuwa shuleni waweze kuzingatia kusoma tu na uzio japo hautamaliza, lakini utawazuia kutokutoka nje na kukutana na watu ambao nia zao siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Nami naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa Minza Simon Mjika, ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Ofisi ya Rais, *TAMISEMI*. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na afya njema kwa siku ya leo na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo sekta ya afya na elimu. Sisi kama Wilaya ya Nyang'wale kwa fedha hizo ambazo mama ameweza kuzitoa kwa nchi nzima; na sisi kama Nyang'wale kwa mwaka 2022/2023 ametupatia zaidi ya shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo upande wa afya na elimu. Hongera sana mama, kwa kweli unafanya kazi kubwa, hongera sana, sisi tuko nyuma yako, kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya. Naipongeza Serikali kwa kuendelea kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nyang'wale. Pia namwomba Mheshimiwa Waziri atenge fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo la Mkurugenzi wa Wilaya ya Nyang'wale ambaye hivi sasa anatumia jengo la Hospitali ya Wilaya na kumfanya *DMO* asiingie kwenye lile jengo. Kwa hiyo, tenga fedha ili ulikamilishe jengo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nyang'wale aweze kuhama aende kwenye jengo lake, na kumpisha *DMO* naye aingie kwenye jengo lake la utawala ili aweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo kwenye sekta ya afya hususan kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nyang'wale, Vituo vya Afya na Zahanati, kwa kweli kuna uhaba mkubwa wa watumishi. Uhitaji wa watumishi ambao wanahitajika katika Wilaya ya Nyang'wale ni watumishi 841, lakini waliopo hivi sasa ni 193, sawasawa na asilimia 22. Kwa hiyo upungufu ukiuangalia hapo, ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa mwaka huu wa fedha basi tupatiwe angalau hata watumishi 100 ili tuweze kupunguza *gap* lililopo pale. Kwa sababu ukiangalia 842 na 193 ni upungufu mkubwa sana. Waliopo kwa kweli wamechoka, lakini nawapongeza sana wanajituma na wanafanya kazi kwa moyo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zipo. Kuna wananchi walijitolea kujenga maboma ya Zahanati na maboma ya Vituo vya Afya, wametoa nguvu zao. Namwomba Mheshimiwa Waziri kupitia bajeti hii atenge fedha ili kwenda kuziunga mkono juhudi za wananchi wangu waliojitolea kwa ajili ya kujenga maboma ya zahanati pamoja na Vituo vya Afya ili kuwatia moyo, ili kwa mara nyingine hata ukiwaambia njooni tuungane pamoja watakuwa wako tayari kuliko hivi sasa wanatoa nguvu zao lakini Serikali haiwaungi mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya elimu, naipongeza sana Serikali. Kwa kweli Mama amefanya kazi kubwa kwa kipindi hiki kifupi, tumeweza kujenga madarasa mengi upande wa sekondari, madarasa mengi shule za msingi na pia kwa shule shikizi. Tumeweza kufungua sekondari tatu mwaka huu wa fedha. Kwa kweli tunampongeza Mama, anafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palipo na mafanikio hapakosi kuwa na changamoto. Namwomba Mheshimiwa Waziri wetu aweze kutenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za Walimu kwa sababu kuna upungufu mkubwa, lakini pia atenge fedha kwa ajili ya kumalizia maboma ya vyumba vya madarasa ili kuwaunga mkono wananchi ambao walijitolea katika ujenzi huo wa maboma ya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna upungufu mkubwa upande wa sekta ya elimu. Tuna upungufu wa walimu takribani asilimia 70 katika Wilaya ya Nyang'hwale. Ukweli Mheshimiwa Waziri jaribu kuangalia sana upungufu huo na hususan kwenye elimu ya sayansi na hisabati walimu ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri, naomba unisikilize vizuri. Ushauri huu jaribuni kuufanyia kazi. Naomba myafanyie uchunguzi magenge ya vyakula

vinavyouzwa nje ya mageti ya shule zetu za sekondari na msingi. Vyakula vile na vinywaji siyo salama sana kwa watoto wetu. Pia ukiangalia maeneo haya, tayari kuna viashiria; mimi ni mmoja wa waathirika katika watoto wangu ama katika familia yangu, ameathirika na vinywaji hivi vya hapo shuleni, sasa hivi ni teja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, angalieni sana usalama wa chakula na vinywaji vya watoto kwenye magenge yaliyoko nje ya mashule. Jaribuni kufanya utafiti kwa kuwa pia ni vyanzo vya kuanza kufundisha watoto wetu mambo machafu kutokana na hizo Shilingi elfu moja moja na mia tano tano ambazo tunawa. Ukifika muda wa kwenda kula, kanunue pipi, kanunue mandazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakumbuka, Mzee Mkuchika anakumbuka, sisi tuliokuwepo zamani kidogo, tulikuwa tunafungiwa viazi, mihogo au mandazi, tunaondoka navyo nyumbani. Leo hii sisi tunaona watoto wetu ni bora umpe shilingi 1,000 aende akale chakula pale shuleni na chakula hicho kina madhara makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jaribuni kuchukua hata watoto kumi, mkawapime afya zao, utakuta watoto wanane wana matatizo kutokana na vyakula hivyo. Kama siyo *Typhoid* na maradhi mengine kutokana na hivyo vyakula. Hatujui vinatengenezwa kwa mfumo gani na nia zao ni zipi kutokana na hali iliyopo. Mheshimiwa Waziri chukua ushauri wangu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *TARURA,* imefanya kazi vizuri sana katika Wilaya yangu ya Nyang’hwale. Mwaka huu wa fedha tunaoenda kuumalizia, 2022/2023 tumeweza kupokea zaidi ya shilingi bilioni 2.2. Pamoja na hayo, bado kuna matatizo kwenye Kata zetu. Naishauri Serikali iiongezee fedha *TARURA* ili aweze kufanya kazi vizuri kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna daraja ambalo linaunganisha kati ya Kata ya Kharumwa na Nyijundu, ni kilomita saba tu kati ya hizo Kata, lakini daraja hilo tumeshindwa kulijenga kwa sababu linahitaji fedha zaidi ya shilingi milioni 500. Nakuomba zitengwe Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kulijenga hilo daraja, barabara ile ifunguke. Kwa sababu barabara hiyo sasa hivi haitumiki, utakapotoka Kharumwa kwenda Nyijundu ni kilometa 30 kwa njia ya mzunguko, lakini ukitoka Kharumwa kwenda Nyijundu kwa njia ya mkato ni kilomita saba. Kwa hiyo, itasaidia sana kuinua uchumi wa wa Nyang'hwale, lakini kwa sababu tumejenga Hospitali ya Wilaya, ni karibu sana kuleta wagonjwa kwa njia ya mkato, kutoa wagonjwa wilayani na kupeleka Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili kwa ajili ya kutuongezea fedha tuweze kujenga hilo daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amar. Tunaendelea na Mheshimiwa Minza Simon Mjika na Mheshimiwa Agnes Hokororo ajiandae.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo makuu ambayo ameendelea kutupatia. Tuna afya njema na ndiyo maana tuko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu ya Tanzania. Wala haina sababu ya kueleza, wote tuanaona mambo makuu ambayo anaendelea kuyafanya. Vilevile namshukuru dada yangu, Waziri wa *TAMISEMI* kwa ajili

ya kazi nzuri ambazo anaendelea kufanya pamoja na Manaibu Waziri. Endeleeni kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwa upande wa *TARURA; TARURA* ni watu ambao wanafanya kazi vizuri sana. Barabara zetu zimefunguka, ziko vizuri, japokuwa ni za changarawe, lakini tunaenda vizuri utadhani ni barabara ya lami, tunashukuru kwa hilo. Tunapenda kumshukuru sana kiongozi wetu wa mkoa, Meneja wa *TANROADS* Gaston Gasana anafanya kazi nzuri sana, ikiwa ni pamoja na Mkuu wetu wa Mkoa anafanya kazi nzuri sana, anasimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya, namshukuru Rais wetu ametupatia hospitali kubwa mbili tena za wilaya; Wilaya ya Itilima na Wilaya ya Busega. Meatu, Maswa pamoja na Bariadi tuna hospitali hizo za muda mrefu na zina vifaa, tunashukuru sana kwa kazi nzuri ya Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hizi mbili ambazo zimejengwa bado ni mpya na bado ni changa zinahitaji wafanyakazi wa kutosha, tunaomba tupate wafanyakazi katika hospitali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vifaa vya kufanyia kazi katika hizo hospitali, tunaomba vifaa vipatikane kwa ajili ya kazi hiyo. Vinginevyo ninapenda tu nimshukuru sana Mama kwa kazi nzuri ambazo anaendelea kufanya. Wafanyakazi ni wachache sana katika hospitali, kwa mfano Mkoa wa Simiyu una asilimia 33 ya wafanyakazi mkoa mzima una wafanyakazi 1,500 tu. Kwa hiyo, tuna upungufu wa asilimia 65, ni upungufu ambao ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Waziri wa TAMISEMI, Dada yangu Angellah jitahidi sana kutupatia wauguzi katika Mkoa wa Simiyu. Tunawapenda sana kazi

mnazozifanya lakini tunaomba tuongezewe wafanyakazi. Nadhani ajira zimetangazwa nyingi tunaomba basi na sisi katika mkoa wetu tuweze kupatiwa wafanyakazi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninahama hapo naenda upande wa barabara, kuna barabara ambayo imekuwa ni ahadi ya muda mrefu sana, Kolandoto – Lalago inapita mpaka Kishapu – Lalago mpaka Meatu. Barabara ile iko katika Ilani na ni ya muda mrefu, miaka mingi. Tunaomba mtupatie lami na sisi ili nasi tujisikie kwamba ni miongoni mwa Watanzania, kutoka Meatu mpaka Kolandoto tunaomba tupate barabara ya lami lakini pia kuna barabara inayotoka Bariadi inapita Itilima – Meatu mpaka Singida. Tunaomba barabara ile pia tuwekewe lami. Tunahangaika sana barabara ile ni nzuri sana na ni *shortcut* nzuri haina sababu ya kuzunguka Mwanza au Shinyanga tukishatengenezewa ile barabara magari mengi yatapita pale na uchumi wa nchi yetu utaendelea kuwa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia upande wa elimu, ninashukuru Rais wetu ametupatia madarasa mengi ya kutosha. Sekondari na *primary* madarasa ni mengi tu yanatosha vizuri lakini tatizo ni moja, changamoto hatuna walimu wa kutosha. Walimu ni wachache sana, wanafunzi ni wengi ndio wanakaa kwenye madarasa lakini hata yale madarasa yana upungufu tena wa madawati. Tunaomba wanafunzi wakae katika sehemu ambazo ni nzuri ili anapojifunza basi ajisikie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia tunaomba walimu muwasaidie waweze kupata na wawe na ofisi za kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho napenda niseme ni kwa upande wa maji. Katika Mkoa wa Simiyu

tunachangamoto kubwa sana ya maji. Maji ni tatizo sana yaani wakinamama wa Mkoa wa Simuyu, kina baba tunahangaika sana juu ya maji. Tunaomba msaada mkubwa ambao ni mwarobaini utakaotibu hili tatizo ni kupata maji ya kutoka Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hili mlifanyie kazi, TAMISEMI tusaidieni sana Mkoa wa Simiyu tunahangaika sana hasa Wilaya ya Meatu. Wilaya ya Meatu haina vyanzo vya maji muda mrefu tumekuwa tukihangaika tukilia. Nadhani Mheshimiwa Angellah ulifika katika Mkoa wa Simiyu, Wilaya ya Meatu uliona changamoto iliyoko kule ni shida huwezi hata ukapanda miti ukamwagilia. Tuna ukame wa hali ya juu sana lakini hata vile visima tulivyonavyo tena tembo wanashambulia yale maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba mtusaidie tunapoongea namna hii kweli masikitiko ukifika katika Mkoa wa Simiyu hizo wilaya zina changamoto kubwa sana, tunaomba Serikali iweze kutusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda nikiiongee hapa ni kwa upande wa walimu, nirudi samahani kule, walimu wengi wanadai malipo ya muda mrefu, wameenda likizo hawajapewa pesa zao na wengine wanachangamoto nyingi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa upande wa elimu muweze kuwasaidia. Mwalimu anafanya kazi kubwa sana unajikuta mwalimu mmoja anaweza akafundisha watoto 140 darasa moja mwalimu pekee yake lakini bado hata yale malipo yake ni shida anapoenda likizo hapati chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna upungufu wa nyumba za walimu, walimu wengi wanaishi mijini shule zao zipo vijijini unajikuta kutoka mjini mpaka kijijini kule ni kilometa

saba. Mwalimu aende na kurudi kilometa 14, tunaomba walimu wa kutoka kule kwetu Mkoani Simiyu tupate walau hata kila shule hata nyumba kumi kumi za walimu waweze kukaa karibu na mazingira ya shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niseme kuhusu upungufu sasa wa hivo vifaa katika hizo hospitali nilizozisema nadhani hilo nimeliongea na ninaamini kwamba nimeelewaka. Napenda kushukuru, naishia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. nilimtaja Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya ajiandae.

Mheshimiwa Agnes Hokororo hayupo? Mheshimiwa Stella Manyanya *Engineer*.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima lakini pili nami niungane na wenzangu na Watanzania wengi kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na jitihada ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika niipongeze Waziri hii chini ya kiongozi wetu Mama Angellah Kairuki, kwa kazi kubwa inayofanywa. Kwa sababu Wizara hii ni Wizara ambayo ni kuunganisha cha Wizara nyingine ambazo kama Wizara ya Afya, hata Wizara za Ujenzi. Unakuta Wizara hii ndio kila kitu ndio mama wa kila kitu na ndio maana hata kwenye bajeti yake unaona kwamba ni fedha nyingi sana inatengwa lakini ukiangalia mahitaji ambayo yapo ni hazitoshi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binadamu ameumba kupenda kusikia neno lile linalomfurahisha ndio binadamu wanafurahi lakini mtu anapenda kusikia neno lenye utu. Neno ambalo linagusa watu na mahangaiko ya watu, shida za watu huyo ndio mtu. Kwa hiyo, naamini Wizara hii chini ya Mama Angellah Kairuki, ninyi ni watu, sasa kwa sababu ni watu mna utu naomba mnisikilize haya nayojaribu kuyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majimbo yetu yanatofautiana sana, kuna majimbo ambayo yameeanza kupata fursa za kiwekezaji, fursa za migao ya Serikali miaka nenda rudi. Toka wakati huo enzi za mkoloni yalipata hiyo bahati lakini kuna majimbo yalisemwa kwamba haya ni pembezoni tusubiri kwanza. Yakasubiri kwa muda mrefu, sasa hivi ndio yanaanza kuibuka sawa na lile Jimbo langu la Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majimbo haya au wilaya hizi za aina hii ndizo ambazo zinachangamoto kubwa na siku nyingine nilikuwa naziita Wilaya za *TASAF* yaani ni maskini. Sasa wilaya hizi ndizo zinazokumbana na changamoto nyingi lakini kwa sasa kwa utaratibu unaoendelea naona pia hizo wilaya au haya majimbo ya aina hiyo itakuwa ni ngumu sana yenyewe kupiga hatua ya kuyafikia hayo majimbo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani nasema hivi? Tuna ile hali ambayo tunaizungumza hasa katika migao yetu ya fedha, kiurahisi tunagawa fedha kila jimbo tupate sawa. Kweli sisi Wabunge ni vizuri tupate sawa lakini mtu mwenye kata 20, vijiji 84, vitongoji 423 kama Wilaya yangu ya Nyasa. Unategemeana kwamba tukipeana kwa mtindo huo sisi tutawafikia lini hawa wenzetu ambao sasa wameshaanza kupata kwenye zile kata au vijiji vinajirudia. Vijiji 84 unahangaika upate angalu zahanati 20 za kukaa angalau kwa umbali umbali watu wapate huduma, unakuta wewe unapata zahanati moja wenzako wengine wanapata zahanati 3, 4. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo hatuwezi kulifumbia macho lazima tuseme, na tunatabia ya sisi wakati mwingine kusema tukishakuwa kwamba yule mtu tunayemfikiria hayupo dunia au hayuko kwenye kiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mheshimiwa Mama Angellah Kairuki, kwa sababu wewe una utu tunasema hapa hapa sasa hivi. Haturidhiki na mgao unavyokwenda. Kwa mfano, hata hizi shule za sekondari kuna wengine kata zao hazina hata hiyo sekondari lakini pia hata hizo kata ukiziangalia zina hali mbaya sana au zimetengwa kijiografia. Kata kama ya Mipotopoto ukienda kule Mitomoni unavuka katikati kilometa 40 ndo unafikia kijiji kingine cha Mipotopoto. Sasa kwa mazingira kama hayo hao watoto watasomaje? Lakini tumeshaandika barua nyingi ziko kwenye mabenchi yenu, tumezileta, tumelalamika na tunasema kwa dhati lakini unakuja ikija migao inaendelea kwa mtindo ule ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza changamoto ni nini? Kwamba sisi Wabunge tunasema uongo kiasi kwamba hatustahili kusikilizwa au ni nini? Lakini pia kuna hali ya kutokuwaamini wale ambao wapo kwenye maeneo. Unakuta jambo la kuweza labda pengine kuifanyia kazi kwa haraka mpaka atoke mtu Wizarani aende huko na yeye kwa sababu ya muda wake ni mfupi ataenda kukagua sehemu fulani atachagua tofauti na kile ambacho pengine hata wewe Mbunge umekipendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule niliitembelea, mfano inaitwa Songambele, shule ile nilikuta madarasa mawili yapo pamoja yana nyufa yana hali mbaya na mle watoto walikuwa wanaingia wanacheza. Nikaona kwa nini tuunde tume ya kukagua mtu gani amesababisha kifo, nikasema wananchi hali hii si hatari wenyewe tunaiona na walinilalamikia. Nikasema ndio, nikasema tubomoe kwa usalama tutaendelea na masuala ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo nimeandika barua chungumbovu kwenye Wizara hata sisikilizi hivi mlitaka nifanyaje? Angekufa kwanza mtu halafu ndio niwaambie, ndugu zangu tusiende hivyo. Mama anafanya kazi kubwa ya kutafuta hizo fedha basi tuzitendee wema na kwa haki zaidi lakini kuna majengo. Kuna jengo la Sekondari Mbamba *Bay*, nimeshasema…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Stella Manyanya, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia kwamba jambo hili limekuwa likijirudia sana na kwa kuwa jambo hili limekuwa likijirudia na wewe umekuwa ukiomba mara kwa mara na husikilizwi. Unaonaje leo Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya sisi kama Wanaruvuma tuondoke na Siwa hapa mpaka Siwa hili litakapokuja kufuatwa Ruvuma na darasa hili liwe limeshajengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nasmhukuru sana Mheshimiwa Msongozi, mdogo wangu kwa kunipa hiyo taarifa ambayo imeongeze thamani, isipokuwa Siwa nakusihii tusiondoke nayo maana yake Bunge litakuwa limeshasimama na itakua tumekosa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba ni mambo ambayo yanahuzunisha kuna majengo yapo. Kwa mfano pale Mbamba Bay Sekondari kuna jengo la ghorofa chini ya

ofisi ya utawala juu makataba, kwa sababu ule mradi ulikwisha basi hakuna hela ya kumalizia. Tunaambiwa tutenge mapato ya ndani, mapato ya ndani kwenye wilaya, Halmashauri ya Nyasa ndio hiyo ya Ki - *TASAF*. Sasa hivi tunaishusia kwamba ipunguze hata hela ya kupeleka kwenye maendeleo, tutakamilisha lini?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella.

**MHE. ENG. STELLA MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nisaidiwe, tuende tutembelee ile wilaya tuione vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. nilimtaja Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya TAMISEMI. Moja kwa moja niende kwanza kwa kuimpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kufanya kazi kubwa katika Taifa hili lakini kwa jinsi ambavyo ametugusa sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa kutupatia hospitali za wilaya katika kila halmashauri. Sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi tumebahatika kupata hospitali zenye *level* ya wilaya katika kila halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hopsitali hizo za wilaya ambazo tunazo katika halmashauri zetu hospitali nyingi zinashindwa kufanya kazi kwa masaa 24 kutokana na upungufu mkubwa sana wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hospitali kama hospitali ya Halmashauri ya Msimbo lakini Hospitali ya Wilaya ya

Tanganyika lakini Hospitali ya Halmashauri ya Mpimbwe, Hospitali ya Wilaya ya Mlele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hizi kwa kweli zina *operate* kwa *level* ya zahanati. Kama Serikali ni lazima tuhakikishe kwamba fedha hzi nyingi zilizowekezwa na Serikali katika hospitali hizi zinaenda kutumika vizuri kwa kupeleka watumishi ili wananchi waliokusudiwa waweze kupatiwa huduma iliyobora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Katavi kwa upande wa upungufu wa watumishi kwa upande wa afya pamoja na elimu. Tunaupungufu wa watumishi kwa asilimia 56.18. Kwa upande wa Wilaya ya Tanganyika tunaupungufu wa asilimia 66, katika Wilaya ya Mlele tuna upungufu wa asilimia 61 upande wa Nsimbo tuna asilimia 63.2, upande wa Mpanda Mjini tuna upungufu wa asilimia 36.1 na upande Mpimbwe tunaupungufu wa asilimia 69.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huo ni mkubwa na wananchi wanakutana na adha mbalimbali kutokana na kwamba wanashindwa kupatiwa huduma Serikali iliyokusudia kwa kujenga hospitali hizo za wilaya katika Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naipongeza Serikali kwa kuleta pesa nyingi katika kuwekeza katika vituo vya afya pamoja na zahanati. Katika Mkoa wetu wa Katavi tuna zahanati nyingi ambazo Serikali imeziwekeza, hadi hivi ninavyoongea kuna zahanati zaidi ya 16 ambazo zimeshindwa kufuguliwa kutokana na upungufu mkubwa sana wa watumishi na kufikia mwezi wa Sita tutakuwa na zahanati zaidi ya 26 ambazo zinashindwa kufunguliwa kutokana na upungufu mkubwa wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vituo vya afya, kuna vituo vya afya ambavyo vimejengwa ikiwepo Ilunde, Majimoto, Mwamapuli, Gulamata na kwa upande wa Kibaoni. Zahanati hizi na vituo vya afya nyingi zinashindwa kufanya huduma ya upasuaji na matokeo yake wagonjwa wengi wakienda pale wanapatiwa tu *paracetamol*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali kupitia Wizara hii ya TAMISEMI, kwa kuwa tumepata ajira 21,000. Tunaomba wananchi wa Mkoa wa Katavi tuweze kukumbukwa tuangalie wanaopata adha hapa sana sana ni mama zangu wa Mkoa wa Katavi. Unakuta kituo kama hiki Kituo cha Afya cha Kibaoni, cha Kasansa na Majimoto, vinashindwa kufanya huduma ya upasuaji. Sote tunaelewa wakina mama wengi wanapoenda kujifungua kuna wengine wanatakiwa wafanyiwe upasuaji lakini zahanati hizi na vituo vya afya havifanyi huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Waziri wa TAMISEMI aliangalie kwa jicho la pili suala hili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kupelekewa watumishi ili waweze kuhudumiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambapo nilikuwa napenda kulichangia, katika ajira na usawa, natokea katika mikoa ambayo ipo pembezoni. Mfano Mkoa wetu wa Katavi, kuna Mkoa wa Kigoma lakini kuna Mkoa kama wa Lindi. Watumishi wengi wanapopangiwa maeneo haya wanashindwa kuja kufanya kazi kutokana pengine na miundombinu ambayo hawaijawa *supported*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara iweze kuboresha mazingira ya walimu pamoja na watumishi hususan wa afya ili wanapokuja kupangiwa katika maeneo haya waweze kufanya kazi katika mazingira yaliyobora ili wasiweze kutukimbia. Kwa kweli unakuta wafanyakazi wanapopangiwa katika mikoa hii kwa mfano Mkoa wangu

wa Katavi unakuta mtu amepangiwa eneo la Gulamata lipo upande ule wa Mishamo. Ni eneo ambalo ni mbali usipomuwekea miundombinu mizuri, mtumishi huyu lazima ataomba kuhama aweze kuhamia maeneo mengine. Ila tukiwawekea mazingira rafiki na mazuri lazima watumishi hawa watakaa waweze kufanya kazi na kusaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nilikuwa napenda kuchangia ni kuhusiana na kuboresha kitengo cha wakaguzi wa ndani. Katika kuboresha kitengo hiki cha wakaguzi wa ndani linaweza likamsaidia sana CAG. Kitengo hiki kimekuwa kwanza hakitengewi bajeti ya kutosha lakini pia wanakosa uhuru kutokana na kwamba wanafanya kazi kubwa ambayo wanakuwa wanamuangalia Mkurugenzi aweze kuwapatia mafuta lakini wanamuangalia Mkurugenzi ndio aweze kuwapatia magari ya kwenda kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Serikali waboreshe kitengo cha wakaguzi hawa wa ndani ili waweze kudadavua na kutoa madudu yote ya pesa zinazoliwa katika halmashauri zetu. Tukiwawezesha hawa wakaguzi wa ndani kwa kweli kazi kubwa itafanyika katika halmashauri zetu na fedha zote zinazopelekwa na Serikali ziitaweza kusimamiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Festo Mariki, tunaendelea na Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mheshimiwa Dkt. John Pallanyo na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunge ajiandae.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliopo mbele yetu hoja ya TAMISEMI. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Dada yangu Kairuki na Manaibu wake wawili mapacha kwa kazi nzuri wanazozifanya hakika nimejionea. Mheshimiwa Kairuki hata ukipiga simu saa nane usiku anapokea. Anapokea anakusikiliza lakini pia hata Manaibu wake wawili wanapokea simu wanakusikiliza wanakutatulia changamoto, hongera sana, huo ndio uwajibikaji na utumishi ulio wa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kumsahau Mkuu wangu wa Mkoa Queen Sendiga, naye nampongeza sana anaisimamia ilani vizuri katika Mkoa wetu wa Rukwa. Kipekee nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya. Wanawake na wananchi wa Mkoa wa Rukwa wamenipa salamu tunamshukuru sana, tumeweza kupokea miradi; miradi ya madarasa, miradi ya maji, miradi ya barabara, miradi mingi fedha nyingi sana tumezipokea katika Mkoa wetu wa Rukwa. Hongera sana Rais wetu, chapa kazi tuko pamoja na wewe, 2025 kitaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Simba. Wamembamiza mtu jana, wamembamiza vibao viwili. Hongera sana *Simba Sports Club*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa kwenye hoja zangu za msingi. Mkoa wangu wa Rukwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kuniona. Naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba wananchi hawakututuma huku ndani kuja kuongea ushindi ushindi wa michezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe naomba uipokee hiyo taarifa, uipokee hiyo taarifa.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsamehe ngoja niendelee asinipotezee muda.

**MWENYEKITI:** Uipokee hiyo taarifa.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei. Niingie kwenye suala la 10% ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu…

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Haya taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba miongoni mwa mambo ambayo Mheshimiwa Rais anayaunga mkono ni pamoja na mambo ya michezo. Kwa hiyo kilichofanyika jana ni jambo ambalo linaendeleza hamasa kubwa ya Mheshimiwa Rais na Simba wameitekeleza kwa vitendo. Naomba kutoa taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo taarifa ya mwisho kuhusu suala la michezo. *(Makofi)*

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa kwenye mambo yangu ya msingi nianze kuongelea suala la 10% ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Nimshukuru sana Rais na Serikali yetu. Kwa kweli jambo hili la 10% ni zuri sana na limefanya hamasa kubwa sana kwenye jamii yetu, lakini nimesikia juzi Mheshimiwa amesema kunakuwa na ubadhirifu wa fedha ambazo zinapotea bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha kama zinapotea tusiwahukumu wanawake wale wanaokopa. Wale wanawake wanaokopa na vijana wanarudisha kwa uaminifu mkubwa sana. Wanacheza *VICOBA* wanarudisha. Hizi fedha kama zinapotea inawezekana kuna vikundi hewa ambavyo vinapoteza hizo fedha kwa asilimia kubwa. Naomba tuliangalie vizuri. Hii fedha ibakie kwanza halmashauri, wanawake wakihamishiwa mikopo hii kwenye mabenki wengi wao watashindwa kwenda kukopa kwa sababu ya dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 10% hii inasaidia sana makundi haya na sisi kama Mkoa wa Rukwa tunasubiri sana hii utaratibu ulioanza wa kilimo tunasubiri tunajua kwamba 10% hii itasaidia sana wanawake wengi wanalima Mkoa wa Rukwa kwa hiyo 10% hii, 4% na 2% itawasaidia sana makundi haya kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Rais kwa kutangaza ajira 21,200. Ajira ni nzuri, nyingi sana na tunamshukuru sana Rais kwa kujali watoto wake ambao wamesoma lakini wanaishi mitaani hawana kazi. Ushauri wangu, hizi nafasi 21,200 zigawanywe kwenye mikoa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nafasi ni Rais na Serikali yetu inatangaza kila mwaka. Mwaka uliopita ilitangaza ajira 6,000 lakini wengine mikoa mingine hatukuona kama kuna vijana wetu ambao wamepata hizi ajira. Ushauri wangu, hizi ajira

zigawanywe kwenye mikoa tugawanye kwa uwiano bila kupendelea ili vijana wa mikoa yote waweze kufaidika na hizi ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe ahsante sana muda umekwisha.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ilio nichangie kwenye hii Wizara ambayo ni Wizara muhimu sana iliyotubeba sisi Wabunge, Wizara ya TAMISEMI chini ya Ofisi ya Rais, lakini ambayo inasimamia Tawala za Mikoa, halmashauri zetu na kule kwetu tunakotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwanza kushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi ambayo anawafanyia Watanzania. Anatubeba Watanzania kama watoto wake, kama mama anavyobeba watoto wake. Amesambaza fedha majimboni, kila jimbo, ukijaribu kufuatilia kila Mbunge akisimama anazungumzia habari ya mabilioni mabilioni na sisi kule Arumeru Mashariki pia tumepata hiyo neema ya kupokea mabilioni. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Dada yetu Mheshimiwa Angellah Kairuki pamoja na wasaidizi wake Mheshimiwa Dkt. Dugange na Mheshimiwa Deo Ndejembi ambao kusema kweli wanafanya kazi nzuri. Kwa dhati kabisa niseme kwamba hawa vijana wawili ni vijana wema sana lakini Mheshimiwa Waziri naye ni mwema sana, kila Mbunge amesema kwamba akipigiwa simu anapokea, kama asipopokea anarudisha ujumbe kwamba nitakupigia. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tumepokea fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo Jimboni kwangu. Naomba niseme machache kisekta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimboni kwangu changamoto kubwa sana ni miundombinu ya barabara. Ni ngumu kwa sababu lile jimbo letu sehemu kubwa limebeba Mlima Meru, kwa hiyo wananchi wanaishi kwenye miinuko, miteremko ya Mlima Meru na kwa hiyo miundombinu barabara huwa zinaharibika sana kila msimu wa mvua na barabara nyingi ni za udongo na changarawe. Kwa hiyo tuna shida kubwa ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niseme kwamba *TARURA* wamekuwa wanafanya kazi nzuri. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mtendaji Mkuu *Engineer* Seif, kwa kazi ambayo anafanya. Ni kijana mzuri ambaye ukimpigia simu anapokea na anachukua hatua saa hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu nina barabara ambazo ni ahadi za Viongozi Wakuu. Barabara ya King'ori ni ahadi ya Rais kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini mpaka sasa hiyo ahadi haijatekelezwa. Hiyo barabara inaanzia Malula – Kibaoni - Ngarenanyuki lakini inapitia King'ori. Kutoka Ngarenanyuki iko chini ya *TANROADS,* lakini ni

barabara muhimu Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri. Ile barabara ikijengwa kwa kiwango cha lami itakuwa *bypass* ya mashariki ambayo itasaidia sana utalii kwenye lile jimbo na kuchangia uchumi kwa kuwa itazalisha ajira kwa kata nane ambako inapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana waifikirie ni ahadi ya Rais na ahadi ni deni na kusema ukweli ahadi za Viongozi Wakuu zinatusumbua na ziko nyingi. Nilitoka kuzungumza na Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde akaniambia inatakiwa ifanyike *operation* ya kuondoa madeni haya ya ahadi za Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* wamepata shilingi bilioni 855. Fedha hizi kila tukizichambua bado ni kidogo. Bajeti ya *TARURA* iko chini kwa sababu wanahangaika na barabara za vumbi, changarawe ambazo huwa zinaathiriwa sana na hali ya hewa. Kwa hiyo tuiombe *TARURA* waongezewe fedha na kule kwetu ambako barabara zinapanda milimani na siyo kwetu tu, maeneo yote ambayo yana milima *TARURA* wanapata shida sana. Waongezewe fedha, sisi kwa mwaka tunapata kama shilingi bilioni mbili kama na nusu. Hizo fedha ni kidogo, tungepata kama shilingi bilioni tano, ungeona Wabunge wangekuwa watulivu. Wangeona kwamba kazi zinafanyika na zinaonekana. Kwa sasa hivi nakiri kwamba Bajeti ya *TARURA* iko chini. *TARURA* wanafanya kazi vizuri lakini hawapati fedha za kutosha, muhimu waongezewe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafuatilia pia kupanga na kusema kwamba tunatoa fedha kiasi Fulani, ni suala moja lakini kutekeleza kwa maana ya kutoa fedha miradi itekelezwe ni suala lingine. Taarifa nilizonazo ni kwamba sisi tulipata shilingi bilioni 2.1 kwa mwaka huu wa fedha ambao tunamaliza kesho kutwa, lakini mpaka sasa tumepata shilingi bilioni moja na chenji. Utekelezaji unafanyika umeshafikia 46%

peke yake. Tunaomba fedha zitoke kwa wakati ili miradi ambayo imepangwa kutekelezwa itekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali. Toka kipindi cha miaka miwili ya Mheshimiwa Rais aliyokaa madarakani, Sekta ya Afya tumepata fedha nyingi. Nimepata Kituo cha Afya cha Mareu, kazi iliyofanyika ni nzuri sana, lakini niseme kwamba tulipata ahadi ya vituo vitatu vya kimkakati kwa kila tarafa. Sasa namuuliza Mheshimiwa Waziri, nimepata kituo kimoja, vile viwili viko wapi? Pale Karangai kuna eneo tumetenga kwa ajili ya kuweka kituo cha afya naomba wakumbuke mwaka huu wa fedha tupate kituo kingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana, kengele imeshalia.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni ya kwanza, si bado ya pili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni ya pili hiyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga; Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Boniphace Butondo wajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya TAMISEMI. Kiukweli niseme tu kwamba nilikuwa najaribu kupitia pitia taarifa ya Mheshimiwa Waziri, lakini

mengi niliyokuwa nikiyapitia sioni yale ambayo nilitamani kuyasema. Mimi nitasema ya kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie nilipoishia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu kuhusiana na suala zima la hizi shule kongwe. Nadhani hapa sasa leo ndiyo hasa sehemu yenyewe. Niiombe sana Wizara ya TAMISEMI na kwa bahati nzuri wakati tunatembelea miradi tulikuwa na Mheshimiwa Dugange, anajua nilichoomba na naendelea kusisitiza kwenye taarifa hii hapa sasa hivi. Hebu tujitahidi, ni aibu kubwa shule kongwe ambayo hata Baba wa Taifa amesoma, inatia aibu. Naomba sana wasitegemee sisi Tabora eti mapato ya ndani yaweze kufanya karabati za shule zetu kongwe, haiwezekani kwa sababu hatuna fedha hiyo, kutokana na mapato yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shule hizo niongelee hata shule nyingine za msingi. Tuna Shule moja inaitwa *Town School*. Hii shule imeanzishwa mwaka 1940, ujenzi wa shule hii umetumia mawe. Hapa ninavyozungumza shule imechoka kweli kweli. Sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mambo ya kuja Tabora waje watupe pole watoto wetu kule wameangukiwa na madarasa, jamani hatutaki. Kinga ni bora kuliko tiba. Nawaomba sana pamoja na shule nyingi kuwa kongwe na zina changamoto, lakini naomba hii Shule ya *Town School* waiangalie kwa jicho la peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombeni sana na niombe mbele ya Bunge hili tukufu mambo ya kuja kupeana pole, hapana. Tunaomba watusaidie hii shule ni ya toka mwaka 1940, ina changamoto, imechakaa sana na iko kati kati ya Kata yetu ya Gongoni. Kwa hiyo niombe sana Wizara iangalie hizi shule kongwe na hizi za msingi maana walikuwa wanahangaika na shule za sekondari na hizi za msingi nyingi zimechoka sana. Kwa hiyo tunaomba sana waweze kuzifanyia ukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombee *TARURA* fedha. *TARURA* inahitaji kuongezewa bajeti. Mimi natoka Mkoa wa Tabora na hapa naomba nizungumzie hususan kwenye Jimbo ambalo natokea mimi la Tabora Mjini. Kwenye kata zetu kuna mitaa mbalimbali, kuna vijiji na kuna vitongoji. Barabara hazipitiki, leo nikikwambia hizo kata zetu za mjini barabara nyingi za ndani kwenye mitaa yetu ni barabara za vumbi. Hazina mitaro, mvua ni nyingi zikinyesha maji yanaingia kwenye nyumba za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana wakati wanafikiria kununua magari ya ma-*DC* na ma-*RC* na watu wengine, tunaomba sana bajeti iongezwe kwenye *TARURA*. Wananchi wetu wanateseka, wanapata shida. Mvua zikinyesha maji yanaingia ndani. Sisi hatukatai ununuzi wa magari, wanunuliwe kwa sababu ni watendaji, lakini watapita wapi huko hawa ma-*DC* kama barabara ni mbovu. Lazima wawatengenezee na barabara kwanza ili yale magari watakapowanunulia waweze kupita kwenye sehemu salama. Wapunguze bajeti kidogo wazipeleke kwenye *TARURA* ili hawa watu waweze kufanya kazi vizuri jamani, wananchi wetu wanalalamika. Barabara za mitaani nyingi ni mbovu na *especially* sasa hivi mvua ndiyo zimekatika, wawape hizo fedha watu wa *TARURA* ili waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya hii miradi ya afya ambayo haikamiliki, ni aibu kubwa. Amezungumza Mheshimiwa Mbunge wa Itilima, Mheshimiwa Njalu. Amesema, hizi fedha wanazopeleka kwa maelekezo wanakosea. Maeneo mengine wananchi wameshatumia nguvu kubwa ya kujenga zahanati, vituo vya afya, wakiwapelekea fedha shilingi milioni 500 hii eti nendeni mkajenge kituo cha afya wanacha yale majengo waliyokuwa wameshayajenga, wanaenda kujenga majengo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepita huko Naibu Waziri wa TAMISEMI anajua, kuna majengo mengine ya afya yamekaa mpaka yameshachakaa hayajatumika kwa sababu ukiwauliza wameanza kujenga miradi mipya kwenye maeneo hayo badala ya kuwa wamepewa fedha ama TAMISEMI waulize kwenye maeneo wanayopeleka fedha, je, mnahitaji kujenga vituo vya afya maeneo gani na maeneo gani? Mnahitaji kujenga hospitali za wilaya zipi na zipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta hospitali ya wilaya tayari ilishajenga majengo saba, Serikali imepeleka fedha ya kujenga majengo mengine matatu. Yale saba yanaachwa, yanajengwa yale matatu ambayo zile fedha wamepeleka. Kwa nini zile fedha wasiwaambie kwamba wamalizie yale majengo ili watu waweze kupata kutumia hayo majengo. Fedha nyingi za Serikali zinazopelekwa, Mheshimiwa Rais anapeleka fedha nyingi lakini hazina thamani kwa wananchi kwa sababu hawatumii miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo kwenye elimu wanajitahidi kwa sababu tunaona watoto wetu wanasoma madarasani lakini hawana madawati. Kuna mikoa ambayo unapita kuna baridi ya hatari. Sisi tumeenda Sumbawanga huko Rukwa, tumeenda Katavi kuna baridi kweli kweli. Wanajenga madarasa mawili mnatoa madawati 30, kila darasa madawati 15, 15. Darasa gani la Tanzania ambalo watoto wanakaa 45? Darasa moja watoto 100, watoto 70 watoto wote 40 unakuta wamekaa chini na baridi iliyoko katika mikoa hiyo mpaka unasikia huruma wewe mzazi tumbo linakucheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe wakati huu ambapo wako kwenye bajeti waweke bajeti wasaidie halmashauri zetu waweze kupata madawati. Pamoja na halmashauri zetu kujikongoja, lakini bado Serikali inatakiwa isaidie wananchi wetu, kule watoto wetu wa Kitanzania

waweze kusoma wakiwa wamekaa kwenye madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la hii 10%. Ni aibu kubwa, amezungumza Mheshimiwa Halima hapa na ndiyo ukweli ulioko huko chini. Hizi fedha hazijapotea hizi zipo. Kuna maeneo tumekwenda kuna kikundi cha familia; baba, kaka, mtoto wa baba mkubwa, mtoto wa mjomba, mtoto wa nani. Wamekaa sasa pale ehee, biashara gani ambayo mnafanya tunawauliza, wanaanza ooh, vikaenda vikarudi, vikafanyaje. Wamepewa zaidi ya shilingi milioni 30. Hiyo fedha inarudi na nini? Unawauliza wamebaki hawa, wawili. Sasa hawa wengine wako wapi? Wameingia mitini. Unamuuliza Afisa Maendeleo ya Jamii wakati unakuja kukikagua hiki kikundi ulijua kwamba hawa watu wakoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha kupitia Bunge lako Tukufu tunataka pamoja na kusimamisha mikopo ya 10%, hizi fedha kwanza zirudi. Zirudi fedha hizi za Watanzania walipakodi, wavuja jasho, halafu ndiyo tuanze mpango mzima wa kuhakikisha tunaanza kugawa tena hizi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla hatujaanza kugawa fedha hizi huko kwenye halmashauri wapelekwe wataalamu wa fedha kwenye vikundi hivi ili waweze kusaidia wananchi wetu kujua miradi. Hawa maafisa maendeleo wa jamii mnaowapelekea hizi kazi si za kwao; na ndiyo maana maeneo mengi wamefeli kwa sababu hawana ushauri mzuri kwa vikundi wafanye biashara gani ili waweze kutoa marejesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ajirini maafisa maendeleo ya jamii kwenye maeneo husika, na mnapoajiri msiajiri kwa upendeleo. Tumekwenda eneo moja jimbo lina kata 19, maafisa maendeleo wa jamii wako 43 wako kwenye

jimbo moja. Katika mkoa huo kuna jimbo lina kata 27 lina maafisa maendeleo ya jamii wawili, kuna jimbo lingine kina kata 27 maafisa maendeleo wa jamii watatu. Sasa kata 27 zinafanywaje kazi maafisa maendeleo ya jamii 23? Hapo ndipo utakapoona huu ubabaifu wa hizi fedha unapoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingine, watendaji wetu wasiokuwa waaminifu wa TAMISEMI, wanachukua fedha hizi kwa visingizio vya vikundi halafu wanazichukua wao wenyewe. Ndiyo maana tunasema hili Bunge tusikubali fedha hizi zipotee, hizi fedha lazima zirudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme, namshukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipangia kwenye kamati ya *LAAC,* nitakuwa nasema kila siku hizi fedha mpaka zirudi ndipo zitoke fedha zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hawa. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Boniphace Butondo na Mheshimiwa Anton Mwantona wajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema kwa kunijali afya na kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niunge mkono hoja. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa TAMISEMI kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM, nampongeza sana Rais wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kusahau ninaomba nimwombe Mheshimiwa Waziri; kwanza nimpongeze kwa kuajiri walimu na watumishi wa afya. Baada ya hapo niombe ombi maalum, naomba watumishi waalimu na wa kada ya afya waletwe Mkoa wa Kigoma, Kigoma ya sasa si ya zamani. Sasa hivi tuna barabara na zinaendelea kujengwa, lakini pia tumeshapata umeme wa *grid* ya Taifa; kwa hiyo Kigoma ni maeneo mazuri ya kuweza kuishi watumishi kwa sasa. kwa hiyo tunaomba mtuletee watumishi, Kigoma sasa hivi tuna barabara na tuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwa jinsi vituo vya vilivyojengwa zahanati, hospitali za wilaya, vilevile hospitali za mikoa zikakarabatiwa na nyingine zikapatiwa hadhi ya kuwa hospitali za rufaa, ikiwemo na Hospitali ya Mkoa wetu wa Kigoma. Ombi maalum; ninaomba mtuletee watumishi. Kwa mfano katika Wilaya ya Kasulu tumeweza kupatiwa fedha bilioni 3.6, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, lakini tulipata msaada kutoka kwa wadau milioni 500 kwa ujenzi wa nyumba za watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nyumba tunazo na miundombinu ni mizuri. Tumepata vifaa vya thamani ya bilioni 1.5 kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Kasulu DC ambayo ni Hospitali mpya ya Wilaya ya Halmashauri ya Kasulu DC. Hivyo basi changamoto tuliyonayo ni kwamba hatuna watumishi, hatuna wataalamu wa mionzi, maabara na huduma ya meno. Kwa hiyo tunaomba tupatiwe wataalam angalau hata watano kuja katika Halmashauri ya Kasulu DC kwa sababu hospitali hiyo ni mpya inahitaji wataalam wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi moja; Kata ya Kagera Nkanga ipo kilometa 80 kutoka Makao Makuu ya wilaya; ninaomba tujengewe kituo cha afya kwa sababu ni kutoka kituo hicho kuja mjini kilometa 80 tunaweza kuangalia ni kwa umbali gani. Wanawake wanapoteza maisha kwa ukosefu wa huduma ikiwemo kupoteza damu nyingi wanapokuwa wamecheleweshwa kufikishwa kwenye hospitali ya wilaya. Si hivyo tu, eneo hilo kuna majambazi wanateka sana katika aneo hilo la kutoka Kagera Nkanda kuja Kasulu au Kasulu kwenda Kagera Nkanda, kilometa 80. Angalia, kilometa zote hizo kwenda kufata huduma eneo lingine tunaomba kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Buhigwe, wilaya anayotoka Makamu wa Rais, na wakati alipokuwa akigombea, alienda katika Kata ya Mkatabnga akashuhudia wananchi wametumia nguvu wameshaanza kujenga jengo la kituo cha afya. Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Angellah Kairuki nakuomba sana, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa wananchi wameshajitolea wameshaweka msingi wana matofali ya akiba, nakuomba mama yangu utupatie kituo cha afya katika Kata ya Mkatanga Kijiji cha Kitambuka. Nakuomba sana utusaidie kwa sababu wananchi wameshaonesha njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri ninaomba uiangalie *TARURA* kwa macho ya huruma kwa sababu, kwa mfano sisi Mkoa wa Kigoma hatuna mgodi wa dhahabu, wananchi wetu ni wakulima na kilimo kinafanyika shambani. Tunaomba utupatie pesa ili barabara zinazoenda mashambani barabara zinazounganisha vijiji na vijiji, barabara zinazosafirisha mbolea kupeleka mashambani ziweze kujengwa kwa mfuko wa *TARURA*. Kwa hiyo tunaomba *TARURA* waongezewe pesa barabara zinazoenda mashambani zinazounganisha vijiji vyetu ziweze kujengwa na kupitika kiurahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephine Genzabuke, nilimtaja Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mheshimiwa Anton Mwantona ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara muhimu kabisa ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba na mimi nirudishe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama Samia Suluhu Hassan. Hii ni kwa namna ambavyo Watanzania tumeshahudia fedha nyingi zikiletwa katika majimbo yetu katika sekta mbalimbali na wananchi wamekuwa wakishihudia na kujionea wenyewe jitihada kubwa za maendeleo katika sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie pia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake wote, Katibu Mkuu  na Watendaji wengine wote katika Wizara hii ya TAMISEMI kwa namna ambavyo wamejipanga kuhakikisha wanasimamia wizara hii vizuri; na sisi wananchi wa Kishapu tunawapongeza kwa namna ambavyo wamekuwa pamoja kabisa kuhakikisha kwamba mambo ya maendeleo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Mdeme. Mkuu wangu huyu ni Mkuu wa Mkoa wa aina ya pekee kwa sababu ana ushirikiano wa karibu na sisi Wabunge na halmashauri zetu zote katika Mkoa wa Shinyanga. Nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mkuu wa wangu wa Wilaya Mheshimiwa Mkude, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Bwana Emmanuel

Johnson, pia nimshukuru Mwenyekiti wa Halmashauri yangu ya Kishapu na Waheshimiwa Madiwani kwa namna ambavyo tunashirikiana kwa pamoja kupeleka mbele maendeleo katika wilaya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nikuhakikishie kwamba nimepokea zaidi ya bilioni 11 kwa mwaka wa fedha uliopita lakini mpaka sasa nimeshapokea tena bilioni nane ambazo bilioni hizi zimekwenda kutekeleza shughuli mbalimbali za kimaendeleo kwenye jimbo langu ikiwemo sekta ya barabara, maji, elimu, afya na maeneo mengine yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya mambo ambayo nataka niyazungumzie katika eneo la barabara, nimepokea zaidi ya bilioni 2.43. Fedha hizi mpaka sasa ninavyozungumza ipo miradi muhimu kabisa ambayo inatekelezwa. Mradi wa Mwajidalala Bulekela ambapo kuna kunyanyua daraja na kuweka makalavati, barabara ambayo inakwenda kuunganisha Wilaya ya Kishapu na Wilaya ya Igunga. Pia kuna Mangu-Somagedi kuna fedha, tayari sasa hivi fedha zipo na mradi unatekelezwa; na Ngunga pamoja na maeneo ya Munze. Kuna barabara ya Seseko, Busangwa, pia kuna Barabara ya Buganika Kabila. Barabara hizi zote mpaka sasa hivi wakandarasi wako *site* na shughuli zinakwenda vizuri. Kwa hiyo katika eneo hili la *TARURA* ninashukuru kwa sababu miradi mingi naamini kwamba itatekelezwa na maeneo haya yote yalikuwa maeneo korofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana na ninaomba tuamine. Meneja wa *TARURA* wilayani kwangu Kishapu anafanya kazi nzuri na sisi Madiwani tunampa ushirikiano mzuri kazi zinakwenda vizuri. Jitihada zinazotakiwa ni kuwaongezea fedha…

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili barabara nyingi ziweze..

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Butondo.

**TAARIFA**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanta sana nataka kumpa taarifa Mheshimiwa anayechangia, ukiifungua barabara inayotoka Kishapu kwenda Igunda utakuwa umeunganisha Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Simiyu, kama ambavyo sera yetu inasema kila mkoa uunganishwe na barabara ya lami kwa maana ya barabara kubwa. Pia itakuwa ni *shortcut* nyepesi ya kutoka Simiyu Shinyanga kupita Tabora kwenda Mbeya, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa ya Mheshimiwa, ni taarifa ya muhimu kabisa. Naomba niendelee upande wa sekta ya elimu. Katika sekta ya elimu tuna upungufu mkubwa wa walimu kwanza mahitaji ni 1983 waliopo ni 922 upungufu ni 1,061, ni idadi kubwa sana ya walimu. Sasa kama tunasema kipaumbele chetu katika nchi yetu ni elimu, elimu, elimu, ni lazima jitihada kubwa ifanyike kuhakikisha kwamba tunaongeza walimu ili mradi tatizo hili liweze kuondoka. Vivyo hivyo hata katika sekondari mahitaji ni 482 waliopo ni 403 pungufu ni 79, bado ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu katika ajira hizi zilizotangazwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba sana kipaumbele wapewe walimu ambao wamekuwa wakijitolea katika maeneo yetu; na hii tumejionea wenyewe. Tumekuwa tukipata ajira za watumishi kutoka maeneo mbalimbali lakini wanapofika katika maeneo hayo, baada ya muda mfupi wimbi kubwa la watumishi wanaandika barua za kuomba kuhama. Sasa kwa nini Serikali tunatumia *resources* nyingi kwa ajili ya kuhamisha, kuwaondoa mahali pengine na maeneo mengine yanabaki kuwa na ma-*gape* makubwa na hasa ambayo yako pembezoni? Naomba sana, hawa walimu wanaojitolea hata katika sekta ya afya pia tuweke kipaumbele na tuwatizame, kwa sababu tayari wakurugenzi, maaifisa elimu wamekuwa wakitoa taarifa huku wizarani, zinazoonyesha walimu wanaojitolea lakini na madaktari wanaojitolea, hawa ndio wapewe kipaumbele katika ajira hizi zitakazokuwa zinatangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie mahitaji katika sekta ya afya. Tunahitaji watumishi 664 lakini waliopo ni 274 na upungufu ni 391; unaweza ukaona kwamba ni upungufu mkubwa sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishukuru sana Serikali ya Mama Samia kwa namna ambavyo mmeweza kutusaidia katika Hospitali yetu ya Wilaya, kwa mwaka uliopita tulipata bilioni 1.3 Hospitali yetu ya Wilaya, Kalitu tulipata milioni 900, milioni 500 Negezi, milioni 300 Mwangalanga na Shinongela milioni 50. Lakini kwa mwaka huu wa fedha Jakaa tulipata milioni 500, Hospitali yetu ya Wilaya tumepata milioni 50, Wella *dispensary* tumepata milioni 500 Mwamalasa. Hii miradi mpaka sasa ninavyozungumza inakwenda kwa kasi. Naomba niwapongeze sana Madiwani wangu kwa namna ambavyo wamejipanga kusimamia na kuhakikisha kwmaba miradi hii

inakwenda vizuri, na niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, ninaomba sana; kuna maboma zaidi ya 32 ambayo yanahitaji kukamilishwa katika sekta ya afya. Kwa hiyo nitoe ombi kwamba katika eneo hili tuone umuhimu wa kupeleka fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha maboma. Jambo lingine nilitaka nizungumzie upande wa ukaguzi. Tumeshuhudia kwamba taarifa ya *CAG* kwa sehemu kubwa tumeona upotevu mkubwa wa fedha. Sasa napozungumzia katika halmashauri hatuwezi tukawa na halmashauri imara na zinazosimamia vizuri taratibu, kanuni zile za kifedha na matumizi ya fedha kama hatujawa na wakaguzi wa kutosha katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ina mkaguzi mmoja tu wa ndani. Nataka niulize kata 29 halmashauri penyewe pale Makao Makuu, huyu ni mkaguzi mmoja anawezaje kusimamia shughuli hizi zote katika wilaya ya nzima? Ipo miradi inayotekelezwa katika ngazi ya kata, ipo miradi inayotekelezwa ngazi ya wilaya, majengo mbalimbali, miradi hii inayotokana na mapato ya ndani, fedha za ruzuku na wahisani wengine mbalimbali huyu anajigawa vipi, mkaguzi wa ndani mmoja peke yake? Akiugua homa mwezi mmoja halmashauri ina-*paralyze*. Hebu tuangalie mama yangu kama kweli una nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba hizi hati chafu, huu upotevu wa fedha hautoki ni lazima tufanye mikakati ya lazima kuhakikisha tunapeleka wakaguzi katika halmashauri zetu. Hili nilitaka niombe sana lifanyiwe kazi ili tuweze kudhibiti haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala la Madiwani. Tumezungumza kwa muda mrefu kwamba Waheshimiwa Madiwani walipwe kupitia Serikali, tunaishukuru Serikali kwa uamuzi wake kuamua kulipa fedha hizi moja kwa moja kupitia Serikali Kuu, lakini bado

changamoto kubwa ni suala zima la fedha wanazolipwa, ni kiasi kidogo sana. Majukumu wanayoyafanya na kusimamia mabilioni haya hayastahili na kile ambacho wanalipwa kutokana na usimamizi wanaofanya. Hebu tuoneni utaratibu wa kuwasaidia hawa watu, na ni wa muhimu sana. Sisi Wabunge bila wao hatuwezi chochote kile. Ninaomba sana Serikali muwe wasikivu Serikali ya Mama ni sikivu. Ninakuomba Mheshimiwa Kairuki ufanye jitihada zote kuhakikisha kwamba ushawishi huo unatokea na Waheshimiwa Madiwani waweze kuongezewa stahili zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni waraka unaohusiana na Kamati ya Fedha kufanya ukaguzi wa miradi kila baada ya miezi minne, utaratibu huu ni wa ajabu kabisa. Kanuni zinasema kamati za kudumu zitakwenda kila baada ya miezi minne kwenda kukagua miradi iliyotelekezwa katika kipindi hicho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana; tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Anton Mwantona, Mheshimiwa Abeid Ramadhan Ihondo ajiandae.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni mimi nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia mpango wa bajeti katika Wizara hii ya TAMISEMI. Nishukuru na nimpongeze sana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Angellah Kairuki, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ndejembi pamoja na Mheshimiwa Dugange, Katibu Mkuu na wote walio katika Wizara hii ya TAMISEMI wametengeneza bajeti nzuri ambayo

inaenda kutatua matatizo ya wananchi katika ngazi za chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niseme wazi kwamba namshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Biblia inasema kila jambo lina wakati wake. Kipindi hiki ni cha Mama Samia na yuko tayari kuwasaidia Watanzania kutatua matatizo yao mbalimbali ambayo yanatukabili kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na *TARURA* nampongeza sana Mkurugenzi wa *TARURA* pamoja na Injinia ambaye amewekwa kule chini kijana wangu mmoja anaitwa Kamara anatusaidia sana kutatua matatizo ya barabara katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kwamba kuna barabara ambazo zilikuwa hazipitiki miaka na miaka; kuna barabara ya kutoka Maskulu mpaka Kikole. Hii barabara iliwekewa jiwe la msingi na kipindi kile alikuwa anaitwa Salim Mohamed Salim, lakini kwa bahati mbaya hii barabara haikutengenezwa. Mama Samia ameingia madarakani tumeletewa milioni 473 barabara kutoka Maskulu mpaka Kikole imetengenezwa na wananchi kule wanafurahia matunda ya uhuru wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara ya kutoka Kapugi kuelekea Lienje, pia ilikuwa ni barabara ya miaka mingi haikutengenezwa; lakini Mama Samia ametuletea pesa zaidi ya milioni 270 barabara imetengenezwa na sasa iko katika hali nzuri wananchi wanafurahia matunda ya uhuru wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi sana katika barabara. Mimi wakati naingia kama Mbunge kuna barabara zaidi ya nne zilikuwa hazipitiki kabisa lakini leo ni barabara moja tu ambayo imebaki ambayo ni kutoka

namba *one* pale Idweri kuelekea Ngumbulu. Namwomba sana Waziri aliangalie hilo kwa sababu ni barabara pekee ambayo imebaki ambayo kwa sasa hivi upitaji wake umekuwa ni mgumu, tuwasaidie pia wananchi wa Idweri kuelekea Ngumbulu ili barabara ile pia ipitike kwa muda wote wananchi waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *TARURA* ninayo changamoto kidogo, Rungwe ni wilaya ambayo ina mvua nyingi. Tuna mtandao wa barabara zaidi ya kilometa 1,300 tuna mvua za kutosha, barabara nyingi zinaharibika lakini bajeti yetu ambayo tunapata ni zaidi ya shilingi bilioni 2. 5 ambayo ni ndogo sana kwa Rungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kama kuna uwezekano *formula* ya ugawaji wa fedha za barabara iweze kuangaliwa upya kwa sababu Rungwe ni kubwa lakini kipato tunachopata bado hakitoshelezi katika utendaji wetu wa kazi. Kwa hiyo, naomba hiyo tuliangalie tuone ni jinsi gani, pia hata fedha zinazopatikana za barabara kwa sababu ya hali ya hewa ya Rungwe ziweze kuletwa mapema katika maeneo yetu, zitumike mapema kwa sababu ikishaanza mvua tu utekelezaji wa barabara unakuwa tayari ni shida kubwa katika Jimbo langu la Rungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya mwaka jana tulipata na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais tumepata vituo Vitatu vya afya Bilioni 1.5. Tulipata Kituo cha Ipojora, tulipata kituo cha Ndanto, tulipata kituo pia cha Kiimo ambavyo vyote vimeishakamilika na vifaa tiba vimeishakuja. Wananchi wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwamba kazi sasa imeishaanza kufanyika na wananchi pale wanapata matibabu karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia bajeti ya mwaka huu pia tumepata vituo viwili vya afya, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwamba tumeletewa pesa Bilioni Moja

ambayo itaenda kutusaidia wananchi wa Rungwe kuweza kupata huduma kwa karibu katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hospitali yetu ya Wilaya tumepewa bilioni moja kumalizia jengo la *OPD* pamoja na Wodi kwa ajili ya wagonjwa zaidi ya 90, pia tunashukuru sana katika hilo kwamba Serikali imetufikilia kutusaidia katika kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana kengele ya pili imelia, tunaendelea na Mheshimiwa...

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa ahsante, naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Vincent Mbogo ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi nichangie katika mjadala huu wa Wizara ya TAMISEMI.

Kwanza, nami nichukue fursa hii kwanza kupongeza utendaji mzuri wa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake Naibu Mawaziri pamoja na Katibu Mkuu na Makatibu Wakuu, kwa kweli tunayo imani kubwa na tunawaomba waendelee na moyo huo wa utendaji mzuri ambao tunauona. Vilevile pia nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu ambae kwa kiwango kikubwa anatuheshimisha bajeti hizi kwa kipindi hiki akiwa madarakani miaka miwili sasa, tunaona jinsi ambavyo zinaelekea kwenye maisha halisi ya mwananchi, kwenye maeneo ambayo ndiyo tunamkuta Mtanzania, kwenye elimu, afya, kwenye barabara ndiko tunako mkuta mwananchi halisi wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Waislam wa Mkoa wa Singida ambao jana walifanya maandamano kupinga suala la zima la mmong'onyoko wa maadili hapa nchini, ambayo hivi sasa tunaona kuna nia ovyo inayofanywa na baadhi ya watu kutaka kuteketeza kizazi, kuteketeza maisha ya mwananchi au maisha ya binadamu ambayo ni tunu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Nawapongeza sana Waislam wale wa Mkoa wa Singida pamoja na Viongozi wa Dini kwa ujumla hapa nchini hata Mkoa wa Singida Maaskofu nao wametoa matamko na wamesema kwenye maeneo yao, nawaomba waendelee na moyo huo na wasiache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Spika, ambaye pia alitoa mwongozo kuhusu suala hili hapa nchini na naomba Serikali ichukue hatua wasibaki kujitafuna na kumung'unya maneno wakati tayari wanayo mamlaka ya kushughulika na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie upande wa eneo la afya kwenye Jimbo langu la Singida Kaskazini. Kwa nafasi ya kipekee sana nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumshukuru kwa fedha nyingi ambazo ametupa kwenye eneo la afya kwenye Jimbo la Singida Kaskazini. Tunayo Hospitali ya Wilaya na sasa ina vifaatiba na kazi inaendelea kufanyika, pia tunavyo Vituo vya Afya, Kituo cha Afya cha Makuro nacho kimeanza kufanya kazi Tarehe 03 Machi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa kwa kipindi hiki kifupi tumeshajenga zahanati Tisa na baadhi zinafanyakazi ikiwemo ya Mwachambia, Unyampanda pamoja na zahanati ya Mwakichenche. Ninaipongeza Serikali kwa eneo hili, ninaomba bado ninayo maeneo ya changamoto kuna Boma la Kituo cha Afya pale Ngimu, hili boma lina miaka 14 sasa, ameishafika Katibu Mkuu wa CCM ameona na amepita pia Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa ameona na alitoa

machozi baada ya kuona nguvu kazi za wananchi zimepotea kwa muda mrefu lakini Serikali haijawapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake walione hili. Eneo lile ni *tense* liko kwenye mazingira magumu ya Bonde la Ufa wananchi wanateseka kupanda Milima kufuata huduma za afya mbali. Naomba Serikali iwapokee wananchi hawa, iwaokoe mama zetu wanaoteseka wakati wa kujifungua. Watoto wanaohangaika na huduma za afya pamoja na Wazee wasiyoweza kutembea, niombe sana Serikali ilichukue hili na nione kwenye bajeti hii fedha zije zijenge Boma lile la Kituo cha Afya *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Kituo cha Afya Kinyagigi nalo naomba fedha pamoja na boma la zahanati pale Sagara naomba nako fedha zije pamoja na Mwakichenche pale Minyenye. Eneo hili la afya ninaiomba Serikali itupatie *ambulance,* kuna umuhimu mkubwa sana tupate *ambulance* kwa sababu maeneo haya kama nilivyosema tumepata zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali ya Wilaya hakuna *ambulance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye eneo la *TARURA* ninashukuru sana kwa fedha ambazo zimekuja kwenye eneo la barabara mpaka sasa tunapokea Shilingi Biloni 2.2 kwenye miundombinu ya barabara upande wa *TARURA*. Ninaomba fedha ziendelee kuja na *TARURA* iendelee kuongezewa fedha lakini na wao waendelee kuboresha madaraja, waendelee kuboresha mitaro ile ya kutiririsha maji, wafanye kazi kwa ufanisi *value for money* tunataka tuone fedha zinazokuja zifanyiwe kazi ipasavyo ili kuondokana na kero ambayo wananchi wamekuwa wakiipata kwenye eneo la miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili *specific* naomba nizungumzie ile barabara inayotoka pale njia panda Mgori kwenda Mughunga mpaka Mukulu, Nduamughanga barabara kipande cha kilomita 25 kutoka Nduamughanga kwenda Mukulu ambapo ndiyo tunakutana na Wilaya Chemba, eneo lile ni baya, lina madaraja Saba ni eneo fupi sana kilomita 25 lakini ni maporomoko, mito naomba sana barabara hii ipate fedha za ziada mwaka huu ili iweze kutengenezwa na madaraja yale yaweze kuimarishwa ili kuwaunganisha wananchi wale na wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie maeneo ya Miji yanayokua. Mji wa Ilongero ambapo ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri hakuna barabara hata kidogo, niombe sasa tupatiwe fedha kwa ajili ya kuboresha barabara za ule Mji ili uweze kuwahudumia wananchi ipasavyo wanaotoka Kanda zote za Wilaya ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe madaraja mahusisi, daraja la Mpambano nashukuru limepatiwa fedha Shilingi Milioni 650 kupitia ule mapango wa Mama wa *World Bank* lakini sasa niombe fedha kwenye daraja la Mgori, daraja lile limekuwa likiua watu, wananchi wamekuwa wakizama pale na limekuwa likikata mawasiliano ya wananchi hasa wakati wa mvua. Niombe sasa tupatiwe fedha na kwenyewe tukalijenge lile daraja. Kama haitoshi daraja lile la pale linalounganisha Minyaa na Mwanyonye daraja lile ni baya limekuwa likitutesa, naomba nako tupatiwe fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu ninashukuru kwa fedha za mradi wa *BOOST* shule mbili za msingi tumepata lakini niombe sasa ujenzi wa nyumba za Walimu pamoja na vyumba vya madarasa lakini na madawati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abeid, muda wako umeisha ahsante sana.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana ninaunga mkono hoja lakini naomba *next time* mtupe muda wa kutosha angalau dakika kumi na kuendelea. Ahsante sana. *(Makofi*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea. Nilimtaja Mheshimiwa Vincent Mbogo, Mheshimiwa Charles Kajege nae ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara ya TAMISEMI. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea fedha nyingi sana pamoja na miradi hasa katika Majimbo ambayo yalikuwa yamesahaulika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubali ukweli Wabunge tunatoka kwenye Majimbo ambayo yana historia tofauti. Jimbo la Nkasi Kusini lilikuwa halina miundombinu, miundombinu imeanza kujengwa ndani ya kipindi cha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Nkasi Kusini lilikuwa na Kituo cha Afya kimoja tu, nacho kilikuwa hakijakamilika kwa hiyo ina maana mimi nimeingia ndani ya Jimbo la Nkasi Kusini halina Kituo cha Afya na lina Kata 11 na umbali wa kutoka Kata moja kwenda Kata nyingine kuna umbali wa kilomoita 40 mpaka 50, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naomba mgao wa Kata ili huduma za kijamii wananchi waweze kupata kwa uraisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu linapakana na Nchi za Jirani Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Kule kuna makambi ya wavuvi ni maeneo mazuri sana kwa uchumi lakini wananchi wamekuwa wanaishi katika mazingira ambayo kuna uhalifu wa mara kwa mara, ndani ya miaka mitatu wamevamiwa mara sita. Vipo Vijiji karibia ishirini

ambavyo viko mwambao wa Ziwa Tanganyika ambapo hali ya hewa ikichafuka, Ziwa likichafuka usafiri wao ni ndani ya Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawana mbadala kwa hiyo wakinamama wajawazito wanapoteza maisha, wakinamama hawapati huduma ya afya na hata huduma za jamiii ambazo Mheshimiwa Rais anatoa kwa ajili ya maendeleo kufika kwake tu kule hakuna barabara, hakuna miundombinu. Mheshimiwa Rais ametoa magari ya kuchimba visima, tulikuwa tunajadili na Wakurugenzi wa Maji, namna ya vifaa vile kufika kule kuchimba visima hakuna kwa sababu hakuna barabara. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tena nikushukuru sana hiyo timu mnaenda kwa kasi mmevaa kiatu cha Mheshimiwa Rais, nawapongezeni sana. Kwanza ni wasikivu, mlituita tukakaa tukawapa vipaumbele vyetu vya Majimbo na tumeishawapa tunaomba mtekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini lina Vijiji ambavyo havina maboma, vingine vina maboma wananchi wamejitolea kwa nguvu zao, maboma ya zahanati na maboma ya shule pia baadhi ya shule hazina madawati nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, mje na mkakati maalumu kwa sababu ya kuleta madawati pamoja na viti shule za msingi kuna hali mbaya sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shule ambazo watoto mpaka sasa hivi wanasoma chini ya mwembe (chini ya mti) na huo ni mfano wa Kijiji cha Tundu, Mkomachindo, Kapumpuli, Kilambo cha Mkolechi, Tuondokazi, Msamba, Lyela, Mwinza, Izinga, Katani, Kata, Yapinda, Isambara, King’ombe kuna Vijiji ishirini wanafunzi wanasoma chini ya mti Pamoja, kijiji kimoja wanafunzi wanasoma chini ya mwembe, vijiji vingine wanakalia mawe! Karne ya Ishirini na moja wanafunzi wanakalia mawe hata elimu wanayoipata wanaipata katika mazira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais ametangaza hizi ajira ninakuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu kuna mazingira ambayo ni magumu, tuleteeni fomu sisi Wabunge, tumepita huko kero na mazingira tunayajua tujaze fomu mazingira yale ambayo watumishi waende moja kwa moja. Kwa sababu mkiwapeleka kule wataishia Mjini wata robu kwa hiyo wanafunzi wa nchi hii hawatapata haki ya walimu wanao husika kwa sababu kuna shule nyingine kuna mwalimu mmoja nyingine hakuna wana azima kutoka shule jirani kwa hiyo ajira hizi tuleteeni fomu tuwape vipaumbele vya maeneo yetu yenye changamoto ili mnapo ajiri waende moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo ahadi za viongozi, ahadi za viongozi hizi wanapofika kwenye Kata zetu wananchi wana amini sana Viongozi Wakuu wa Nchi yetu. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye kampeni alihaidi Ujenzi wa Kituo cha Afya Tarafa ya Chala ni Makao Makuu ya Tarafa ambapo Kata hii Kituo chake hiki kina hudumia Kata Tatu. Kina hudumia Kata ya Ntuchi, Kata ya Katumbila na Kata ya Chala, ambazo mpaka sasa hivi kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini bado hakuna kinachoendelea, akaja Mheshimiwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Chama Mheshimiwa Daniel Chongolo nae kahaidi Ujenzi wa Kituo cha Afya Chala nacho bado, akaja Mheshimiwa Waziri Mkuu kapita napo katoa maagizo kijengwe Kituo cha Afya Chala pia Hayati Mheshimiwa John Pombe Magufuli nae alitoa ahadi ya Ujenzi wa Kituo cha Afya Chala bado mpaka sasa. Ahadi ya Viongozi Wakuu wa Nchi karibu watatu bado maandalizi Mheshimiwa Waziri, naomba Kituo cha Afya Chala kianze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo Kata ya Sintali, Miula wananchi wanapata huduma ya mbali sana wanatoka maeneo wanatembea karibu kilomita 20 mpaka 40. Naomba Kata ya Sintali, Kata ya Miula pamoja na Kata ya Chala

ijengewe Vituo vya Afya. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Vincent Mbogo. Nilimtaja Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Oliver Semuguruka ajiandae.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika hotuba ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Kama walivyofanya watangulizi wangu na mimi napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana ambayo amefanya katika kipindi hiki kifupi. Katika kipindi hiki kifupi tumeona miradi yote mikubwa inaendelea kutekelezwa kawa kasi kubwa na kwa ubora wa hali ya juu, mahusiano yetu na nchi zingine za nje yamepanuka zaidi na kukua zaidi, biashara yetu ya nje na ya ndani imekua na kupanuka zidi yote hii katika kipindi kifupi hiki cha utawala wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa TAMISEMI na timu yake kwa uongozi mzuri ambao wamefanya katika kipindi hiki kifupi. Kama walivyozungumza wezangu imekuwa ni raisi zaidi kumpata Mheshimiwa Waziri Kairuki, muda wote ukimpigia simu anapokea simu na bado anakuletea mrejesho ambao ni mzuri. Nakupongeza sana Waziri wetu Kairuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Mwibara nitazungumzia baadhi ya changamoto ambazo ndiyo kikwazo kikubwa katika maendeleo yetu. Changamoto ya kwanza ipo katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitembelea katika shule za Mwibara nyingi hasa shule za msingi utakuta kuna upungufu

mkubwa sana wa vyumba vya madarasa na hata vile vyumba vya madarasa viliyopo bado vimechakaa sana, wanafunzi katika chumba kimoja utakuta ni zaidi ya mia moja, vilevile vyumba hivi vingi havina sakafu kwa hiyo watoto wanasoma katika vumbi. Shule hizi ni kama Shule ya Msingi Gundu, Chitengule, Nampangala, Igundu, Buyomba, Susi, Bwanza, Shabirizi, Visambu, Bunele, Mlagata, Kinkombe na Kabaija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kutembelea katika hizi shule ni kama hazipo, kwa sababu majengo ni mabovu na mengine sasa hivi hawaruhusiwi hata watoto kuyatumia, kwa hiyo ni kama majengo hayapo. Vilevile upungufu wa madawati madarasa mengi hayana madawati kwa hiyo wanafunzi wanasomea chini. Sasa ukiangalia kwamba madarasa kwanza wanafunzi wako wengi katika darasa moja vilevile ni kwamba hawana madawati *plus* kwamba hata sakafu hazipo, ni chafu, ni vumbi kwa hiyo mazingira ya kusomea hawa wanafunzi yanakuwa ni magumu sana. Sasa inakuwa ni vigumu kumchukua mwanafunzi anatoka katika madarasa haya aka–*compete* na wanafunzi wengine ambao wanatoka katika mazingira mazuri sana ya elimu, kwa hiyo lazima naiomba Serikali iweze kuangali hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kingine ni upungufu wa walimu. Katiba hotuba ya TAMISEMI Mheshimiwa Waziri amesema kuna upungufu wa Walimu zaidi ya 89,932 katika shule za msingi wanaokuja kuajiriwa mwaka huu tunaona ni kama 13,000 peke yake ambayo ni sawa sawa na asilimia 14 hawa walimu ni wachache sana hawatoshi. Nilikuwa naomba Serikali yetu ifikilie namna ya kuongeza walimu, kwa sababu kama hatuna walimu hizi shule tunatoa elimu ya namna gani kama hatuna walimu na tulikubaliana kuanzia mwanzo kwamba mojawapo ya maadui wetu ni ujinga sasa hatutoweza kutoa ujinga kama walimu hawatoshi katika mashule yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ina changamoto ni katika sekta ya afya. Kwa sasa hivi ninavyo vituo Vitatu vya Afya Kisolya, Kasaunga, Kasuguti lakini bado havijakamilika, hivi bado havina majengo kutosha, vifaatiba havipo na wauguzi hawatoshi. Ningeomba sana Serikali ifikirie namna ya kuvikamilisha vituo hivi ili viweze kutoa huduma inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna maeneo ambayo sasa huduma ya afya iko mbali sana, kwa mfano Kata ya Igundu na Kata ya Namuhula nilikuwa nasikia kwamba Serikali ifikirie kujenga vituo vya afya katika Kata hizo mbili. Vilevile mwaka jana wakati ziara ya Mheshimiwa Rais katika Wilaya ya Bunda Tarehe Saba Februari, alielekeza kwamba hospitali ya Halmashauri nyingine ijengwe katika Jimbo la Mwibara, hilo agizo bado halijatekelezwa naomba hii Wizara ifikirie namna ya kujenga hiyo hospitali mapema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni michango ya wananchi kusaidia katika miradi ya maendeleo. Sina tatizo na michango, lakini tatizo langu ni kwamba michango mingine imekuwa ya holela. Kwa mfano, juzi nilipokuwa Jimboni, nilipita katika Kijiji kimoja cha Busambara. Hawa wameletewa pesa shilingi 54,824,000 kujenga matundu 20 ya choo. Wananchi wameombwa kuchangia tena shilingi 15,000 katika kila kaya. Nikawauliza, hivi gharama ya choo kimoja, tundu moja ni kiasi gani? Wakasema ni shilingi 1,500,000. Sasa kwa hesabu rahisi ni shilingi milioni 30. Nikawauliza, hizi Shilingi milioni 24 zinazobakia zinakwenda wapi? Hawakuwa na jibu. Nikawaambia wananchi msichange, hizo pesa zinatosha. Nilikuwa naomba, Serikali yetu iangalie vilevile kuhusu uchangishaji holela kutoka kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, bado kuna upotevu wa pesa katika Jimbo langu. Kuna wizi tuseme, kwa mfano, kuna shilingi milioni 300 ambazo zimepelekwa katika Kituo cha Afya cha Kasuguti, hazijulikani zilipo; kuna shilingi milioni mbili

nilitoa katika Kata ya Nyamihoro kutoka katika mfuko wangu wa Jimbo, hazijulikani zilipo; kuna Shilingi milioni moja ilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa choo katika Shule ya Msingi ya Msambara, *VEO* kakimbia nazo hazijarudi; na vilevile nilitoa shilingi 500,000 kwa ajili ya Nyamihoro na zenyewe hazijulikani zilipo. Naomba sasa wakati wa majumuisho nipate majibu ya nini kinafanyika au tutapataje hizi pesa ziweze kufanya maendeleo katika jimbo langu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuanzishwa kwa kidato cha tano katika Shule za Sekondari za Nansimo na Buramba. Katika Shule ya Nansimo miundombinu imetosha, yaani kuna mabweni na madarasa, yanatosha; lakini katika Shule ya Buramba kuna madarasa lakini hakuna bweni. Nilipoongea na Afisa Elimu, akasema kwamba haiwezekani kuanzisha Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari ya Buramba kwa sababu hamna bweni. Mimi naona hilo siyo tatizo, haya mambo tumeambiwa kuanzia miaka mitano iliyopita mpaka leo na shule haijaanzishwa. Naomba tuanzishe Kidato cha Tano, bweni litatufata baadaye. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWNEYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

**MWNEYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mheshimiwa Isack Francis Mtinga ajiandae na mchangiaji wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya TAMISEMI. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya katika Taifa letu. Pia nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI, wifi yangu Kairuki na Manaibu wake pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu. Nawapongeza sana. Pia nampongeza Mkuu wangu wa Mkoa, Albert Chalamila, anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Mkoa wetu wa Kagera, anafanya kazi asubuhi, mchana na jioni. Nampongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye mchango wangu. Ujenzi wa madarasa ya msingi na sekondari, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ujenzi huo. Hata hivyo, kuna changamoto ambayo ipo kwenye shule hizo ambayo ni matundu ya vyoo. Kwa kweli shule nyingi zimejengwa lakini matundu ya vyoo ni machache sana, nilikuwa naomba sana Serikali iweze…

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji anayechangia kuwa, kazi kubwa sana imefanywa kujenga madarasa na miradi mingi, na Mkoa wetu wa Arusha ni mfano wa Mkoa mmoja, na yote hayo yamefanywa chini ya Mkuu wa Mkoa John Mongella. Tunampongeza sana na tunakushukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuletea John Mongella. *(Makofi)*

**MWNEYEKITI:** Mheshimiwa Oliver, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili na John Mongella alikuwa ni Mkuu wetu wa Mkoa wa Kagera kabla hajaenda huko. Namjua ni jembe sana, kwa hiyo, naipokea sana taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka kwenye matundu ya vyoo, naomba nijielekeze kwenye nyumba za watumishi. Kwa kweli waalimu wanapata shida sana. Tumejenga madarasa ya kutosha katika shule za sekondari na shule za msingi, lakini waalimu hawana nyumba za kuishi. Unakuta mwalimu anatoka kilomita kama 10 au 20 kutoka sehemu *A* Kwenda *B,* anafika shuleni ameshachoka, atafundishaje wadogo zetu na watoto wetu kwa weledi sana? Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ijielekeze kwa nguvu zote kwenye ujenzi wa nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile walimu wanatakiwa wawe na mazingira mazuri, wakitoka shuleni kuna jinsi ya kuandaa andalio la kesho yake, na kuandaa *notes.* Anatoka shuleni ametembea kilomita saba au kilomita 10, anakuwa ameshachoka chakari. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu sikivu iweze kujenga hata nyumba za watumishi hasa za walimu wa shule za msingi, kwa kweli wanapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa watumishi. Mheshimiwa Waziri naomba kipaumbele kwenye ajira hizi wanazoajiri wapewe wale ambao wanajitolea. Unakuta mtu amejitolea zaidi ya miaka mitatu, lakini ajira zikitokea hayupo.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja, kuna shule moja ya Ngara; Shule ya Msingi Nyamiaga, kuna mwalimu ameshajitolea zaidi ya miaka mitatu, lakini huyo mwalimu kila akiomba nafasi zikija jina lake

halipo. Kwa bahati nzuri, hakati tamaa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali yetu sikivu iwaone kwa jicho la pekee, hawa walimu wanaojitolea, kwa upande wa afya pia, waweze kuwapa kipaumbele kwa ajira hizi ambazo zimetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pia nilikuwa naomba katika hizi ajira, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Kairuki wakati anasoma hotuba, kwamba wakishaajiri hawawezi kukuhamisha kabla ya miaka mitano. Nilikuwa naomba iwe hivi, kwa mfano kama Kagera waajiri kikanda. Wakiajiri kama ni mwalimu, wameshaona kwenye *database* ni wa Kagera, basi wamwajiri Mwanza au Geita au Kahama ili iwe rahisi hata kwenda kuona familia yake, wasianze kusumbua kwamba naomba uhamisho. Kwa mfano, umemtoa Kagera, umemepeleka Mtwara. Umemtoa Kagera, umempeleka Songwe, kwa kweli inakuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, naomba katika hizo ajira wazingatie sana Kanda ili kupunguza kusumbuliwa katika mambo ya uhamisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri waangalie katika ajira hizi, pembezoni huku, kwenye Halmashauri za vijijini unakuta hakuna waalimu, hakuna watu wanaoenda huko; kila mmoja anakataa. Kwa mfano, ukimwajiri mtu ambaye yuko Kagera ukampeleka Wilayani kule pembezoni, ataenda tu, lakini umtoe Kagera, umpeleke Songwe huko karibu na Zambia, kwa kweli inakuwa ni changamoto. Ndiyo hii inaanza kuleta usumbufu kwa ajili ya kuomba uhamisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najielekeza *TARURA*. Kwa kweli *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana. Wana muda mfupi lakini kazi zinaonekana. Changamoto kwa *TARURA* ni bajeti. Mfano kwa Mkoa wangu wa Kagera, nilikuwa naomba, kuna Kivuko cha Nyabasa kiko Wilaya ya Bukoba Vijijini. Hicho ni kivuko ambacho tunategemea tujenge daraja. Nilikuwa naiomba Serikali yangu Sikivu, na Mheshimiwa Waziri wa

TAMISEMI, huko ndio nyumbani kwenu pia. Naomba sana kuharakisha usanifu na ujenzi wa Daraja la Chanyabisa la Halmashauri ya Bukoba. Mwaka jana 2022 kuna gari ilitumbukia kwenye hicho kivuko, likakaa *almost one-week* mle, bila kutolewa.

**MBUNGE FULANI:** Uuh!

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Kwa kweli ni shida. Ukitupatia bajeti ya kutosha, daraja likajengwa, italeta tija pia kwa wananchi na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza bajeti kwa ajili ya ujenzi pia wa barabara za ulinzi na usalama katika Wilaya za mipakani hasa kule kwetu Ngara, Kyerwa na Missenyi, tujenge barabara ambazo zitakuwa ni za usalama zaidi. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iweze kutupatia bajeti ya kutosha katika hii *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Missenyi na Bukoba vijijini naomba zipatiwe fedha maalum *(special fund)* kwa sababu kule barabara zake hutengenezwa kwa bajeti ambayo ndiyo hiyo ya *special fund*. Barabara ni tambarare, mvua zikinyesha maji yanajaa, wananchi hawawezi kwenda upande *A* na upande *B*, yaani inakuwa ni changamoto kubwa sana. Tukipata bajeti ya kutosha, watatengeneza barabara ziinuke ili mvua zikinyesha sana maji yasituame na kusababisha wananchi kushindwa kwenda kwenye shughuli zao katika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha! Eh, mh!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani! Naunga mkono hoja. Mengine nitaandika kwa maandishi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Oliver. Nilimtaja Mheshimiwa Isack Francis Mtinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu inayogusa maisha ya Watanzania, Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja kwa sababu muda wangu ni mfupi, na ninataka nijikite sana kwenye suala la ugawaji wa maeneo ya kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesimamisha muda mrefu sana suala la ugawaji wa maeneo ya kiutawala. Zipo Kata zetu ni kubwa mno kiasi kwamba wananchi wanapata taabu sana kufuata huduma. Nikitoa mfano, Kata yangu ya Mwangeza, kutoka mwanzo wa Kata mpaka mwisho wa Kata ni takribani kilomita 70. Kata kama hii yenye wananchi takribani 30,000 ina vijiji sita tu. Kutoka Kijiji mpaka Kijiji hakuna barabara. Mtu akitaka kwenda Kijiji kingine aje Makao Makuu ya Wilaya ndiyo aende Kijiji kingine. Kwa hiyo, wananchi wanapata taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sensa za mfano, kwenye Kitongoji kimoja tu, kwa mfano cha Gajaroda katika Kata hii kulikuwa kuna kaya 280. Kitongoji kama cha Msanga kaya 265, na Kitongoji cha Midibwi kaya 315. Unaweza ukaona kwamba hivi ni Vitongoji, maeneo mengine kaya 300,

unaongelea Kata. Sasa tunapokuwa hatugawanyi maeneo, tunawatesa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia maeneo ya utawala ndipo wananchi wanakopata huduma. Sasa wapo wananchi kuna maeneo yao ni madogo tu, wana vijiji vya kutosha, wana mitaa ya kutosha, wana-*enjoy* hii nchi nzuri inayoongozwa na Mama Samia anayemwaga mambo huku. Sasa inapokuja kwenye Kata hizi kubwa ambazo hazigawanywi, wananchi wanapata taabu, hawafurahii maisha mazuri ya Watanzania. Kwa sababu mtu anasafiri umbali mrefu kufuata shule, kufuata hospitali na Mahakama; na hivi vitu viko kwenye maeneo ya kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara sasa ifuatilie maombi ambayo tumeshayatuma mengi, ambayo tumeyaleta mara nyingi, yanawekwa kapuni. Mfano, tumesema kata kama hii, tunataka tupate Kata ya Dominiki, tupate kata ya Endasiku na tupate Kata yenyewe ya Mwangeza kutoka kwenye Kata moja. Kata kubwa kama ya Ibaga, tunataka tupate Kata ya Ibaga na Kata ya Mkalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya tunayoongea kama ni Matawi ya Chama, tunaongelea matawi mpaka 15, au 20, tunapata shida. Kwa hiyo, namwomba Waziri suala hili alichukulie umuhimu mkubwa. Nimeamua nibaki kwenye eneo hili kwa muda mrefu kwa sababu tumekuwa tunalisema tu na kulipapasa, hebu tugawe maeneo ili wananchi wapate huduma nzuri ambayo Rais wetu anaitoa, kwa sababu bila kugawa maeneo, huduma hizi haziwafikii, wananchi wengine anateseka maporini kwa sababu Serikali iko mbali na maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa nataka niseme kuhusu uhaba wa watumishi. Naomba wakati Waziri ana-*wind up* atueleze, hivi ni kwa nini tunashindwa kujaza

ma-*gap* ya wafanyakazi ambao tayari walikuwa kwenye bajeti? Wafanyakazi waliostaafu na waliotangulia mbele ya haki. Kwa sababu mtu anapostaafu, anastaafu katikati ya mwaka; au mtu anapofariki, kifo ni ghafla, tunaweza tukapitisha bajeti leo, mtumishi akafariki kesho; tayari yuko ndani ya bajeti. Kwa nini, tusitumie kanzidata kujaza yale ma-*gap* kwa sababu tayari wako kwenye bajeti, ili Rais anapotangaza ajira mpya ziwe ajira mpya kweli? Kwa sababu hizi ajira mpya zinaishia kujaza ma-*gap* tu ya wastaafu na watu waliofariki, matokeo yake hatuoni ajira mpya zinafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waziri atueleze, tatizo ni nini? Kama tumeshapitisha bajeti ya watumishi kwa mfano 1,000, wakafariki 50, si wajazwe wale 50 kwa sababu wako kwenye bajeti? Hii ikiendelea tutapunguza hili *gap* la watumishi, kwa sababu wastaafu wanastaafu kila siku. Watu wanatangulia mbele ya haki kila wakati, lakini nafasi zao wako kwenye bajeti hazijazwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuelezwe tatizo liko wapi? Kama tumeshapitisha bajeti, tutumie kanzidata, mtu aandikiwe tu barua, nenda karipoti mahali fulani. *Interview* zinafanyika kila wakati, kwa hiyo, tunayo *list* ya watu wamesoma hawa, kuna walimu hawa, kuna manesi kuna madaktari, mtu anaandikiwa tu karipoti ujaze *gap,* ili hizi mpya zinapotoka ziwe mpya kweli. Hizi ajira tunasema mpya, siyo mpya hizi, kwa sababu ma-*gap* yamejaa kote huko. Kwa hiyo, hakuna cha ajira mpya, ndio maana tatizo hili halipungui kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, naomba kabisa Waziri akija, aliambie Bunge hili, kwa nini hatujazi ma-*gap* wakati watumishi tunao na bajeti tunakuwa tumeipitisha? (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la watoto wetu kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Tatizo hili ni kubwa. Leo ukienda kwenye shule za msingi unaweza ukakuta zaidi ya watoto hata nusu, hata robo tatu au robo darasa, hawajui

kusoma na kuandika. Hili tatizo halisababishwi na watoto. Watanzania hatuna watoto wajinga wa kutokujua kusoma na kuandika. Haya yanasababishwa na matatizo mengine ambayo pengine sisi hatujayapa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo mojawapo kubwa kabisa ni la utoro; watoto kukosa chakula cha mchana shuleni. Watoto kama hivi hatugawanyi maeneo, wanakaa mbali. Mtoto anasafiri kilometa sita mpaka saba au 10, anaenda shuleni hajala; anafika anakaa shuleni muda wote hajala. Kwa hiyo, naomba hili tatizo la kutokuwapa watoto chakula kutoka shuleni, Wizara iliangalie upya.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mtoa taarifa, yuko wapi? Mheshimiwa Amar.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, KKK inasababishwa na upungufu wa waalimu na pia tatizo hilo la chakula. Nilikuwa nataka nimpe tu taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine walishachangia, naomba unilinde muda wangu hata dakika moja nimalizie.

**MWENYEKITI:** Malizia dakika moja basi.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, tungeweza kupata chakula shuleni pia kupitia kuwafundisha watoto wetu somo la *EK* ambalo limefutwa. Shule zetu zina maeneo makubwa ya kulima, lakini watoto

wetu tumeacha kuwafundisha *EK,* kwa hiyo, tukirudisha lile somo tukawafundisha watoto wetu jinsi ya kulima vizuri kisasa ili wakitoka wakasaidie jamii, watapata chakula na wazazi tukichangia kiasi kidogo kilichobaki watoto wetu wapate chakula shuleni, tuondoe hili suala la kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Linatutia aibu nchi yetu na Mama yetu anamwaga fedha huko kwa ili ya watoto wasome lakini watoto wetu wanakuwa hawajui kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mhehsimiwa Isack. Tunamalizia na mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Taifa letu. Vilevile naipongeza Wizara ya TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri, Manaibu na timu nzima na vipaumbele vyao 19 walivyoviainisha kwenye bajeti hii ya 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye mikopo ya asilimia 10. Ni kweli fedha nyingi zimepotea kwenye mikopo hii na sababu kubwa za msingi zinasababisha kwanza ni wahusika na wasimamizi wa mikopo hii kutokuwa waaminifu, hali iliyopelekea kuwa na utitiri mkubwa sana wa vikundi hewa. Vile vile wanufaika wa mikopo hii, wengi wao hawana elimu ya fedha, hawana elimu ya ujasiliamali, yaani ni watu tu kujikusanya; watu watano kutengeneza kikundi, wanapata fedha. Pia maandiko mengi; wanahamasishwa kuandika maandiko ya viwanda vya ufyatuaji matofali, ununuzi wa magari, kilimo cha mjini *(green house)*, na ufugaji wa ngombe wa kisasa. Sasa hivi vitu vyote siyo kweli kwamba

mtu anapewa mikopo wiki hii, wiki ijayo anaweza kufanya haya. Hivi vyote vinahitaji elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona mikopo hii sasa itoke Halmashauri ipitie kwenye taasisi za Kifedha. Naomba, tumeshaona udhaifu mkubwa kwa vikundi hivi vya watu watano watano, kwa nini mikopo hii sasa wasishirikishwe na vikundi vya huduma ndogo za kifedha, hawa ambao ni *VICOBA*? Kwa sabbau ni vikundi ambavyo vinazungusha hela zao benki. Wananunua hisa zao, wanakopeshana wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona vikundi vidogo hivi vya watu watano watano wakipata zile fedha, walikuwa wanagawana mtu mmoja mmoja, matokeo yake wanashindwa kurudisha, lakini vikundi vya huduma ndogo za kifedha, wale tayari wana fungu lao ambalo wanakopeshana ndani ya kikundi. Ni vikundi ambavyo vina miaka mitano, miaka kumi na wana uwezo wa kukopeshana Shilingi milioni tano, milioni 10 mpaka milioni 20 kwa mtu mmoja. Kiu yao na malengo makubwa ni kufanya mambo makubwa sasa; kufungua viwanda, kufungua makampuni na biashara kubwa kwa ajili ya vikundi. Sasa kwa nini fedha hizi zinazopotea wasiingize na hawa wakawa wanufaika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa wanapeleka fedha zao benki, marejesho yao yanapitia benki na benki wanaona kabisa *cashflow* yao inavyokwenda, ni rahisi zaidi hata marejesho kukatwa kule. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, vikundi vya huduma ndogo za kifedha wanatamani nao wakawa wanufaika wa mikopo hii ili wafungue viwanda, akina mama wapeane ajira. Watoe ajira kwa vijana, hata kwa watu wenye ulemevu, wote wapo kwenye vikundi vya *VICOBA* wanahitaji mikopo hiyo wafanye vitu vikubwa. Lengo lao siyo kukopeshana, wana malengo ya kufanya vitu vikubwa, lakini mikopo hii haiko wazi kuonesha

kwamba wao ni wanufaika. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho, tunaomba aliweke hili wazi: Je, vikundi vya huduma ndogo za kifedha ni wanufaika wa hii mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa tunaiomba Wizara itakapokaa na mabenki kuweka utaratibu, wekeni utaratibu mzuri. Mikopo hii wapate watu sahihi kabla ya kupata mikopo watu waandaliwe kwanza *at least* hata miezi miwili, mitatu. Siyo kweli, elimu ya wiki moja tu, mtu anapewa fedha, anaweza. Kuna wanufaika ambao ukiwafuata huko mtaani, ukiwauliza kwa nini hamrejeshi? Anashangaa, lini amepata mkopo? Tunaamini kwa kupitia benki haya yote yatakwisha. Kwa hiyo, tukuombe Mheshimiwa Waziri, mikopo hii hata kama itapitia kwenye mabenki, lakini bado Halmashauri ina kazi kubwa ya kufanya. Kuwe na utaratibu wa Halmashauri husika kukaa na vikundi; waliopata mikopo, wasiopata na wanaotarajia kupata. Kuwe na elimu endelevu za hii mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kabisa *VICOBA* wanafanya vizuri kuliko hawa; lakini ndio hawa hawa akina mama, ndiyo hao hao vijana na ndio hao hao watu wenye ulemavu. Shida kubwa ni kwamba hawa wanaohamasishwa hivi vikundi vya watu watano kuna kitu hakiko sawa. Unakuta kikundi kimeandikiwa andiko. Ukikaa nao ukiwauliza hili andiko lenu mlikuwa mnataka nini? Hawajui hata wameandikiwa andiko gani? Wanaandikiwa maandiko hawayajui. Wanapewa hela, Halmashauri inajua kabisa tunawapa hii hela hawa, andiko lao linasema hivi, hii hela wana uhakika itakwenda kurudi, lakini hairudi, kwa sababu hata walichoandikiwa hawakijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe suala la elimu na kuandaa watu lizingatiwe sana. Kinyume na hapo, kama mikopo hii itaenda benki, utaratibu usipowekwa vizuri, wanufaika wakawa ndio hawa hawa, na taratibu za benki

zikatumika kama zile za kuwakopesha watu wengine, tunaenda kutengeneza janga kubwa kuliko lile la *PRIDE*. Kwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasisitiza utaratibu, Halmashauri itenge fedha kwa ajili ya kutoa elimu kwa hivi vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba Wizara, tuangalie kada ya akina mama wanaofanya biashara ya Mama Lishe. Tunaona majengo ya biashara makubwa yanajengwa, lakini akina mama hawa hawapewi kipaumbele, hawapewi eneo. Akina mama hawa, wateja wao ndio hao wafanyabiashara. Majengo yanajengwa, wanapewa wafanyabiashara tu, wao wanakosa maeneo; na wengi wana mikopo, wanatakiwa warudishe marejesho. Biashara zao wanunuzi ndio hao walioko hapo. Kwa hiyo, tunaomba masoko yaliyojengwa maeneo ya biashara yaliyojengwa litengwe eneo kwa ajili ya akina Mama Lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nami niungane na wenzangu waliozungumzia na suala la ajira. Mtaani tuna vijana wengi hasa kada ya walimu ambao wanafanya kazi kwa kujitolea. Tunaomba ajira za safari hii zije kitofauti. Hawa wanaojitolea wakapewe kipaumbele; wapate kwanza wao kabla ya wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janeth ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, hapa nimekuwa napata malalamiko ya muda, lakini kutokana na changamoto iliyopo, ni kwamba waliotakiwa wachangie leo walikuwa ishirini na kitu, lakini tumepata wachangiaji 38. Kwa hiyo, kwa

vyovyote vile, lazima muda upungue. Hayo ni makubaliano ya kwenye chama wenyewe. Kwa hiyo, kama mtaona kwamba mnataka muda ule ule, basi mkubaliane na Katibu wenu kwamba wanaochangia wawe wachache ili wapate muda ule ambao unastahiki. Vinginevyo, kama mtataka wote muwekwe siku moja, basi muda kwa vyovyote utapungua. Hiyo ndiyo inavyokuwa na msikate tamaa bado tuna uchangiaji mwingi, na huko mbele tutakuwa na mjadala wa jumla, bado tutaendelea kuchangia. Kwa hiyo, msivunjike moyo kwa muda kuwa ni mdogo.

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo nawapongeza kwa kazi nzuri mliyoifanya tokea asubuhi, Mwenyezi Mungu awabariki sana; pia awabariki viongozi wetu Mawaziri waliokuwa wanapokea michango ya Wabunge kwa umakini wa hali ya juu; na awabariki nyote kwa pamoja.

Kabla sijaahirisha Shughuli za Bunge, nawakumbusha mwaliko wa *Iftar* kwa Waheshimiwa Wabunge wote, Makatibu wote wa Bunge, pamoja na Wakuu wa Mikoa ambao wako hapa Dodoma. *Iftar* hii imeandaliwa na wenzetu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania. Kwa hiyo, tunaomba wote ambao mmealikwa mhudhurie kwenye *Iftar* hiyo.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12:03 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 18 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*